ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma naUtawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando

13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga

29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasiza Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni

52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
56.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Thalathini – Tarehe 26 Julai, 2012.

Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi.

DUA

Mhe. Mwenyekiti, *(Mahmoud Muhammed Mussa)* alisoma dua.

TAARIFA

Mhe. Mwenyekiti: Kabla hatujatoa fursa ya kuanza na shughuli zetu za masuala, leo hapa tumebahatika kupata wageni na wageni wetu wa leo ni ndugu Sada Hama Ali ambaye ni kocha wa timu ya walemavu wa akili akifuatana na ndugu Tifle Mustafa Nahoda, kocha msaidizi. Naomba wasimame pale juu.

Vile vile na mchezaji Ahmada Bakari wa timu hiyo ambaye amepata tunzo ya Dhahabu ya Medali ya Dunia nchini Ugiriki pia amepata tunzo ya mwana michezo Bora ya mwaka tarehe 14/06/2012 amaye anatarajia kwenda nchini Zambia hivi karibuni kwa michezo hiyo hiyo, naomba asimame vile vile. (*Makofi*)

Tulipata na mwalimu wa masuala hayo ya ulemavu sasa sijui kama tunaye hapa karibu inaonekana bado hajafika huyu. Ahsanteni.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 148

Uondoshaji wa Matuta Barabara ya Mahonda

Mhe. Panya Ali Abdalla – Aliuliza:-

Ni muda mrefu sasa wananchi wa Zanzibar kupitia Wawakilishi wao wamekuwa wakilalamika juu ya uwekwaji wa matuta katika barabara zetu kwa kuwa hauangalii umuhimu wa matuta hayo na hata viwango vya uwekwaji wake katika barabara hizo.

Wizara imekuwa ikitoa ahadi ya kuondosha aina ya matuta yale madogo madogo ambayo yamekuwa yakileta athari na usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa barabara hizo. Barabara ya Mahonda kuelekea Donge karibu na daraja la Mwanakombo, yemejengwa matuta ya aina hiyo karibuni tu na kusababisha usumbufu wa hata ajali kwa wanaotumia barabara hiyo.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuendelea kujengwa kwa matuta hayo kunaenda kinyume na ahadi zako ulizozitoa katika Baraza hili tukufu.

(b) Je, ni lini utayaondoa matuta yale ili kunusuru ajali zinazoweza kuepukika hasa kwa watumiaji wa vyombo vya maringi mawili.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 148 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo tumekuwa tukieleza katika Baraza lako hili tukufu, kwamba uwekaji wa matuta barabarani si suluhisho la ajali na hivyo naahidi kuyaondoa

au kuyapunguza matuta hayo kwa baadhi ya maeneo ambayo yameonekana kuwa ni kero kwa watumiaji wa barabara.

(b) Mhe. Mwenyekiti, matuta yaliyojengwa kwenye daraja la Mwanakombo tutayafanyia kazi na kuona malalamiko ya wananchi yanazingatiwa. Ninawaasa watumiaji wa barabara kuzingatia na kuzitunza alama za Barabarani zilizowekwa kwa ajili ya usalama wa utumiaji barabara hizo na si kudai kuwekewa matuta ambayo si suluhisho la ajali za barabarani.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na vyombo vya usalama barabarani itaendelea kuwaelimisha wananchi wote wanaotumia barabara zetu kufahamu umuhimu wa kuzitunza na kuziheshimu alama za barabarani kwani ndio utaratibu uliozoeleka duniani kote.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini pamoja na majibu hayo naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza.
Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa mimi nimeshuhudia mara nyingi katika matuta haya hasa watu wenye vyombo vidogo wakianguka na hata mimi siku moja alianguka mtu mbele yangu nikashuhudia. Nikaona kwamba kweli matuta haya yanaleta usumbufu.

Kwa kuwa ahadi hii Mhe. Waziri ambaye amestaafu alisema kama atahakikisha matuta haya anayaondoa.

(a) Je, kuchelewa kuyaondoa matuta haya huoni kuwa kunawasababishia usumbufu na kunaendeleza mtiririko wa ajali na kupoteza nguvu kazi za taifa.

(b) Je, ni lini hasa Serikali itazingatia kuyaondoa matuta haya kwa haraka. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tuta analolizingumzia Mhe. Mwakilishi ni kweli kwamba lilijengwa wakati huo wakandarasi wetu walikiwa wanaendelea na ujenzi wa daraja husika. Madhumuni makubwa ilikuwa nikuweza kuzidhibiti gari ili zisiweze kusababisha usumbufu wakati wakiwa wanaendelea na ujenzi. Kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi kwamba dhamira yetu ni kulindoa. Mimi nakuahidi kwamba tuta hilo tutaliondoa haraka iwezekanavyo baada tu ya kuweka alama husika ili kuweza kuongoza vizuri kwa watumiaG100
ji wa barabara.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.
Kwa kuwa matuta yaliyopo kwenye barabara inayotoka Mazizini hadi Chukwani hayamsaidii dereva wa gari wala mwenda kwa miguu ni lini Mhe. Waziri atafikiria matuta yale kuyang'oa na kuyaweka matuta yatakayosaidia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, msingi mkubwa wa matumizi ya barabara ni kuona kwamba alama zilizokuwepo barabarani zinaheshimiwa kwa kutunzwa na kwa kufuatwa. Kwa bahati mbaya kwa muda mrefu madereva wetu hawakuwa wakizitii sheria na ndipo hapo serikali ilipoona wajaribu kuweka matuta ili kupunguza ajali ambazo zilikuwa zikitokea mara kwa mara.

Suala la Mhe. Mwakilishi anauliza ni lini tutakwenda kuyatoa matuta hayo yote. Napenda kumuahidi kwamba tutawatuma watu wetu wafanye tathmii yale malengo ya kuwepo kwa matuta kama yamekuja na faida yataendelea kuwepo. Ikiwa hayana faida basi tutayaondoa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Majibu yake mazuri anayotueleza hapa. Kwanza niipongeze sana Serikali kwa kutuwekea matuta kwenye barabara kwa kupunguza ajali.

Mhe. Naibu Waziri mara nyingi sana huwa mnasema mtaweka matuta pale pahali ambapo panapostahiki na panapo skuli na katika wingi wa watu kama soko na sehemu nyenginezo. Je, Mhe. Waziri huoni iko haja pale Kazole kuna skuli ya chekechea kila leo watoto wanapata ajali. Huoni kama ipo haja ya kuweka matuta haraka haraka tukapunguza vifo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa matumizi ya barabara kunaongozwa na sheria, kanuni na alama zilizokuwepo barabarani. Kilio cha Serikali ni kwamba madereva wetu waziheshimu taratibu na sheria ziliopo ili kunusuru ajali. Ni kweli Serikali ilifanya maamuzi kuweka matuta kwa maeneo maalum baada wa kuona athari na usimamizi wetu umekuwa hafifu katika kuwadhibiti madereva na hivyo kupelekea majanga yakiwemo yakiwemo na ajali.

Utaratibu wa kuweka matuta tumeuweleza kwamba maeneo husika, viongozi wahusika watakuja kutuletea maombi na sisi tutakwenda kutekeleza. Lakini kama kuna maeneo ambayo hayajawekwa matuta na tukiona kwamba kuna haja ya kufanya hivyo tutafanya baada ya kukaa na wahusika wa maeneo hayo.

Kwa hivyo nikuombe tu Mhe. Mwakilishi kama kuna skuli ya chekechea ambayo kuna majanga yanatokea ajali tunaomba tuletee *official* na tunakuhakikishia kwamba watu wetu watakwenda kukagua na tutamuomba Mhe. Waziri ayazingatie kwa kuona hatua gani stahiki au maridhawa haichukue katika eneo hili ili kunusuru maisha ya vijana wetu.

Nam 150

Matengenezo ya Uwanja wa Ndege wa Zanzibar

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 -
Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana na namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba amekujaalia leo kuwa ndio muongozaji wa Kikao hichi labda amekufanya hivyo kukusadifu kwamba wewe ni mwanamichezo mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ili lipokee, lijadili na hatimaye lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema kwa kutujaalia kukutana tena tukiwa na afya njema katika nchi yenye amani na utulivu chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya viongozi na wafanyakazi wa Wizara yangu, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, nashukuru sana kwa uongozi wake wa busara, na juhudi zake kubwa anazoendelea kuchukua katika kuiongoza nchi kwa mwelekeo wa kuiletea maendeleo endelevu ya ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii. Aidha, nawapongeza Makamu wa Kwanza, Mheshimiwa Maalim Seif Shariff Hamad na Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd kwa kushirikiana kwa pamoja na Mheshimiwa Rais katika utendaji kazi za kila siku. Kwa pamoja nawatakia kila la kheri na baraka na kuwaombea Mwenyezi Mungu azidi kuwapa hikima, imani na busara ili waendelee kuingoza nchi hii kwa kufuata misingi ya demokrasia na Utawala bora – Amin.

Mhe. Mwenyekiti, ninaamini kuwa ni kupitia mashauriano ya viongozi wetu hao wakuu wa Kitaifa ndio naomba kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuniteua kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo miezi mitatu iliyopita nikitokea Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba uniruhusu pia kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Waziri aliyeanza kusimamia Wizara hii katika awamu hii ya saba, Mheshimiwa Abdillah Jihad Hassan kwa kuiongoza na kuiendesha Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya viongozi na wafanyakazi wa Wizara yangu naomba pia kutoa mkono wa rambi rambi kwa Wazanzibari wote kwa janga kubwa lilitokea la kuzama meli ya Mv. Spice Islender na Mv. Skagit na kupoteza roho za Wazanzibari wenzetu katika ajali hiyo. Tunamuomba Mola azilaze roho za marehemu hao mahala pema Peponi - Amin.

Kupitia tukio hili la msiba naomba nivipongeze vyombo vyote vya habari vya Serikali na vya binafsi kwa namna vilivyojitolea katika kuwapa wananchi taarifa sahihi kuhusiana na kadhia ile ya kusikitisha. Nakumbuka sana ubunifu wa waandishi na watangazaji wa Shirika la ZBCTV ya kuonesha picha za waliofariki zikiwa na namba maalum kwenye televisheni yao, iliharakisha watu wengi waliokuwa hawajajua majaaliwa ya jamaa zao kwenda uwanja wa Maisara kutambua maiti za jamaa zao.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nikijitayarisha kuiwasilisha hutuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2012/2013, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Moh'd Raza, mwanamichezo mashuhuri, kwa kuchaguliwa na wananchi wa jimbo la Uzini kuwa mwakilishi wao katika jimbo hilo na pia nampongeza Mheshimiwa Marina Joel Thomas kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa

Zanzibar kuwa Mwakilishi wa Baraza hili. Nawatakia mafanikio mema katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kukushukuru wewe na wasaidizi wako wote, Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Maofisa na wafanyakazi wote wa Baraza kwa kazi nzuri za kuliendeleza Baraza hili.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari mama yangu Bi Asha Bakari wa Baraza lako tukufu na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo kwa msaada na mashirikiano makubwa waliyoipa Wizara yangu. Napenda kuwahakikishia kwamba daima ushauri, mawazo na maelekezo yao tutayapokea, kuyathamini na kuyafanyia kazi kwani ndiyo yanayotuongoza katika kufanya kazi zetu kwa ufanisi na kujiamini. Naomba pia niwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Gando kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza utumishi wangu wa ujumbe wa Baraza la Wawakilishi kwao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa niruhusu kutoa maelezo kuhusu mwelekeo wa bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Katika maelezo hayo nitatoa uchambuzi wa malengo tuliyoahidi katika mwaka wa fedha 2011/2012 na utekelezaji wake. Kisha nitaelezea malengo ya mwaka wa fedha 2012/2013 ambayo Wizara imekusudia kuyatekeleza baada ya kuidhinishiwa na Baraza lako tukufu fedha tunazoziomba.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo imeunganisha sekta nne (4) muhimu ambazo ni Sekta ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo zilizo chini ya taasisi 19. Ndani ya taasisi hizo zimo idara nne (4), Kamisheni mbili (2), mashirika matatu (3), Vyuo viwili (2), Hoteli moja (1), Mabaraza matatu (3), Tume moja (1), Bodi moja (1), kituo kimoja (1) na Ofisi Kuu iliyoko Pemba. Taasisi hizo ni:

i. Idara ya Utumishi na Uendeshaji,
ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
iii. Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC),
iv. Idara ya Habari Maelezo,
v. Shirika la Magazeti ya Serikali,
vi. Chuo cha Uandishi wa Habari,
vii. Tume ya Utangazaji,
viii. Kamisheni ya Utalii,
ix. Shirika la Utalii,
x. Chuo cha Maendeleo ya Utalii,
xi. Hoteli ya Bwawani,
xii. Kamisheni ya Utamaduni na Michezo,
xiii. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale,
xiv. Baraza la Kiswahili,
xv. Baraza la Sanaa,
xvi. Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho,
xvii. Baraza la Taifa la Michezo,
xviii. Kituo cha EACROTANAL,

xix. Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara yangu ilipangiwa kupata Shilingi 7,284,572,049 kwa kazi za kawaida na Shilingi 2,960,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Aprili 2012, Wizara ilikwishapatiwa jumla ya Shilingi 5,741,176,899/= kwa kazi za kawaida, sawa na asilimia 79 na Shilingi 2,906,000,000/= kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 98 (Tafadhali angalia Viambatisho Nam. 1a na 1b).

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara ilipanga kukusanya mapato ya Shilingi 1,212,800,000/=. Hadi kufikia Aprili 2012, Wizara imeweza kukusanya jumla ya Shilingi 1,306,233,431/= sawa na asilimia 109 (Tafadhali angalia Kiambatisho Nam. 2).

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MWAKA 2011/2012 NA MALENGO YA MWAKA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, majukumu na utekelezaji kamili kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na malengo yanayokusudiwa kufanywa katika mwaka wa fedha 2012/2013 kwa kila taasisi iliyo chini ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji ina jukumu la kusimamia shughuli zote za Utawala, Utumishi (Rasilimali watu), maslahi ya wafanyakazi wote na kusimamia udhibiti wa bajeti katika Wizara. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

Kuongeza ufanisi wa uongozi na utawala katika taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa kusimamia na kutathmini utekelezaji wa kazi kwa watendaji wa Wizara.

i. Kusimamia upatikanaji wa nafasi za masomo na mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi wa Wizara ili kuwa na wafanyakazi watakaokuwa na ujuzi na uwezo katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

ii. Kuandaa mipango ya kupunguza maambukizi mapya ya virusi vinavyosababisha ukimwi (VVU) na kuhakikisha masuala mtambuka yanaingizwa na kutekelezwa katika mipango ya Wizara.

iii. Kusimamia na kuimarisha upatikanaji wa miundo mbinu mbali mbali pamoja na vitendea kazi katika maidara yaliyomo ndani ya Wizara ili kufanikisha ufanisi wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa fedha 2011/2012 Idara iliidhinishiwa jumla ya Sh. 772,612,116/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Aprili 2012 imefanikiwa kupata Sh. 667,204,567/= sawa asilimia 86.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii imefanikiwa kutekeleza malengo yake ya mwaka wa fedha 2011/12 kama ifuatavyo:

i. Kusimamia upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya intaneti, faksi na simu, ununuzi wa mafuta na vilainishaji, ulipaji wa gharama za maji na umeme na ununuzi wa vifaa vya kuendeshea ofisi ili kuiwezesha ofisi kuendesha kazi za kila siku. Aidha, Idara imeweza kulifanyia matengenezo madogo madogo jengo la Wizara, kuyafanyia matengenezo magari, kununua samani za ofisi na kulipa wafanyakazi maposho mbali mbali yanayowastahikia.

ii. Imeandaa mikutano ya ndani ya Wizara iliyojadili utekelezaji wa majukumu ya Idara na taasisi zilizomo katika Wizara, kuwagharimia masomo wafanyakazi saba (7) wanawake wanne (4) na wanaume watatu (3). Kati ya hao wafanyakazi wawili (2) ngazi ya cheti, mfanyakazi mmoja (1) stashahada, wafanyakazi wawili (2) shahada ya pili na mfanyakazi mmoja (1) shahada ya uzamili, na pia kulipia gharama za posho la kujikumu kwa watendaji wa Wizara wanaohudhuria masomo ya nje ya nchi. Aidha, imesimamia upatikanaji wa nafasi za masomo kwa taasisi zilizomo ndani ya Wizara na kwamba jumla ya wafanyakazi 54, kati yao wanawake 42 na wanaume 12 walipatiwa mafunzo katika fani mbali mbali (Tafadhali angalia kiambatisho nam. 3a)

iii. Idara imesimamia na kuwapatia masomo wafanyakazi 37 kutoka taasisi zilizomo ndani ya Wizara, katika nchi za China, Egypt na India, Masomo hayo yalihusisha fani ya habari, makumbusho ya kihistoria, utawala na uongozi, teknolojia ya habari, utamaduni na mipango (Tafadhali angalia kiambatisho nam. 3b)

iv. Kutoa elimu kwa wafanyakazi pamoja na kuandaa vipindi juu ya kuepukana na maambukizo mapya ya virusi vinavyosababisha ukimwi (HIV/AIDS). Aidha, idara imeandaa na kuratibu maadhimisho katika nyanja za michezo, utamaduni na utalii. Kwa mwaka huu timu za Wizara za michezo ya mpira wa miguu na mpira wa pete zimeshiriki mashindano yanayoandaliwa na NSSF huko Dar es Salaam na timu ya Habari Sports Club kuchukua ushindi wa kwanza wa mashindano yote ya mpira wa miguu na mpira wa pete.

v. Idara imeweza kusimamia upatikanaji na ulipaji wa gharama zote za vifaa, vitendea kazi kwa ajili ya uimarishaji wa miundombinu ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kuandikia, samani za Ofisi, mafuta na vilainishi, umeme kwa ajili ya matumizi ya Ofisi, kuimarisha mawasiliano ya simu na Internet pamoja na matengenezo madogo madogo ya jengo katika Wizara kwa lengo la kuhakikisha ufanisi wa kazi unaimarika

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara ya Utumishi na Uendeshaji imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuongeza ufanisi wa uongozi na utawala katika taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa kusimamia na kutathmini utekelezaji wa kazi wa watendaji wa Wizara.

ii. Kusimamia upatikanaji wa nafasi za masomo na mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi wa Wizara. Katika kutekeleza hilo Idara inatajaria kuwapatia

nafasi za masomo jumla ya wafanyakazi arubaini na tatu (43) kutoka katika taasisi zote za wizara kwa masomo ya muda mrefu, na wafanyakazi kumi na nane (18) kwa mafunzo ya muda mfupi katika kada mbali mbali katika vyuo vya ndani ya nchi.

iii. Kuyafanyia matengenezo majengo ya Wizara ikiwa ni pamoja na kuligeuza jengo la studio ya zamani iliyopo Rahaleo kuwa studio ya kisasa ya kurikodia muziki na filamu na kuufanyia matengenezo ukumbi wa juu wa Baraza la Wawakilishi la zamani kwa shughuli za mikutano ya Idara ya Habari Maelezo.

iv. Kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi mapya ya ukimwi na kwamba semina tatu, zinatarajiwa kutolewa kwa wafanyakazi wa Wizara na taasisi zake juu ya athari na namna ya kuepusha maambukizi mapya ya ukimwi. Aidha idara itaandaa vipeperushi vitakavyotoa ujumbe juu ya ugonjwa wa ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuifanya Idara ya Utumishi na Uendeshaji iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 1,275,920,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kupanga, kutayarisha, kukagua, kuratibu na kutathmini mipango ya maendeleo ya Wizara, kupitia Sera, kufanya tafiti mbali mbali na kusimamia utekelezaji wake. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

i. Kuimarisha shughuli za mipango, sera na utafiti kwa maendeleo ya Wizara.

ii. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sera na matokeo ya tafiti kwa shughuli za Wizara.

iii. Kuandaa mipango ya hali ya kuzingatia masuala mtambuka (jinsia, mazingira na utawala bora) kwa maendeleo ya Wizara.

iv. Kuimarisha vitengo vya utafiti na takwimu ili kuweka utaratibu mzuri wa ukusanyaji na utunzaji wa takwimu kwa maendeleo ya Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa fedha 2011/2012 Idara iliidhinishiwa jumla ya Sh. 76, 000,000/= kwa kazi za kawaida na mpaka Aprili ilifanikiwa kupata Sh. 56, 326,150 sawa asilimia 74.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara hii imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

i. Idara imeweza kuandaa mpango kazi wa Wizara *(Action Plan)* kwa lengo la kuimarisha shughuli za utendaji kazi. Idara imeweza kuratibu utafiti ulioendeshwa na Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho Unguja na Pemba. Utafiti huo ni kwa ajili ya kuangalia hali ya kuporomoka maadili ya Mzanzibari. Pia Idara imewapatia mafunzo ya siku nne (4)

maofisa 15 kutoka taasisi za Wizara kuhusu namna ya kuandaa na kuratibu miradi ili kuweza kupata wafadhili katika miradi inayoandaliwa. Aidha, Idara imeendesha vikao vya robo mwaka vya kutathmini utekelezaji wa kazi kwa maofisa mipango wa taasisi za Wizara kwa lengo la kukuza na kuimarisha utendaji wao wa kazi.

ii. Idara imeweza kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa mipango wa Wizara na kusimamia na kuratibu mapitio ya Sera ya Utamaduni kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo. Aidha, Idara ilimtafuta mshauri elekezi ambaye ameanza maandalizi ya utayarishaji wa Sera ya Makumbusho na Mambo ya kale.

iii. Idara imeweza kutoa mafunzo kwa watendaji wa Wizara kuhusu masuala mtambuka likiwemo suala la jinsia ambapo taasisi zote za Wizara zimefaidika na mafunzo hayo na kukiimarisha kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kukipatia vitendea kazi. Aidha, Idara imeratibu miradi ya maendeleo kwa kushirikiana na wahisani. Miradi yenyewe ni kukarabati mnara wa mawambi mafupi uliopo Dole kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China, kuhamisha mnara wa masafa ya kati kutoka Chumbuni kwenda Bungi na Ujenzi wa jengo jipya la Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi.

iv. Yametolewa mafunzo elekezi kwa maofisa mipango wa taasisi za Wizara juu ya ukusanyaji wa taarifa za utekelezaji wa malengo ya Wizara zikiwemo za ukusanyaji wa mapato na ukusanyaji wa takwimu zinazohitajika kwa ajili ya uwekaji wa kumbukumbu za Wizara.

v. Aidha, Idara hii imeweza kusimamia na kuitisha vikao kumi na mbili (12) vya zabuni kwa ajili ya kutafuta wazabuni wenye uwezo wa kusimamia zabuni zinazotolewa. Kazi zilizopatiwa wazabuni ni uhamishaji wa mnara wa mtambo wa radio wa masafa ya kati kutoka Chumbuni kwenda Bungi, ujenzi wa uzio wa Chumbuni, kutafuta msimamizi wa ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii, ujenzi wa nyumba za wafanyakazi Bungi, ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii kilichoko Maruhubi na ukarabati wa jengo la studio ya kurikodia michezo ya kuigiza na muziki Rahaleo.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha shughuli za mipango, sera na utafiti kwa kuwajengea uwezo watendaji wa vitengo vya Wizara na taasisi zake, kusimamia na kuratibu utafiti wa majina ya viumbe wa baharini na mazingira yao kwa ajili ya kuandika kamusi na kutafuta sanaa za jadi ambazo zinaanza kupotea Zanzibar.

ii. Kusimamia na kuandaa miradi ya maendeleo na kuratibu utekelezaji wa sera na utafiti kwa taasisi za Wizara.

iii. Kuwajengea uwezo na uelewa mzuri watendaji wa Wizara kuhusu masuala mtambuka ikiwemo jinsia na masuala ya watu wenye ulemavu pamoja na mazingira.

iv. Kuimarisha vitengo vya Takwimu na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa maendeleo ya Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti katika kufanikisha kwa ufanisi malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 115, 000,000/= kwa kazi za kawaida.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Ofisi Kuu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Pemba ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Wizara Kisiwani Pemba. Ofisi hii ni kiunganishi katika kuhakikisha kwamba majukumu, malengo na Shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba zinatekelezwa kama zilivyokusudiwa. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Ofisi hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuratibu mipango ya maendeleo ya Ofisi kuu Pemba.

ii. Kusimamia na kuimarisha utekelezaji wa shughuli za Ofisi Kuu Pemba.

iii. Kuibua mwamko wa kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi na kuratibu shughuli mtambuka za Ofisi Kuu Pemba.

iv. Kusimamia upatikanaji wa nafasi za masomo na mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi wa Ofisi Kuu Pemba ili kuwa na wafanyakazi watakaokuwa na ujuzi na uwezo katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

v. Kufanya tathmini ya utendaji kazi kwa watendaji wa Ofisi Kuu Pemba ili kuongeza ari ya kufanya kazi na kuhakikisha haki na mafao ya wafanyakazi yanapatikana kwa wakati.

vi. Kukamilisha ujenzi wa uzio wa kituo cha TVZ Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi Kuu Pemba iliidhinishiwa jumla ya Sh. 593,979,376/= kwa kazi za kawaida na mpaka Aprili 2012 imepata Sh. 503,078,000/= sawa na asilimia 85.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Ofisi hii imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

i. Kuratibu ufungaji wa transmita mpya ya kisasa ya kurushia matangazo ya Televisheni Mkanjuni Pemba, kusimamia kazi za uwekaji wa nyasi bandia katika uwanja wa Gombani iliyofanywa na kampuni ya Greenfield ya Uholanzi na kutoa huduma katika Radio Jamii iliyoko Micheweni kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata habari, burudani ili kuongeza idadi ya wasikiliza.

ii. Kuimarisha huduma za uendeshaji wa kazi za kila siku na kuwawezesha waandishi, watangazaji na watendaji wengine kutekeleza wajibu wao kwa kuwepo uhakika wa upatikanaji wa vitendea kazi vinavyohitajika.
iii. Kuandaa vikao vya wafanyakazi kuhusu elimu ya mabadiliko ya elimu ya ukimwi na upimaji wa hiari ikiwa ni sehemu ya kuibua mwamko wa kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi.
iv. Kugharimia masomo kwa wafanyakazi tisa (9) kwa ajili ya kukuza viwango vyao vya elimu katika ngazi ya cheti na diploma kwa fani mbali mbali.
v. Kujenga uzio unaozunguka kituo cha televisheni kilichopo Mkoroshoni na ujenzi wa sehemu ya kuhifadhia jenereta.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Ofisi hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazofanywa na taasisi za Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo zilizoko Pemba shughuli hizo zimepangwa kutekelezwa kama ifuatavyo:

ii. Kuimarisha utekelezaji kazi wa wafanyakazi katika Ofisi kuu Pemba na kuwajengea mazingira mazuri yatakayowafanya kuleta ufanisi katika kazi kwa kuwapatia vitendea kazi na kuwapeleka masomoni wafanyakazi watano (5).

iii. Kuendeleza mpango wa taifa wa kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi na kuratibu shughuli mtambuka pamoja na kufanya semina tatu.

iv. Kuifanyia matengenezo madogo Ofisi Kuu Pemba, nyumba ya Ofisi iliyoko Madungu pamoja na kushughulikia matengenezo madogo madogo katika uwanja wa Gombani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kufanikisha malengo iliyojipangia Ofisi Kuu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Pemba, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe Shilingi 590,506,000/= kwa kazi za kawaida, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

SEKTA YA HABARI

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Habari imeundwa na taasisi tano. Taasisi hizo ni

1) Shirika la Utangazaji Zanzibar,
2) Idara ya Habari Maelezo,
3) Shirika la Magazeti ya Serikali,
4) Tume ya Utangazaji na
5) Chuo cha Uandishi wa Habari.

Majukumu ya Msingi ya taasisi hizi ni kutoa taarifa, kuelimisha na kuburudisha jamii kwa njia ya machapisho au utangazaji kupitia vyombo vya Serikali na vya binafsi. Utekelezaji kwa

mwaka 2011/2012 na malengo ya mwaka wa fedha 2012/2013 kwa sekta ya Habari ni kama ifuatavyo:

SHIRIKA LA UTANGAZAJI

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Shirika ni kutoa habari, kuelimisha, kuburudisha na kuhamasisha jamii juu ya masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa na iliyokuwa Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) na Televisheni Zanzibar (TVZ) katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 zimeunganishwa pamoja na kuwa za Shirika. Hivyo, Shirika hili lilipaswa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha usambazaji wa habari kwa kufungua Ofisi Dar es Salaam.

ii. Kununua vifaa vya kisasa vinavyotumia teknolojia ya dijitali katika kuimarisha shughuli za utangazaji Zanzibar.

iii. Kuimarisha ubora wa matangazo ili kuweza kuvutia wasikilizaji watazamaji na wafanyabiashara wa ndani na nje ya Zanzibar.

iv. Kuanza majaribio ya urushaji wa matangazo kwa kutumia teknolojia ya dijitali.

v. Kuanzisha utaratibu wa kupasha habari kwa njia ya ishara ili kuwapatia fursa ya kupata habari watu wenye mahitaji maalumu (wasiosikia na wasioweza kusema).

vi. Kukarabati mnara wa masafa mafupi kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China na kuhamisha mnara wa masafa ya kati kutoka Chumbuni kwenda Bungi.

vii. Kuwapatia wafanyakazi wa sehemu ya ufundi elimu ya teknolojia ya dijitali ili kwenda sambamba na vifaa vya teknolojia hiyo ya kisasa.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa fedha 2011/2012 Shirika liliidhinishiwa jumla ya Sh. 1,551,785,767./= kwa kazi za kawaida na mpaka Aprili 2012 kupatiwa Sh. 1,233,743,063/= sawa asilimia 80. Shirika lilipangiwa kukusanya mapato jumla ya Sh. 160,000,000/= na hadi kufikia mwezi wa April, 2012 Shirika limekusanya jumla ya Sh. 100,700,100/= sawa na asilimia 63 ya matarajio ya makusanyo yote. Katika matumizi ya miradi ya maendeleo liliidhinishiwa jumla ya Sh. 2,440,000,000/= na kupata 2,440,000,000/ sawa na asilimia 100.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji limefanikiwa kutekeleza malengo hayo kama ifuatavyo:-

i. Shughuli za usambazaji wa habari zimeimarishwa tokea kufunguliwa ofisi ya Shirika huko Dar es Salaam. Hivi sasa kupitia idhaa ya *ZBC*-Redio, wasikilizaji wanapata taarifa na matukio mbali mbali kwa wakati unaostahiki kutoka Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kipindi cha Kutoka Magezetini.

ii. Vifaa mbali mbali vya kisasa vinavyotumia teknolojia ya dijitali vimenunuliwa katika kuimarisha shughuli za utangazaji Zanzibar. Vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na transmita mbili zilizowekwa Masingini na Mkoroshoni Pemba na kufunga mitambo mipya ya studio

huko Karume House. Mitambo hiyo ya studio kutoka nchi ya Japan na Dubai imegharimu jumla ya Shilingi 2,400,000,000/=. Fedha zilizotumika kununulia mitambo hii zimetokana na msamaha wa madeni kutoka nchi wafadhili.

Shirika pia limefanikiwa kuweka vifaa vya kurikodia vyenye kutumia teknolojia ya dijitali katika studio zake za kutangazia na kutayarisha vipindi. Vifaa hivyo ni pamoja na *Audio mixer* na *Video mixer*. Kuwapatia malipo wasanii na watu wengine wanaorikodi vipindi vyao. Jumla ya wafanyakazi 16 wamepatiwa mafunzo ya Diploma na mafunzo ya muda mfupi katika vyuo tafauti.

iii. Juhudi kubwa zimechukuliwa za kuimarisha ubora wa matangazo yanayotolewa na Shirika la Utangazaji. Juhudi hizo ni pamoja na kuimarisha utendaji kazi za kila siku, kuifanyia matengenezo Ofisi na kununua vifaa vya kutendea kazi ili kuleta ufanisi mzuri wa kazi. Miongoni mwa vifaa hivyo ni kompyuta, vifaa vya kuandikia pamoja na kuvifanyia matengenezo vyombo vya usafiri ili kuweza kuwachukua na kuwarudisha wafanyakazi. Aidha, Shirika limeongeza urushaji wa vipindi vya moja kwa moja kutoka kwenye matukio muhimu kwa lengo la kuwapasha habari wananchi kwa wakati unaostahiki na kufahamu kinachotendeka katika jamii yao. Miongoni mwa vipindi hivyo ni Vikao vya Baraza la Wawakilishi vinavyoendelea, matukio ya maafa, michezo na shughuli nyengine za kitaifa. Jumla ya matukio 440 yametangazwa moja kwa moja katika kipindi hiki. Pia Shirika limeweza kuhamisha kumbukumbu kutoka kwenye tepu na kuwekwa kwenye sidii.

iv. Hadi hivi sasa bado hakuna majaribio yaliyofanyika ya kuanza kurusha matangazo kwa kutumia teknolojia ya dijitali kutokana na kukosekana miundo mbinu ya kurushia teknolojia hiyo. Katika kutimiza azma hiyo, jitihada zinaendelea za kutafuta mitambo hiyo kwa njia ya mkopo. Hatua iliyofikiwa ya kupatikana mkopo huo kutoka benki ya *Exim ya China* inatia matumaini makubwa. Mashauriano baina ya Serikali na ofisi ndogo ya ubalozi wa China iliyopo Zanzibar na ofisi ya ubalozi wa China iliyopo Dar es Salaam yanaendelea vizuri.

v. Shirika tayari limefanikiwa kumpata mtaalamu wa kutumia lugha za ishara. Kupatikana kwa mtaalamu huyu kutasaidi njia za mawasiliano kwa watu wenye mahitaji maalumu (wasiosikia na wasioweza kusema).

vi. Kazi ya ukarabati wa mnara wa mawimbi mafupi imekamilika na wananchi tayari wanafaidika katika kupata matangazo. Ukarabati huo umefanywa kwa ushirikiano wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China. Aidha, Shirika limefanikiwa kuhamisha mnara wa masafa ya kati kutoka Chumbuni na kazi kujenga mnara huo wa Bungi zinaendelea. Kuhamishwa mnara huo kunarahisisha utuaji wa ndege zinazoingia nchini kwa usalama. Pia Ofisi, Studio na nyumba mbili (2) za kisasa za familia nne za wafanyakazi zimejengwa katika eneo hilo la Bungi ili kuimarisha utendaji mzuri wa kazi.

vii. Mafunzo ya teknolojia ya dijitali yamekuwa yakitolewa kwa wafanyakazi wa sehemu ya ufundi na hata utangazaji ili kuwaweka tayari katika kukabiliana na mageuzi ya teknonojia

ya utangazaji duniani. Mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa na wakufunzi kutoka Idhaa ya Deuche Welle, Ujerumani kutokana na makubaliano maalumu yaliyofikiwa ya kuwapatia wafanyakazi wa utangazaji taaluma hiyo mpya hapa nchini. Mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa hata kwa wafanyakazi wa utangazaji wa vyombo binafsi. Hadi hivi sasa mafundi 23 na watangazaji pamoja na wapiga picha 24 wameshapata mafunzo hayo.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Shirika la Utangazaji limepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

i. Kuimarisha shughuli za utendaji wa Shirika katika ngazi ya uendeshaji na utawala.

ii. Kukuza viwango vya ubora wa matangazo kwa wasikilizaji na watazamaji wa ndani na nje ya Zanzibar.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe.Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Shirika la Utangazaji limepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

iii. Kuimarisha shughuli za utendaji wa Shirika katika ngazi ya uendeshaji na utawala.

iv. Kukuza viwango vya ubora wa matangazo kwa wasikilizaji na watazamaji wa ndani na nje ya Zanzibar.

v. Kuingia katika urushaji wa matangazo kwa kutumia teknolojia ya dijitali.

vi. Kuimarisha sehemu ya ufundi ya Shirika kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China, ambapo tutaanzisha kitengo cha ufundi wa transmita, mixer na vipoza hewa

vii. Kukamilisha ujenzi wa wa kituo cha matangazo cha masafa ya kati (medium wave) bungi.

viii. Kukamisha maandalizi ya muundo wa Shirika ikiwa pamoja na kuweka rasimu ya sheria ya Shirika la Utangazaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya mwelekeo mpya wa shirika la Utangazaji (*ZBC*) kutaka kujiendesha kibiashara, utaratibu uliozoeleka wa kufaidi bure huduma za matangazo na vipindi vya taasisi mbali mbali unakusudiwa kuondoshwa. Hivyo, ni muhimu sana kwa Wizara za Serikali na Mashirika katika mwaka huu wa fedha kulifikiria hilo wanapohitaji huduma zao za matangazo na pia kujiweka tayari katika maandalizi ya bajeti inayokuja.

Mhe. Mwenyekiti, ili Shirika la Utangazaji liweze kutekeleza malengo yake yaliyojipangia katika mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhiniShe jumla ya Shilingi 2,016,224,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, na kuchangia Shilingi 280,700,000/= katika mfuko mkuu wa serikali.

IDARA YA HABARI MAELEZO

Mhe.Mwenyekiti, Idara ya Habari Maelezo ni kiungo cha utoaji wa habari kati ya Serikali na vyombo ya habari. Idara hii pia ina jukumu la kuimarisha uhusiano mzuri kati ya Serikali na Taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi, kutayarisha na kutoa vielelezo katika mfumo wa picha, sinema na majarida kuhusu shughuli za Serikali na kusimamia sera na sheria ya habari Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuratibu shughuli za vyombo vya habari nje na ndani vinavyofanya kazi Zanzibar.

ii. Kukuza usambazaji wa habari za maendeleo mjini na vijijini kwa kutumia Gari la Sinema, zikiwemo kupunguza umasikini, maambukizi ya ukimwi, jinsia, mazingira na utumikishwaji wa watoto.

iii. Kuimarisha uwezo wa waandishi wa habari na wafanyakazi kwa kuimarisha sekta ya Habari kwa kuwaelimisha wafanyakazi katika vyuo vya habari ikiwemo Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar na chuo cha habari cha Royal College cha DSM; pamoja na semina kuhusu mambo ya habari.

iv. Kuimarisha Idara kwa kukamilisha ukarabati wa jengo sehemu ya maktaba na kulipatia vitendea kazi

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara iliidhinishiwa jumla ya Sh. 239,225.089/= kwa kazi za kawaida na hadi Aprili 2012 kupatiwa Sh. 179,764,278/= sawa

asilimia ya 75. na kupangiwa kukusanya jumla ya Sh. 7,800,000/= katika mfuko mkuu wa Serikali na kufanikiwa kukusanya 13,784,750/= sawa na asilimia 177.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti**,** Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kutekeleza malengo hayo kama ifuatavyo:-

i. Shughuli za Vyombo vya Habari ndani na nje ya nchi vinavyofanya kazi Zanzibar zimekuwa zikiratibiwa na Idara ya Habari (Maelezo) kwa kuangaliwa namna vinavyotekeleza shughuli zake na kwa kiasi gani vinazingatia maadili ya kazi na kufuata sheria zilizopo. Aidha, imekuwa ikiwapatia waandishi hao vitambulisho vinavyowawezesha kufanya shughuli zao kila mwaka na kuhakikisha hakuna mtu anayefanya kazi za uandishi bila ya kusajiliwa na kupatiwa kibali cha kuandika au kupiga picha.

ii. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Idara imekuwa ikikuza usambazaji wa habari za maendeleo kwa kuwapatia waandishi ya habari taarifa mbali mbali za Serikali na kusimamia mikutano ya waandishi wa habari iliyofanywa na Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na vyama vya siasa pamoja na Taasisi mbali mbali; yakiwemo Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali na Jumuiya za Wananchi. Mpaka Aprili, 2012 Idara imesimamia mikutano ya waandishi wa Habari 36 Unguja na Pemba. Pia Idara imekuwa ikionesha sinema vijijini kuhusu maendeleo na kutanabahisha juu ya matokeo ya maradhi ya mripuko. Vijiji 112 (Unguja 84 na Pemba 28) vimepata kuoneshwa sinema kuhusu ukuzaji wa Uchumi na Upunguzaji umaskini, maambukizi ya ukimwi, mambo ya jinsia, maafaa, mazingira, chanjo ya shurua na kampeni juu ya uchumaji wa karafuu na kuepukana wa magendo.(Tafadhali angalia kiambatisho nam. 4a na 4b).

iii. Waandishi wa habari wanne (4) wamepatiwa mafunzo katika fani ya habari ngazi ya Diploma katika Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar na Royal cha Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya kuimarisha uwezo wa watendaji hao katika fani ya habari nchini. Aidha, wafanyakazi watatu (3) wamepelekwa Chuo cha Utumishi wa Umma kuchukua cheti na Diploma.

iv. Idara iliifanyia ukarabati ofisi ya maktaba pamoja na maeneo mengine ya ofisi na kuipatia vitendea kazi, zikiwemo kompyuta, kamera, vifaa vya chumba cha kutengeneza vipindi na mashine za kufanyia uhariri wa habari. Hata hivyo, idara inaendelea kukamilisha utengenezaji wa chumba hiki ili kiwe kinakubaliana na mahitaji ya kisasa.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti**,** katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara ya Habari Maelezo imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuendelea kuwasomesha wafanyakazi, ununuzi wa vifaa vya kazi za Ofisi, samani na kutengeneza vipindi vya maendeleo na utalii kwa wote.

ii. Kuweka tovuti ya Idara.

iii. Kuifanyia marekebisho Sheria No. 5 ya Usajili wa Magazeti na vijarida ya mwaka 1988.

iv. Kuweka mbao za matangazo mpya.

Mhe. Mwenyekiti, ili kukamilisha vyema malengo ya Idara ya Habari Maelezo katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya **Shilingi 293,630,000/=** kwa kazi za kawaida na kuchangia **Shilingi 15,500,000/=** katika mfuko mkuu wa serikali.

SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Magazeti ya Serikali lina jukumu la kusimamia uchapishaji wa magazeti ya Serikali ya Zanzibar, kuelimisha wananchi ili kukuza uelewa wao wa mambo na kutoa habari zenye kuhamasisha jamii na kushiriki kwenye harakati za maendeleo ya nchi. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2021, Shirika la Magazeti ya Serikali lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuhakikisha Gazeti linawafikia wasomaji Zanzibar nzima na maeneo zaidi ya Tanzania Bara.

ii. Kukuza uwezo wa waandishi wa habari wa magazeti na wafanyakazi kwa ajili ya kuongeza ubora wa makala, habari na matukio.

iii. Kuongeza ubora wa magazeti ili kuzidi kuingia katika ushindani wa soko kwa kukuza mapato ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara iliidhinishiwa jumla ya Sh. 844,946,775/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia April 2012 shirika limefanikiwa kupata Sh. 638,622,971/= sawa asilimia 76. Shirika lilipangiwa kukukusanya jumla ya Shilingi 300,000,000/= na kufanikiwa kukusanya 295,075,573/= sawa na asilimia 98.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa, Gazeti limeweza kutekeleza kwa ufanisi mkubwa malengo ya mwaka 2011/2012 kwa kufanya yafuatayo:

i. Shirika limeweza kuwafikia wasomaji wengi zaidi kwa kuongeza maeneo ya usambazaji. Gazeti hilo hivi sasa linafika katika maeneo ya Mkokotoni, Nungwi, Uroa, Makunduchi na Jambiani kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba maeneo yalioongezeka ni Madenjani, Wete, Konde na Mkoani. Aidha, Shirika linaendelea na mpango wake wa uhamasishaji wa utamaduni wa kusoma magazeti nchini kwa kusambaza magazeti skulini. Hadi sasa skuli kadhaa zimepatiwa magazeti hayo ikiwemo Konde (sekondari na msingi), Micheweni, Shumbamjini, Chambani, Ukutini, Wambaa, Mkanyageni, Micheweni, Uweleni na Makombeni kwa Skuli za Pemba. Mpango kama huo unafanyika kwa kusambaza magazeti vijijini na kwenye makundi ya watu kwa kushirikiana na *Pemba Press Club*. Kwa upande wa Unguja Skuli zilizokwishafaidika na mpango huu ni Makunduchi, Muyuni, Donge na Mkwajuni.

Kwa upande wa Tanzania Bara, mikoa 15 inasambaziwa gazeti la Zanzibar Leo. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Tanga, Tabora, Mbeya, Bukoba, Morogoro, Mtwara, Kigoma, Arusha, Mwanza, Songea, Singida, Dodoma, Iringa, Shinyanga pamoja na maeneo ya Kibaha na Bagamoyo.

ii. Shirika limeweza kuwasomesha wafanyakazi (20) katika ngazi mbali mbali ndani na nje ya nchi katika fani tafauti. Wafanyakazi hao wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa ajili ya kuwaongezea uwezo wa kuandika makala na habari zenye mvuto na ubora kwa wasomaji.

iii. Kwa kiasi kikubwa Shirika limefanikiwa kuongeza ubora wa gazeti kihali na kihabari na hivyo *Zanzibar Leo* kuwa na nafasi kubwa ya kukubalika ndani na nje ya Zanzibar. Hivi sasa gazeti tayari limeshaingia katika ushindani wa soko na kwamba redio na televisheni kadhaa zimekuwa zikilitangaza katika kipindi cha *Kutoka Magazetini* kinachotolewa na redio na televisheni hizo kila asubuhi.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Shirika la Magazeti ya Serikali limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha ubora wa magazeti ya Shirika na kuongeza idadi ya kurasa za magazeti ya *Zanzibar Leo* kutoka kurasa 16 hadi 20 pamoja na kuongeza idadi ya magazeti yanayochapishwa na Shirika la magazeti kutoka gazeti moja (1) la Zanzibar Leo lililopo sasa na kuongeza jengine la habari za Michezo, Utamaduni na Utalii.

ii. Kukuza uwezo wa waandishi wa habari na wafanyakazi kwa kuwaendeleza kielimu ili kuwaongezea uwezo katika utendaji wao wa kazi. Kwa mwaka huu wa fedha tunatarajia kusomesha wafanyakazi wanane (8) katika kozi tafauti.

iii. Kuendelea kupanua wigo wa usambazaji wa magazeti yanayochapishwa na Shirika la Magazeti ya Serikali ndani ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, pamoja na kuliingiza gazeti katika tovuti ya Shirika ili liweze kusomwa duniani kote.

iv. Kufanya ukarabati na kuhamia kwenye ofisi ya muda ya gazeti kwenye majengo ya ZBC Radio na kutafuta ofisi za kudumu kwa ajili ya Shirika la Magazeti ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti**,** katika kulifanya Shirika la Magazeti ya Serikali liweze kutekeleza malengo hayo, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha **Shilingi 856,000,000/=** kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha shirika limepangiwa kukusanya jumla ya Shilingi 500,000,000/=.

TUME YA UTANGAZAJI

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Tume ya Utangazaji ni kusimamia vyombo vya utangazaji vya Serikali na vya binafsi vinavyoanzishwa nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Tume ya Utangazaji ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuandaa utaratibu wa kupunguza uingizaji nchini vifaa vya analogi na jinsi ya kudhibiti takataka za vifaa hivyo.

ii. Kuratibu shughuli za utangazaji nchini kwa kutoa huduma bora za utangazaji ili zisiingiliane baina ya watumiaji.

iii. Kujenga uelewa kwa vyombo vya utangazaji vya Serikali na watu binafsi juu ya maadili ya utangazaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Tume ya Utangazaji iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 180,000,000/= kwa kazi za kawaida na kufikia Aprili 2012 imeweza kupata Shilingi 166,886,440/= sawa asilimia 93. Tume ilipangiwa kukukusanya jumla ya Shilingi 16,000,000/= na kufanikiwa kukusanya 26,503,000/= sawa na asilimia 166.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Tume ya Utangazaji Zanzibar, imeweza kutekeleza malengo iliyojipangia kwa kufanya mambo yafuatayo:

i. Semina kadhaa zimefanyika kuelezea athari ya kuendelea kuingiza vifaa vya utangazaji vya analogi hasa televisheni ambavyo muda si mrefu havitatumika kutokana na viwanda vinavyotengeneza vifaa hivyo kutokuwepo tena duniani. Jumla ya vipindi 18 vya kuelimisha jamii juu ya masuala ya dijitali vilitayarishwa na kurushwa kupitia ZBC-Redio na Hits FM Redio. Vipindi hivyo pia vimetoa taaluma juu ya athari ya mazingira kutokana na mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji. Aidha, vikao mbali mbali vya mashirikiano kati ya Tume na Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania Bara (TCRA) vimefanyika kwa lengo la kuzungumzia mkakati wa kudhibiti uingizaji wa vifaa vikongwe vya analogi pamoja na kuainisha sifa za kampuni inayostahiki kuwa msafirishaji ujumbe (*multiplex operator*).

ii. Tume imeandaa rasimu ya Kanuni za Utangazaji zitakazoongoza sekta ya utangazaji nchini kutokana na mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji na kuandaa muongozo wa uingizaji wa ving'amuzi nchini ambao utasambazwa kwa wafanyabiashara wote watakaohitaji kuagiza vifaa hivyo. Aidha, Tume imeweza kuandaa mkakati wa kuhama kutoka teknolojia ya utangazaji ya analogi kwenda dijitali kwa kutoa leseni kwa kampuni mbili – Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) na Star Media ili zifanye kazi za kuunganisha huduma za ujumbe (*multiplex operator*) ambapo majukumu makubwa ya kampuni hizi ni kusambaza nchini matangazo ya vituo vyengine vya televisheni.Tume imeweza pia kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa vyombo vya utangazaji vya Serikali na watu binafsi, kuandaa semina juu ya mageuzi ya teknolojia ya utangazaji kwa maofisa na Wakurugenzi wa SMZ, na semina kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu dijitali pamoja na mafundi na watayarishaji vipindi, na viongozi wa vituo vya utangazaji vya Serikali na Binafsi vilivyopo Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji la Ujerumani la *Dutche Welle*. Tume pia imeandaa mkakati wa mawasiliano kwa lengo la kuongoza kampeni ya kitaifa kwa umma ya kuhama kutoka teknolojia ya Utangazaji ya analojia na kuingia dijitali.

iii. Katika kujenga uelewa kwa vyombo vya utangazaji vya Serikali na watu binafsi juu ya maadili ya utangazaji, Tume ya Utangazaji imeweza kuvipatia vyombo vya habari Sera na Sheria ya Utangazaji ya Zanzibar na kutoa mafunzo yanayohusiana na mambo ya maadili na miiko ya uandishi wa habari na utangazaji. Aidha, mkakati wa mawasiliano (*Communication strategy for analog to digital migration*) umeandaliwa sambamba na mkakati wa mageuzi ya teknolojia ya utangazaji kutoka analogi kwenda dijitali (*Analogy to digital migration strategy for 2011-2015*).

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti**,** katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Tume ya Utangazaji imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

i. Kuratibu shughuli za Utangazaji wa dijitali nchini kwa kutoa miongozo na maelekezo ya kitaalamu kuhusu teknolojia hiyo mpya.

ii. Kuandaa na kuendesha kampeni ya kitaifa ya elimu kwa umma juu ya mageuzi ya teknolojia ya utangazaji nchini.

Mhe. Mwenyekiti**,** ili kukamilisha vyema malengo iliyojipangia Tume ya Utangazaji katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **Shilingi 168,000,000/=** kwa kazi za kawaida, Shilingi **100,000,000/=** kwa kazi maendeleo na kukusanya jumla ya **Shilingi 33,000,000/=** katika mfuko mkuu wa Serikali.

CHUO CHA UANDISHI WA HABARI

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya Chuo cha Uandishi wa Habari ni kutoa mafunzo, ushauri na taaluma ya uandishi wa habari na tafiti mbali mbali kwa wanafunzi wa ngazi ya Cheti na Stashahada zinazozingatia mahitaji ya soko la ajira. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Chuo cha Uandishi wa Habari kilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuwa na mtaala bora wa Chuo na kuimarisha ubora wa kiwango cha taaluma ya Habari itakayoendana na mageuzi ya teknolojia ya Habari duniani.

ii. Kuimarisha Chuo kwa kukipatia vifaa vya kufundishia kwa njia ya vitendo na kukipatia walimu wenye sifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Chuo kiliidhinishiwa jumla ya Shilingi 290,000,000/= kwa kazi za kawaida na hadi Aprili 2012 kupatiwa Shilingi 221,100,000/= sawa asilimia ya 76. Chuo kilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 63,000,000/= na hadi kufikia Aprili 2012, jumla ya shilingi 86,172,342/= zimekusanywa sawa na asilimia 136.8.

UTEKELEZAJI HALISI:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo kimetekeleza malengo iliyojipango kwa kufanya yafuatayo:

i. Chuo kimeweza kugharimia mafunzo ya wafanyakazi watatu katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi. Mafunzo hayo ya muda mrefu ni sehemu ya utekelezaji wa mipango ya chuo katika jitihada za kuweka mazingira mazuri ya kusomeshea na kukidhi mahitaji yaliyopo. Aidha, vifaa kadhaa vya kufundishia vimenunuliwa pamoja na zana za ofisi.

ii. Hatua za awali zimechukuliwa za kutafuta mshauri wa kuendesha mafunzo ya mtaala na kukamilisha kutengeneza miongozo ya kitaalamu ikiwemo Kitabu cha Muongozo wa Shughuli za Chuo (Prospectus), Vipeperushi na Mpango Mkakati wa Chuo kwa lengo la kuinua kiwango cha taaluma ya Habari itakayoendana na mageuzi ya teknolojia ya habari duniani.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Chuo cha Uandishi wa Habari kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha shughuli za kitaaluma chuoni kama vile mazingira ya kazi na ya kusoma kwa kulipa maslahi ya wafanyakazi na walimu ikiwemo mishahara na posho zao. Aidha kulipia gharama za huduma zote za uendeshaji wa Chuo.

ii. Kuifanyia matengenezo studio kwa kununua vifaa vikiwemo kamera na redio za kurekodia pamoja kununua vitabu kwa ajili ya maktaba.

iii. Kuandaa miongozo mbali mbali ya kazi itakayosaidia kuimarisha utendaji kazi na kuandaa sheria na miongozo ya shughuli za chuo ikiwemo kanuni za sheria ya Chuo na miongozo ya uendeshaji wa shughuli za Chuo.

Mhe. Mwenyekiti, ili kukamilisha vyema malengo ya Chuo cha Uandishi wa Habari katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, kimekadirio kukusanya shilingi 80,000,000/= na naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya **Shilingi 305,000,000/=** kwa kazi za kawaida**.**

Mhe. Mwenyekiti**,** ili kukamilisha vyema malengo ya Chuo cha Uandishi wa Habari katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, kimekadirio kukusanya shilingi 80,000,000/= na naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya **Shilingi 305,000,000/=** kwa kazi za kawaida**.**

SEKTA YA UTALII

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Utalii inajumuisha Kamisheni ya Utalii, Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Shirika la Utalii na Hoteli ya Bwawani. Taasisi hizi zimepewa jukumu la kupanga, kusimamia, kuendeleza Utalii, kutoa mafunzo kuhu Utalii na kuitangaza Zanzibar ili sekta hii iende sambamba na sera, malengo na mipango ya Serikali katika kufikia malengo ya kuimarisha uchumi wa Taifa na kupunguza umasikini (MKUZA). Utekelezaji kwa mwaka 2011/2012 na malengo ya mwaka wa fedha 2012/2013 kwa sekta ya Utalii ni kama ifuatavyo:

KAMISHENI YA UTALII

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la msingi la Kamisheni ya Utalii Zanzibar ni kuratibu shughuli za utalii, kupanga, kusimamia na kuendeleza Shughuli za kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, KamiSheni ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kukuza idadi na ubora wa huduma za watalii Zanzibar.

ii. Kuimarisha uhusiano wa Sekta ya utalii na taasisi nyengine.

iii. Kukuza, kueneza na kutangaza utalii wa Zanzibar kitaifa, kikanda na kimataifa.

iv. Kukuza shughuli za utalii ili kuwa endelevu kwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kimazingira nchini.

v. Kuanzisha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu utakaotumia "*T-start software*".

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mwaka wa fedha 2011/2012, Kamisheni iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 917,219,774/= kwa kazi za kawaida na mpaka Aprili 2012 kupatiwa Shilingi 592,444,172/= sawa na asilimia ya 65. Aidha, ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi **842,000,000**/= katika mfuko mkuu wa serikali na kufanikiwa kukusanya **1,013,859,829/=** sawa na asilimia 120.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Kamisheni ya Utalii imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

i. Juhudi zimechukuliwa za kugharimia masomo wafanyakazi 10 katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi katika ngazi za cheti, stashahada, shahada ya kwanza, shahada ya pili na shahada ya uzamili (PhD). Aidha, wafanyakazi wawili (2) wamepatiwa mafunzo mafupi nchini Japani katika kozi ya utalii endelevu kwa nchi za Afrika (*Sustaibale Tourism Development in African Countries*) na mfanyakazi mmoja amepatiwa mafunzo katika kozi ya uoanishaji wa hifadhi ya mazingira na upunguzaji wa umasikini katika mpango wa maendeleo (*Mainstreaming*

Poverty Environment Leakages into Development and Planning' nchini Israel) kuoanisha mambo ya mazingira, umasikini na mpango wa maendeleo.

Kamisheni pia imewapatia mafunzo mafupi askari polisi katika mikoa yote ya Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yalilenga kutoa uelewa kwa askari polisi juu ya Sheria za utalii na jinsi ya kutoa huduma bora kwa wageni; zimeandaliwa semina mbili za utalii kwa wote kwa wadau mbali mbali. Aidha, wanafunzi 40 kutoka vyuo mbali mbali hapa nchini na nje ya nchi wamepatiwa taarifa mbali mbali za utalii wa Zanzibar. Wafanyakazi watano (5) kutoka Pemba wamepatiwa ziara ya kimafunzo na maofisa wawili (2) wa kitengo cha masoko wamepatiwa kozi fupi ya utangazaji kwa njia ya mtandao (*e-marketing*) iliyofanyika Mombasa – Kenya. Mafunzo ya ndani yametolewa kwa wafanyakazi wanaohusika na ukusanyaji wa takwimu chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) ambapo mtaalamu aliyetengeneza '*data base'* ya uwekaji taarifa za utalii kwa njia ya mtandao (*t-stat*) alitoa mafunzo hayo. Chini ya ufadhili wa UNDP kamisheni ilifanya utafiti wa utokaji wa wageni kwa upande wa Zanzibar pekee na ripoti ya utafiti huo tayari imeshawasilishwa kwa wanaohusika kwa kuitumia. Aidha, jengo la ofisi kuu iliyopo Amaan, limefanyiwa matengenezo ikiwa ni awamu ya kwanza ya kulikarabati.

ii. Katika kuimarisha uhusiano na taasisi nyengine, Kamisheni ya Utalii ilishiriki katika mkutano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki nchini Kenya na katika vikao mbali mbali vya mashirikiano na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB). Kwa kushirikiana na Idara ya Takwimu, Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii (Bara), Kamisheni imeendelea kushiriki katika kuendeleza utafiti wa utokaji wa wageni (*Tourism Sector Survey*) na ukusanyaji wa taarifa. Aidha, yapo mashirikiano mazuri na Jumuiya ya Wenye Mahoteli Zanzibar. Katika kuendeleza uhusiano na jumuiya mbali mbali, Kamisheni imeweza kuhudhuria katika warsha ya kuimarisha takwimu za utalii (*workshop on tourism statistics & tourism satellite account*) iliyoandaliwa na Shirika la Utalii Duniani (UNWTO) kwa kushirikana na Shirika la Utalii Kusini mwa Afrika (RETOSA) huko Victoria Falls –Zimbabwe.

iii. Zanzibar imekuwa ikishiriki katika maonesho mbali mbali ya kitaifa na kimataifa kwa lengo la kujitangaza kiutalii. Maonesho ni pamoja na ya Saba Saba Mjini Dar es salaam, "*World Travel*

Market" (WTM) Mjini London, BIT Mjini Milan na maonesho ya ITB Mjini Berlin. Maonesho mengine ni *Arabia Travel Market* (ATM) Dubai, kongamano la wawekezaji Dubai na Maeneo ya Utalii INDABA, Afrika ya Kusini. Lengo la ushiriki wa maonesho hayo ni kuitangaza Zanzibar na pia kuyaendeleza masoko hayo. Mbali na kushiriki katika maonesho, kumekuwa kukitolewa machapisho yenye lengo hilo la kuitangaza Zanzibar. Machapisho hayo ni pamoja na kalenda za ukutani, jarida la "*Indian Ocean Experience*" kwa lugha ya Kiengereza na jarida la *Karibu Zanzibar*. Aidha, kumekuwa kukitolewa matangazo mbali mbali katika majarida ya kitalii kama vile "*a.c Braby Commercial Directory*", "*Travel World China*", "*Tanzania Review*" na "*Business Times*". Kamisheni ya Utalii imepokea vikundi vinne vya waandishi wa habari wa Kimataifa kutoka nchi za Sweeden, China (CBN), Uengereza (*The Scottish Sun*) na Malaysia (VAYA) ambavyo huitangaza Zanzibar katika nchi zao kupitia vyombo vyao vya habari. Hatua hii ya kujitangaza imeanza kuiletea Zanzibar heshima ya kujulikana na hata kujipatia tunzo ya Utalii duniani (Tafadhani Angalia kiambatisho nambari nne 4)

iv. Sheria Nam. 6 ya mwaka 2009 ya utalii imefanyiwa mapitio na hatimaye kurekebishwa kwa lengo la kuufanya utalii uwe endelevu kwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na mazingira ya Zanzibar. Marekebisho hayo yamelenga katika dhana pana zaidi ya kuufanya "Utalii kwa Wote" ambapo matunda ya sekta hiyo yatawanufaisha wananchi wengi zaidi. Aidha, marekebisho ya Sheria hiyo yametilia mkazo ulindaji wa silka, mila na desturi za Zanzibar. Kwa kuzingatia hayo, utalii umejengewa misingi ya kuimarika na kuwa endelevu.

v. Upatikanaji wa takwimu sahihi ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Katika kuhakikisha takwimu sahihi za watalii zinapatikana, Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wawekezaji katika sekta ya Utalii Zanzibar (ZATI) chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) wameanzisha mfumo wa kukusanya na kuchambua takwimu kwa kutumia mtandao ujulikanao kwa jina la (*T-stats*). Jumla ya wafanyakazi wanane (8) wamepatiwa mafunzo ya utumiaji wa mtandao huo katika kuhifadhi na kufanya uchambuzi wa takwimu za utalii.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Kamisheni ya Utalii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha shughuli za utalii kwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na mazingira nchini kwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Kamisheni ya Utalii na ununuzi wa zana bora za kufanyia kazi.

ii. Kuimarisha na kuongeza wigo wa vivutio vya utalii kwa kufanya utafiti wa utokaji wa wageni, kukusanya taarifa kwa ajili ya kuweka daraja za hoteli (*Hotel Inventory for Classification*) na kutoa elimu kwa wadau wa utalii juu ya matokeo ya utafiti wa vivutio vya utalii na kuvipangia mpango wa kivitangaza katika masoko ya ndani na nje.

iii. Kuutangaza utalii wa Zanzibar kitaifa na kimataifa na kuandaa utaratibu utakaosaidia kupata takwimu sahihi za idadi ya watalii wanaoingia nchini na kupembua aina za masoko, matakwa ya wageni na kutambua wageni wanaorejea ili kuimarisha masoko ya asili na kuibua mapya kwa kutumia uzoefu tulioupata kwa kushiriki maonesho mbali mbali ya utalii ndani na nje ya nchi na kuhudhuria mikutano na makongamano ya utalii na uwekezaji. Pia kuimarisha upatikana na uchambuzi wa takwimu kwa kutumia "*T-Stat Software*" ili kupata idadi sahihi ya wageni wanaoingia nchini.

iv. Kuendeleza dhana ya utalii kwa wote kwa kuhakikisha kila Mzanzibari anaufahamu na kuuelewa utalii kwa kina, ili wananchi wanufaike na hatimaye waweze kuondokana na umaskini kupitia utalii. Wananchi katika sekta mbali mbali pamoja na taasisi za umma na za binafsi zitawezeshwa kwa kufanyiwa semina, makongamano, vipindi mbali mbali vya redio, televisheni na makala katika magazeti na vipeperushi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Kamisheni iweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya **Shilingi 1,318,000,000/=** kwa kazi za kawaida na kukusanya **Shilingi 1,202,000,000/=** kwa ajili ya kuchangia mfuko mkuu wa serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

CHUO CHA MAENDELEO YA UTALII ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la msingi la Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar ni kutoa taaluma itakayowezesha kujenga rasilimali watu wenye ujuzi, utaalamu na stadi zinazohitajika na kukubalika katika viwango vya kimataifa ili kuimarisha sekta ya Utalii Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar kilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuwa na mtaala bora wa chuo ili kuimaisha ubora wa kiwango cha elimu ya Utalii utakaoenda na soko la utalii.
ii. Chuo kuwa na vifaa vya kisasa vya kufundishia na walimu wenye sifa.
iii. Kufanya ukarabati wa miundo mbinu ya chuo cha Maendeleo ya Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mwaka wa fedha 2011/2012 Chuo kiliidhinishiwa jumla ya Shilingi 443,493,225/= kwa kazi za kawaida na mpaka Aprili 2012 kufanikiwa kupata Sh. 345,471,535/= sawa asilimia 78. Pia kiliidhinishiwa jumla ya Shilingi 400,000,000/= kwa kazi za maendeleo na kupata Shilingi 400,000,000/= sawa asilimia 100% Chuo kilipanga kukusanya shilingi 211,000,000 na hadi Aprili Chuo kimekusanya shilingi 176,672,746 sawa na asilimia 84.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimefanikiwa kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kama ifuatavyo:

i. Mshauri elekezi ameajiriwa kwa ajili ya kupitia upya mpango mkakati, na hivi sasa rasimu ya mwisho imeshapatikana, baada ya kupitiwa na wadau wa utalii na kuingiza mawazo yao. Aidha, Chuo kimeweza kuipitia mitaala yake baada ya kupata mshauri elekezi kutoka katika taasisi ya PUM (kwa kidachi Programma Uitzending Managers)ya Nertheland kwa njia ya msaada. Huduma za taasisi hii kwa Chuo zinaendelea kwa kuingizwa ndani ya mradi ujulikanao kwa jina la "*VEHICLE*" yaani "*Vocational Education for Higher Categories and Levels*". Mradi huu wa miaka miwili utasaidia Chuo kujitangaza kibiashara, kujenga mahusiano mazuri na wadau wengine wa utalii, kuwajengea uwezo walimu katika mbinu bora za kufundishia na kuongeza mada zaidi katika mitaala ya Chuo zitakazokidhi viwango vya mahitaji ya sasa ya watalii. Chuo

pia kimeajiri Mshauri elekezi kwa kuandika muongozo wa shughuli za chuo (*prospectus*) na hivi sasa tayari imeshakamilika.

ii. Katika kuwaendeleza walimu, Chuo kimewapeleka wafanyakazi wawili katika fani ya utalii na ukarimu, kwa masomo ya muda mrefu na kimewapatia nafasi ya mafunzo ya muda wa miezi miwili nchini China walimu watano, kwa ajili ya mafunzo yaliyohusiana na utoaji wa huduma bora katika shughuli za utalii. Katika mahusiano kati ya Chuo na Taasisi nyengine za ndani na nje ya nchi, Chuo kimeendelea kujenga mahusiano ya aina mbali mbali kwa lengo kuwaendeleza zaidi walimu, wanafunzi na wafanyakazi wote kwa jumla. Katika kufanikisha hayo Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimeshirikiana na taasisi mbali mbali katika kutoa taaluma ya utalii na ukarimu kama vile Agakhan ambayo kama tunzo imetoa kompyuta 2 kwa ajili ya matumizi ya ofisi, na mradi wa NICHE (Netherlands Initiative for Capacity development in Higher education) ambao pia umekubali kukipatia Chuo kompyuta, fotokopi na "*server*" kwa ajili ya matumizi ya Chuo, na mafunzo kwa walimu.

iii. Kwa upande wa kuimarisha miundo mbinu, Chuo kimeweza kuyafanyia matengenezo makubwa madarasa matano, kwa kutia sakafu mpya, kuezeka na kutia rangi. Pia majengo ya ofisi, jiko na mkahawa yamefanyiwa matengenezo makubwa kwa kuezekwa, kuweka vigae na kutiwa rangi. Pamoja na matengenezo hayo, Chuo kilifanyia marekebisho miundombinu ya maji kwa kulaza mabomba mapya, kujenga mnara mwengine na kuweka tangi la maji ili kupunguza tatizo la maji lililokuwepo hapo Chuoni. Aidha Chuo kimeufanyia matengenezo makubwa ukuta wa mbele na kuondoa tatizo la uingiaji wa wanyama katika eneo la Chuo.

iv. Mhe. Mwenyekiti, ili kuimarisha mbinu za kufundishia na kujifunzia, Chuo kimeliimarisha jiko kwa kuweka vifaa vipya vya kisasa, kama vile majiko ya gesi, mafriji na friza na vifaa mbali mbali vinavyohusiana na mafunzo ya mapishi. Samani kwa ajili ya matumizi ya mkahawa pia zilinunuliwa.

v. Mhe. Mwenyekiti, katika miradi ya maendeleo, Chuo cha Maendeleo ya Utalii katika mwaka wa fedha 2011/12 kimekuwa na mradi mmoja tu wa maendeleo, nao ni kujenga jengo jipya ambalo litatumika kwa shughuli za utawala na taaluma. Katika jengo hilo zimo ofisi za watendaji wakuu

pamoja na maktaba, madarasa na ukumbi wa mikutano, jumla ya **Shilingi 400,000,000/=** zimetumika kwa ujenzi huo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa masomo 2011/12 chuo kimesajili jumla ya wanafunzi 203 katika fani ya mbali mbali. Aidha Chuo kiliweza kutoa mafunzo ya kompyuta na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano iliyowashirikisha pia wanafunzi wa fani ya Utalii. Pia katika mwaka 2012/2013 chuo kinatarajia kutoa wahitimu 185 katika fani mbali mbali ambazo tunatoa katika chuo hicho.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

i. Kuongeza idadi ya walimu wanne (4) wenye, taaluma bora, idadi ya wanafunzi (150-200), wafanyakazi 6 wenye utaalamu wa kisasa, pamoja na kununua vifaa vya kisasa vya kusomeshea na kujifunzia.
ii. Kujenga mahusiano mazuri kitaifa, kikanda na Kimataifa juu maendeleo ya taaluma ya Utalii kwa kushiriki mikutano mbali mbali ya ndani ya Zanzibar na Nje ya Zanzibar.
iii. Kuimarisha miundombinu ya Chuo ili kuweka mazingira bora ya kufanyia kazi kama vile kujenga ukuta wa Chuo wenye urefu wa mita 106 na Ununuzi wa samani
iv. Kushajiisha vijana wa Kizanzibari ili kuelewa dhana nzima ya utalii kwa wote kwa kutoa elimu kwa skuli kumi (10) katika wilaya zote za Unguja na Pemba ili waelewe na kushiriki katika kutekeleza lengo la utalii kwa wote.

Mhe. Mwenyekiti, ili Chuo kiweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya **Shilingi 420,000,000/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 400,000,000/=** kwa kazi za maendeleo na kukusanya shilingi 262,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

SHIRIKA LA UTALII

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Utalii ni moja ya Mashirika ya Serikali ambalo majukumu yake ni kuendeleza biashara ya utalii kwa kutoa huduma kwa wageni wanaotembelea Zanzibar na wenyeji wanaotembelea maeneo ya kihistoria na yenye vivutio vya kitalii. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Shirika la Utalii lilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha huduma za biashara kwa watalii wanaokuja kwa njia ya bahari (*Cruise tourism*).

ii. Kuongoza kwenye utoaji wa huduma bora kwa watalii watakaoshughulikiwa na Shirika (*Package tourism*).

iii. Kuanzisha vianzio vipya vya mapato kwa kuchochea kuibuliwa utalii wa ndani kwa kuzitumia nyumba za Shirika zilizopo Makunduchi na Jambiani.

iv. Kutafuta wawekezaji watakaoingia ubia na Shirika katika kuyatumia maeneo yaliyoko Kuji na Vitongoji

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Shirika la Utalii hadi kufikia Aprili limeweza kutumia jumla ya Shilingi 107,662,261/= baada ya kufanikiwa kukusanya jumla Shilingi 178,292,800/=.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, Shirika ilimeweza kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Shirika limeweza kufanya mawasiliano na Jumuiya ya Meli za Kitalii kwenye mwambao wa Afrika Mashariki (*Indian Ocean Cruise Association*) na tayari limeshapewa kibali cha kujiunga na kuwa mwanachama. Kujiunga na Jumuiya hii kutaliwezesha Shirika kupata watalii wengi kwa lengo la kujiongezea tija.

ii. Shirika kwa kupitia wataalamu waelekezi linaendelea kulifanyia tathmini ya kuona jinsi gani linaweza kujiendesha kibiashara. Tathmini hiyo inalenga kulielekeza Shirika kuwa na uwezo wa kujiendesha kibiashara kwa kutumia vianzio vilivyonavyo sasa na kuongeza vianzio vipya vya mapato. Shirika limeanza kuzisimamia hoteli zake zilizoko Wete na Mkoani baada ya kuvunja mkataba na Kampuni ya *National Marketing Ltd*. baada ya muekezaji huyo kushindwa kutekeleza baadhi ya masharti yaliyomo katika mkataba huo, ikiwemo kutozifanyia matengenezo hoteli hizo mbili.

iii. Shirika limeanzisha vianzio vya mapato kwa kuanzisha utalii wa ndani kwa kushirikiana na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale kwa kuwapeleka wanafunzi na wananchi wengine kwenye maeneo ya kihistoria. Shirika linatayarisha mpango wake mpya wa kibiashara ambao utatoa muelekeo wa uendeshaji wa kibiashara kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, ambao utakamilika katika robo ya mwanzo wa mwaka huu wa fedha.

iv. Jitihada za Shirika hazikuweza kufanikiwa kupata mwekezaji kwenye maeneo ya Kuji na Vitongoji kutokana na kutokuwepo miundombinu inayohitajika katika maeneo hayo ikiwemo maji, umeme na barabara. Hata hivyo, jitihada zinaendelea za kutafuta wawekezaji wengine watakaoweza kuwekeza katika maeneo hayo.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 Shirika la Utalii limekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha Utalii wa ndani kwa kupanua wigo hadi kwenye soko la Afrika Mashariki.

ii. Kuifanyia kazi ripoti ya tathmini ya Shirika, ambapo itaelekeza ama hoteli za Wete na Mkoani na nyumba za Makunduchi na Jambiani zifanyiwe matengenezo na shirika au zikodishwe kwa sekta binafsi.

iii. Kupokea na kuifanyia kazi ripoti ya tathmini ya shirika kwa jumla ambayo itaamua kuwepo kwa shirika au kulivunja Shirika la Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, ili Shirika liweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya Shilingi 245,440,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kwa fedha itakazozalisha lenyewe.

HOTELI YA BWAWANI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Hoteli ya Bwawani ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuwa na miundombinu bora na ya kisasa kwa huduma bora za hoteli kwa kuendelea kufanya matengenezo ya vyumba, kumbi za mikutano na miundombinu myengine.

ii. Kuwa na wafanyakazi wenye ufanisi wa kazi kwa kuwajengea uwezo na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

iii. Kutatua tatizo la mmong'onyoko wa ardhi kwenye kingo za Hoteli kunakosababishwa na mawimbi makali ya bahari kwa kushirikiana na Mamlaka zinazohusika.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, Hoteli ya Bwawani katika mwaka wa fedha 2011/2012 haikutengewa fedha, kwani ilitakiwa kujipangia malengo yake kutokana na inachokizalisha. Katika hali hiyo, hoteli imeweza kutekeleza kwa mafanikio kwa kufanya yafuatayo:

i. Jumla ya vyumba vinne (4) vimefanyiwa matengenezo na viko katika hali nzuri baada ya kutiwa vigae, kuwekwa vyoo na mahamamu mpya. Sambamba na hilo, yamefanyika matengenezo ya paa la ukumbi wa Salama pamoja na uwekaji wa viyoyozi nane (8) vipya.

ii. Jumla ya wafanyakazi tisa (9) wamepatiwa mafunzo katika vyuo tafauti vya hapa Zanzibar.

iii. Juhudi zimechukuliwa za kukabiliana na tatizo la mmong'onyoko wa ardhi. Hoteli imeipa kazi Mamlaka ya Bandari kujenga ukuta wa kuzuia mawimbi ambapo ukuta huo umeshajengwa. Kazi inayoendelea sasa ni ujazaji wa kifusi kwenye eneo lililojengwa.

Mhe. Mwenyekiti, Hoteli ya Bwawani kwa mwaka 2011/2012 ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi 850,000,000, na ilifanikiwa kikusanya jumla ya Shilingi 730,431,589/= sawa asilimia 85% hadi Aprili, 2012. Aidha hoteli katika mwaka fedha 2011/2012 hadi Aprili 2012 imetumia jumla ya Shilingi 672,534,027/=.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Hoteli ya Bwawani imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

i. Kuendelea na mpango wake wa kuwapatia wafanyakazi wake mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.
ii. Kuendelea kutoa huduma mbali mbali za biashara katika hotel.
iii. Kuendelea na matengenezo muhimu ya vyumba vya wageni na kumbi za mikutano.

Mhe. Mwenyekiti, hoteli imejiwekea kutekeleza malengo hayo na naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya Shilingi 800,000,000/= na kukusanya Shilingi 900,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kwa fedha itakazozizalisha wenyewe.

SEKTA ZA UTAMADUNI NA MICHEZO

Mhe. Mwenyekiti, Sekta za Utamaduni na Michezo zinaundwa na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, Baraza la Kiswahili, Baraza la Sanaa, Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho, kituo cha *EACROTANAL*, Baraza la Taifa la Michezo na Uwanja wa Amaan. Taasisi hizi zimepewa jukumu la kusimamia, kuratibu, kufufua, kuendeleza na kudumisha shughuli zote za Utamaduni na Michezo Zanzibar. Utekelezaji kwa mwaka 2011/2012 na malengo ya mwaka wa fedha 2012/2013 kwa sekta za Utamaduni na Michezo ni kama ifuatavyo:

KAMISHENI YA UTAMADUNI NA MICHEZO

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya Kamisheni hii ni kuratibu na kusimamia maendeleo ya utamaduni na michezo Zanzibar kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kujenga Studio ya kisasa ya kurekodia michezo ya kuigiza na muziki.

ii. Kushajiisha na kuendeleza maendeleo ya vikundi vya Utamaduni kwa vijana katika Wilaya, Mikoa na Taifa.

iii. Kulinda na kuendeleza urithi wa utamaduni kama jukumu la wananchi.

iv. Kuziwezesha timu kushiriki michezo ya kimataifa kwa lengo la kuwapa nafasi wachezaji chipukizi kushiriki vizuri kwenye mashindano ya kitaifa na kimataifa.

v. Kusimamia na kushajiisha kufanyika mashindano ya mawizara na mashirika ya Serikali kwa michezo mbali mbali.

vi. Kusimamia uanzishaji wa viwanja vya michezo vya Wilaya kwa kushirkiana na Ofisi za Wilaya zinazohusika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Kamisheni iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 667, 306,866/= kwa kazi za kawaida na hadi Aprili 2012 kufanikiwa kupata Shilingi 575, 159,900/= sawa asilimia ya 86.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti**,** katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

i. Hatua zimeanza kuchukuliwa za ujenzi wa studio ya kisasa ya kurikodia michezo ya kuigiza na muziki. Lengo lilikuwa studio hiyo kuijenga katika kiwanja maalumu huko Tunguu lakini kutokana na kuwa hadi hivi sasa kiwanja hakijapatikana kwa ajili ya ujenzi huo, imeamuliwa jengo la zamani la studio iliyokuwa Sauti ya Tanzania Zanzibar lifanyiwe matengenezo makubwa ili liweze kukidhi haja kwa kuanzia. Kazi ya kulifanyia matengenezo hayo jengo imeanza kwa kampuni ya Rans kukabidhiwa jukumu la kuligeuza jengo hilo hadi kuwa studio ya kisasa. Matengenezo hayo yanatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha 2012/2013.

ii. Kazi ya kuendeleza maendeleo ya vikundi vya utamaduni kwa vijana katika ngazi ya wilaya, mikoa hadi taifa imeanza kwa kuweka mikakati ya kukuza na kuinua vipaji vya wasanii. Semina tatu (3) zenye lengo la kuvitambua vipaji hivyo na kuanza kuvishughulikia kwa kuviendeleza vimefanyika Unguja na Pemba. Semina hizo zimekuwa zikielimisha wasanii umuhimu wa kazi zao kwa jamii na jinsi ya kulinda na kuthamini utamaduni wa Mzanzibari. Mkazo umetolewa wa kusaidia kuvifufua vikundi vya utamaduni vikiwemo vya taarab asilia na ngoma za asili vilivyojijengea sifa miaka ya nyuma lakini hivi sasa vimefifia au vimekufa kabisa

iii. Mikakati maalumu imechukuliwa ya kulinda na kuendeleza urithi wa utamaduni. Mikakati hiyo ni kuendeleza Tamasha la Mzanzibari ambalo ni kichocheo cha wananchi katika kuuenzi utamaduni wao. Aidha, kufanyika tamasha la utamaduni wa watu wa Oman lililofanyika Zanzibar kuliongeza hamasa kwa Wazanzibari kuona umuhimu wa watu kutukuza utamaduni wao. Semina mbali mbali kwa wasanii na maofisa wa Utamaduni Unguja na Pemba zimeandaliwa kuhusu maudhui ya mkataba wa hifadhi ya utamaduni usioshikika na utekelezaji wa mkataba huo uliotiliwa saini baina ya serikali ya Tanzania na *UNESCO*.

iv. Timu kadhaa za Zanzibar zimewezeshwa kushiriki katika mashindano ya kitaifa na kimataifa. Timu ya Taifa ya Zanzibar ya mpira wa miguu *"Zanzibar Heroes"* imegharimiwa kuweka kambi nchini Misri kwa ajili ya maandalizi ya kushiriki katika michuano ya kombe la "*CHALLENGE*", kushiriki mashindano ya *VIVA World Cup;* chama cha mpira wa netiboli (*CHANEZA*) kilisaidiwa kwenda Msumbiji kwa ajili ya

kushiriki katika mashindano ya *"ALL AFRICAN GAMES"*; timu ya walemavu wa akili ilisaidiwa kushiriki katika mashindano ya '*SPECIAL OLYMPIC*" yaliyofanyika Athens, timu ya judo iliwezeshwa kushiriki mashindano yaliyofanyika Msumbiji ; timu ya wanyanyua vitu vizito iliwezeshwa kushiriki katika mashindano ya vijana yaliyofanyika Uganda na timu ya riadha ilisaidiwa kwenda Botswana katika mashindano ya vijana. Aidha, semina ya mchezo wa *"Handball* na *Volleyball* kwa makocha, zilifanywa kwa ajili ya wataalamu na walimu wa michezo skulini ili kuwajengea vijana uwezo wa kushiriki katika mashindano ya kitaifa na kimataifa.

v. Maandalizi ya kuzishajiisha timu za mawizara na mashirika ya serikali kushiriki katika mashindano ya michezo mbali mbali yanaendelea. Kazi inayofanyika hivi sasa ni kuendelea kuzishajiisha wizara na taasisi mbali mbali kuunda na kusajili timu zao ili ziweze kushiriki katika mashindano hayo na mashindano mengine yatakayoandaliwa.

vi. Kumekuwa na mwamko mzuri wa kuitikia kampeni iliyoanzishwa ya kutaka wilaya kuanzisha viwanja vya michezo ikiwa sehemu ya kuendeleza michezo. Wilaya zilizoanza kuitikia wito huo ni Magharibi (Bweleo) kwa Unguja na Chake Chake kwa Pemba ambayo hivi sasa inatafuta eneo la kujenga kiwanja hicho. Tatizo kubwa linalozifanya wilaya nyengine kutojitokeza katika wito huo ni kukosa maeneo ya kujenga viwanja hivyo na zile zenye maeneo hazina hatimiliki za maeneo hayo.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuviimarisha vikundi vya sanaa za maonesho, kuifanyia matengenezo nyumba ya sanaa na kununua vifaa vya kazi.
ii. Kuandaa programu ya miaka mitatu ya kuibua vipaji vya sanaa na michezo skulini kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
iii. Kuwajengea uwezo maofisa na wataalamu wa Michezo na Utamaduni kwa kuwafanyia mafunzo mafupi kuhusu utalii kwa wote.
iv. Kuziimarisha huduma za wafanyakazi na mazingira ya kazi kwa kuwapatia elimu wafanyakazi na vitendea kazi.
v. Kuimarisha miundombinu ya michezo kwa kukiimarisha kiwanja cha Amaan na katika ngazi ya Wilaya, Mikoa na Taifa kusaidia uanzishwaji wa viwanja vya michezo midogo midogo vya wilaya na kuzisaida timu za taifa za Zanzibar kushiriki mashindano ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, ili Kamisheni ya Utamaduni na Michezo iweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Shilingi 812, 400, 000, /= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

IDARA YA MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya idara hii ni kuenzi, kuhifadhi na kuendeleza historia ya Zanzibar kwa kutumia makumbusho, maeneo ya kihistoria na mambo ya kale. Pia kuelimisha jamii juu ya umuhimu na faida za matumizi ya makumbusho na mambo ya kale. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha makumbusho na mambo ya kale na kushajiisha jamii kuwa na mwamko wa kuyatembelea kwa ajili ya kufahamu umuhimu na matumizi yake.

ii. Kuanzisha makumbusho ya mkoa katika maeneo muhimu ya kihistoria na kuhimiza jamii kuanzisha makumbusho ya kijamii katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mwaka wa fedha 2011/2012 Idara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 374,443,061/= kwa kazi za kawaida na mpaka Aprili 2012 kufanikiwa kupata Sh 292,199,261/= sawa na asilimia 78 pia ilipangiwa kukusanya Shilingi 170,000,000/= na kufanikiwa kukusanya Shilingi 142,362,852/= sawa na asilimia 84.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe.Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imetekeleza malengo yafuatayo:

i. Idara imeanzisha tovuti yake ili kutoa taarifa zake ndani na nje ya nchi pamoja na vipindi vya redio kuhusu historia na mambo ya kale ya Unguja na Pemba. Idara imekamilisha maonesho juu ya historia ya Zanzibar katika karne ya 20. Maonesho haya yatapelekea makumbusho kupokea wageni wengi wa kawaida na wa kiserikali, wanafunzi na watu mbali mbali kutoka katika visiwa vya Unguja na Pemba na sehemu nyengine za Tanzania.

   Katika kuimarisha makumbusho hayo, Idara imewapeleka wafanyakazi wake kwenye mafunzo mbali mbali yanayohusu lugha, ukutubi, usekretari, uhifadhi wa mambo ya kale pamoja na utunzaji wa makumbusho ili kuweza kurahisisha kazi, malengo na mikakati ya Idara. Aidha, imeweza kuyatangaza vyema maeneo ya kihistoria kwa jamii ya Zanzibar na kuyafanyia matengenezo majengo ya Mangapwani kwenye Mahandaki ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia pamoja na mnara wake pamoja na mahodhi ya Kizimbani na Hamamni.

ii. Katika kuanzisha makumbusho ya mkoa katika maeneo muhimu ya kihistoria, kazi za kuimarisha maeneo ya kihistoria katika maeneo mbali mbali imeanza kwa kuwashirikisha wanajamii walio katika maeneo hayo pamoja na kukusanya vitu vingi vya kihistoria vitakavyofanya makumbusho yatakayoanzishwa yawe na hadhi ya mkoa. Sambamba na juhudi hizo, kazi imeanza kufanywa ya kuhimiza jamii kuanzisha makumbusho yao ya kijamii.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti**,** katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuyapima na kuyapatia hatimiliki maeneo ishirini (20) ya kihistoria Unguja na Pemba.

ii. Kuyaimarisha majengo kumi (10) ya kihistoria kwa kufanya tafiti, kukusanya taarifa zake na kuyafanyia matengenezo. Idara pia inatarajia kulifanya jengo lililoko katika bustani ya Victoria kuwa ukumbi wa mikutano ikiwa ni hatua ya kulirejesha katika historia yake ya awali.

iii. Kuanzisha makumbusho nyengine mpya kama Unguja Ukuu, Mnazi mmoja, Chwaka-Tumbe na jengo la *Livingstone*.

iv. Kuimarisha vitengo vya ndani vya makumbusho na mambo ya kale kwa kuvipatia huduma na vitendea kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Makumbusho iweze kutekeleza malengo yake naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya shilingi 482,320,000/= kwa kazi za kawaida na Shilingi 100,000,000/= kwa kazi za maendeleo na kuchangia Shilingi 210,000,000/= katika mfuko mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

BARAZA LA KISWAHILI

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Baraza la Kiswahili la Zanzibar ni kukuza, kushajiisha na kufuatilia matumizi na maendeleo ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Baraza hili lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kushajiisha kuendeleza matumizi ya Kiswahili kimkoa, kitaifa na kimataifa.

ii. Kuchapisha makamusi ya lahaja ya Kitumbatu, Kipemba na Kimakunduchi.

iii. Kuandika Kamusi la lugha mbili: Kiingereza kwa Kiswahili.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Baraza la Kiswahili liliidhinishiwa jumla ya Shilingi 90,000,000/= kwa kazi za kawaida; mpaka Aprili ilifanikiwa kupata Shilingi 68,955,500/= sawa asilimia ya 77. Aidha, lilipangiwa kukusanya jumla yua Shilingi 10,000,000/= na kuweza kukusanya Shilingi 6,024,500/= sawa na asilimia 60.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Baraza la Kiswahili limetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Baraza limefanya mashindano ya mashairi katika kushajiisha na kuendeleza matumizi fasaha, sanifu na sahihi ya Kiswahili. Jumla ya mashairi 28 yamekusanywa na washindi kupewa zawadi. Aidha, wasanii wakongwe wakiwemo marehemu Bwana Bakari Abeid Ali, marehemu Bwana Iddi Abdalla Farhan na marehemu Bwana Issa Haji Pandu (Issa Matona) wamefanyiwa kumbukumbu kwa kuandikiwa makala zao zilizowasilishwa kwenye maadhimisho ya siku ya Kiswahili Zanzibar. Utafiti zaidi wa wasanii wengine unaendelea ili kuandika kitabu. Baraza pia limerusha vipindi vya Kiswahili 24 kupitia

redio na 24 kupitia Televisheni ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar, na vipindi vinane vimerushwa kupitia Shirika la Utangazaji la Uingereza (*BBC*).

ii Makamusi ya lahaja ya Kitumbatu, Kipemba na Kimakunduchi yameshachapishwa na yako tayari kutumika.

iii Kamusi la lugha mbili za Kingereza na Kiswahli linaendelea kuandikwa, kwa kuingiza fasili kwenye vidahizo vilivyofanyiwa utafiti wa awali.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Baraza la Kiswahili limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kushajiisha na kuendeleza matumizi ya Kiswahili kimkoa, kitaifa na kimataifa kwa kuwajengea uwezo walimu na waandishi chipukizi kwa kuwapa mafunzo na kuchapisha makala za wasanii wakongwe.

ii. Kuendeleza uandishi wa kamusi la lugha mbili la Kiswahili kwa Kingereza.

iii. Kuanza utafiti wa majina ya viumbe vya baharini na mazingira yao kwa lengo la kuandika Kamusi.

iv. Kuanzisha kijarida cha Kiswahili.

v. Kuimarisha maktaba ya BAKIZA kwa kutengeneza rafu za kuwekea vitabu, kununua mashine ya fotokopi, kipoza hewa na kununua vitabu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Baraza la Kiswahili Zanzibar liweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Shilingi 95,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na kuchangia Shilingi 10,000,000/= kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

BODI YA SENSA YA FILAMU NA SANAA ZA MAONESHO

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la msingi la Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho ni kukagua na kuzihakiki filamu na sanaa za maonesho ili kuhakikisha kuwa haziharibu maadili ya jamii zinapooneshwa hadharani na kusikika kwenye vyombo vya habari na rikodi za sidii na kaseti za sauti na picha. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Bodi hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuhakikisha maadili ya utamaduni wa Zanzibar yanafuatwa kwa kusimamia na kukagua kazi za wasanii kwa maendeleo ya utamaduni wa Zanzibar.

ii. Kufanya utafiti juu ya maadili ya Kizanzibari na kutumia matokeo ya utafiti huo kuendeleza sanaa yenye maslahi kwa faida ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa fedha 2011/2012 Bodi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 38,380,000/= kwa kazi za kawaida na hadi Aprili, 2012 kufanikiwa kupata Shilingi 34,800,000/= sawa asilimia 91.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Semina mbili zimeandaliwa Unguja na Pemba zilizowashirikisha viongozi wa vikundi mbali mbali vya sanaa, vyombo vya ulinzi, taasisi za kidini, makatibu wa masheha, vyombo vya habari na maofisa wa utamaduni wa wilaya kwa ajili ya kuwapatia miongozo juu ya namna bora ya kujenga ushirikiano wa karibu miongoni mwa jamii na Bodi katika kulinda na kusimamia utamaduni wetu ambao ni dira ya maadili mema. Kazi mbali mbali za sanaa pamoja na matamasha yamehakikiwa ili kuhakikisha kwamba maonesho yanayofanywa hayakiuki mila na desturi za Mzanzibari. Albamu ya "*History no change*" iliyotayarishwa na *Island Promotion* na filamu ya "*7 days*" ya *Surprise Art Group* ni baadhi ya zilizokataliwa kuoneshwa kutokana na filamu hizo kukiuka maadili ya Zanzibar. Kwa jumla bodi imehakiki matamasha matatu (3), rasimu tatu (3) za michezo tafauti, matangazo 10 ya kibiashara, vidio za nyimbo 20, tenzi tatu (3) zenye maudhui tafauti ya kiserikali, na jumla ya filamu 2,324 kutoka katika maduka mbali mbali ya kukodishia kanda Unguja na Pemba. Aidha, kukagua vikundi tisa (9) vya ngoma tafauti, michezo saba (7) ya kuigiza jukwaani, tenzi 14 na mashairi 11 ya kughani. (Tafadhali angalia kiambatisho nam. 5).

ii. Utafiti umefanywa juu ya suala zima la maadili katika wilaya zote za Zanzibar kwa shehia zilizochaguliwa kwa ajili ya utafiti huo. Watafiti walipita kila Shehia kwa ajili ya kupata taarifa sahihi kuhusiana na ufahamu wa jamii juu ya suala zima la maadili na jinsi yanavyoporomoka. Uchambuzi wa taarifa hizo umekamilika na ripoti itatolewa hivi karibuni.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Bodi ya Sensa na Filamu za Maonesho imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kukagua na kuhakiki filamu na sanaa mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha haziendi kinyume na maadili yetu.

ii. Kuandaa programu maalumu kwa kushirikiana na Idara ya Habari Maelezo na Kamisheni ya Utalii juu ya umuhimu wa kulinda na kuendeleza maadili katika kuimarisha utalii kwa wote.

Mhe. Mwenyekiti, ili Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho iweze kukamilisha shughuli zake, naliomba Baraza lako tukufu iliidhinishe Shilingi 38,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

BARAZA LA SANAA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Baraza la Sanaa Zanzibar ni kusimamia na kuratibu maendeleo ya shughuli za Sanaa Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Baraza la Sanaa lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kushajiisha maendeleo ya kazi za sanaa kwa wasanii wa vikundi mbali mbali.

ii. Kuendelea kushirikiana na nchi mbali mbali na kubadilishana utaalamu katika fani za sanaa.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa fedha 2011/2012 Baraza liliidhinishiwa jumla ya Shilingi 45,180,000/= kwa kazi za kawaida na mpaka Aprili 2012 limefanikiwa kupata Shilingi 39,200,000/= sawa asilimia 87. Aidha, Baraza lilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi 7,000,000/= na limeweza kukusanya Shilingi 4,133,400/= sawa na asilimia 59 mpaka kufikia Aprili 2012.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Baraza la Sanaa limetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Baraza limeweza kushajiisha wasanii kwa kuwapatia mafunzo ya sanaa za maonesho, kazi za mikono kama vile uchoraji, ufinyanzi, udarizi, uashi na uchongaji. Baraza pia limeweza kuandaa semina iliyowashirikisha wasanii wa taarab asilia kwa lengo la kuhuisha sanaa hiyo inayoonekana kudhoofika. Katika kuimarisha sanaa nchini kumekuwepo ushirikiano kati ya mabaraza ya sanaa Zanzibar na Tanzania Bara. Aidha, Baraza limefanya kikao cha pamoja na Bodi ya Sensa ili kubadilishana uzoefu baina yao katika kujenga maadili ya wasanii wa Zanzibar ili waweze kufuata maadili ya Mzanzibari.

ii. Utaratibu unaendelea katika kuifanyia marekebisho Sheria nam. 6 ya mwaka 1983 ya Baraza la Sanaa Zanzibar. Lengo la marekebisho ya Sheria ni kuondoa upungufu uliojitokeza katika utekelezaji wa Sheria hiyo.

iii. Safari za nje kwa wasanii mbali mbali wa Zanzibar zilifanyika miongoni mwa hizo ni kikundi cha Tausi cha akinamama watupu mbacho mwezi wa Aprili 2012 kilikwenda Alexandria nchini Misri na Beirut. Kwa upande mwengine tulishirikiana na ndugu zetu wa Oman kufanya Maadhimisho ya Tamasha la Utamaduni wa Oman hapa Zanzibar tarehe 18/7/2011. Kwa madhumini hayo tulishirikiana katika kupanga na kusimamia uendeshaji wake. Tamasha hilo liliadhimishwa katika sehemu mbali mbali ikiwemo Ngome Kongwe, ambapo kulifanyika ngoma za utamaduni; *Beit El Ajab* kulifanyika ufunguzi wa tamasha na maonesho mbali mbali ya kuchora, kuchonga, usukaji, uhunzi na ufumaji, jumba la

wananchi Forodhani kulifanyika kongamano la Utamaduni na Historia chini ya watoaji mada kutoka Zanzibar na Oman.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti**,** katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Baraza la Sanaa limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia maendeleo ya sanaa na utamaduni wa Mzanzibari kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya utamaduni nje na ndani ya Zanzibar na kuandaa mafunzo mafupi kwa viongozi wa vikundi vya sanaa vilivyosajiliwa.

ii. Kufanya utafiti mdogo wa ngoma za jadi ambazo zinaanza kupotea na kuhifadhi matokeo ya utafiti huo.

iii. Kusimamia na kuratibu mafunzo ya sanaa na Utamaduni kwa watoto kwa kuwajengea uwezo kushiriki katika sanaa za maonesho na uchoraji kupitia vyombo vya habari.

iv. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na wafanyakazi kwa kuwapatia Elimu wafanyakazi na vitendea kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Baraza liweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naliomba Baraza lako tukufu liidhiniShe jumla ya Shilingi 42,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na kuchangia Shilingi 7,000,000/= mwaka wa fedha wa 2012/2013**.**

KITUO CHA AFRIKA MASHARIKI NA KATI CHA SIMULIZI ASILI NA LUGHA ZA AFRIKA (*EACROTANAL*)

Mhe. Mwenyekiti**,** jukumu la msingi la *EACROTANAL* ni kuwa chombo kikuu cha kupashana habari, kuhifadhi kumbukumbu na kuwa chanzo cha utafiti katika ngazi ya kitaifa na kimataifa kuhusu lugha za Kiafrika na Simulizi Asili za nchi wanachama, ambazo ni Burundi, Comoro, Ethiopia, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Somalia, Sudan na wenyeji Tanzania Bara.

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Kituo kiliidhinishiwa jumla ya Shs 20,000,000/= kwa kazi za kawaida na kufanikiwa kupata Shilingi 12,544,307/= sawa na asilimia 63.

Mhe. Mwenyekiti, ili kituo kiweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Shilingi 21,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

BARAZA LA TAIFA LA MICHEZO

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya Baraza la Taifa la michezo Zanzibar ni kusimamia maendeleo ya michezo yote iliyosajiliwa. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Baraza hili limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kutilia mkazo ushiriki wa jamii kwa kuandaa mabonanza ya michezo na mashindano ya ndani katika ngazi ya shehia, wilaya, mikoa hadi Taifa.

ii. Kuimarisha vyama vya michezo katika ngazi zote kwa kuhakikisha vinafanya kazi kulingana katiba zao pamoja na kufanya uchaguzi.

iii. Kuwapatia mafunzo walimu wa michezo mbali mbali kwa mashirikiano na taasisi za kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Baraza iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 140, 000, 000,000/= kwa kazi za kawaida na mpaka Aprili 2012 kufanikiwa kupata Shilingi 113, 675,755/= sawa na asilimia 81.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Baraza la Taifa la Michezo limefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Mashindano mbali mbali yameanzishwa ili kutilia mkazo ushiriki wa jamii katika michezo. Mashindano ya Kombe la Urafiki la mpira wa miguu yalifanyika Pemba kwa kuzishirikisha timu nane (8). Aidha, mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa mpira wa miguu na netiboli yalifanyika Unguja kwa kuzishirikisha pia timu za Tanzania na nje ya Tanzania. Kumekuwa na mashindano ya michezo mengine mbali mbali iliyoandaliwa ikiwemo michezo ya hoki na wavu. Pamoja na mashindano hayo. Zanzibar imeweza kushiriki katika mashindano ya *VIVA World Cup* ambayo hushirikisha nchi zisizokuwa mwanachama wa *FIFA*. Katika mashindano hayo *Zanzibar Heroes* imeweza kuwa mshindi wa tatu. Mabonanza mbali mbali ya michezo yameandaliwa kwa lengo la kuongeza ushiriki mkubwa wa jamii katika michezo. Bonanza la michezo ya watu wenye ulemavu limefanyika Mkoa wa Kusini Unguja, bonanza la mpira wa wavu limefanyika Mkoa wa Kusini Pemba, bonanza la michezo ya mazoezi ya viungo na michezo mbali mbali lenye ujumbe wa michezo kwa wote limefanyika Mkoa wa Mjini/Magharibi; bonanza la mpira wa miguu kwa vijana pamoja na mabonanza mengi mengine nayo pia yamefanyika.

ii. Vyama vya michezo viilimarishwa kwa kupatiwa ruzuku zao za fedha kwa ajili ya kuendesha mashindano ya ndani pamoja na kuziwezesha timu zao kushiriki katika mashindano ya ndani na nje ya Zanzibar. Aidha, baadhi ya vyama vimepatiwa fedha kwa ajili ya ushiriki wa timu zao katika michezo yao ya nje. Miongoni mwa vyama hivyo ni pamoja na judo, riadha, mpira wa mikono, mpira wa pete, mpira wa miguu, mpira wa wavu, karati, mpira wa magongo, baiskeli, kuogelea, chama cha mazoezi ya viungo, pamoja wanyanyua vitu vizito pamoja na vyama vyengine.(Tafadhali angalia kiambatisho namba 6).

iii. Walimu wa michezo wamepatiwa mafunzo ya aina mbali mbali ili kuweza kuongeza ufanisi katika kazi zao. Walimu wa mpira wa miguu kupitia *ZFA* na *TFF* wamepatiwa mafunzo ya juu (*Advance*) na walipatiwa mafunzo ya daraja la 'C' yanayoandaliwa na Shirikisho la mpira wa miguu la Afrika (*CAF*) yaliyofanyika Zanzibar Aprili mwaka huu. Aidha, walimu wa mchezo wa riadha wamepatiwa mafunzo juu ya mbinu bora za utumiaji wa vifaa vya michezo hiyo, mafunzo hayo yamefanyika kwa mashirikiano na mwalimu kutoka Ujerumani kwa msaada wa Ubalozi wa Ujerumani. Kwa upande wa mchezo wa kriketi, mafunzo yametolewa kwa walimu wa michezo kutoka skuli mbali mbali kwa mashirikiano na Shirikisho la Kriketi la Afrika kupitia Chama cha Kriketi Tanzania (*TCA*) yenye lengo la kufufua mchezo huo hapa Zanzibar. Aidha, mabaraza ya michezo ya wilaya zote yamejengewa uwezo kwa kuwapatia mafunzo juu ya namna ya kuendesha shughuli za michezo katika ngazi za wilaya kwa ajili ya kuimarisha michezo nchini. Pia walimu wawili wa mchezo wa Mpira wa Vinyoya pamoja na walimu wawili wa mchezo wa karati wote wamepatiwa mafunzo ya michezo hiyo nchini China kwa mashirikiano na Balozi wa China.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Baraza la Taifa la Michezo limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

I. Kuimarisha programu za vyama vya michezo vya taifa.

II. Kuimarisha shughuli za maendeleo ya michezo za mabaraza 10 ya wilaya za Zanzibar.

III. Kuimarisha miundo mbinu ya michezo katika Ngazi ya Wilaya

Mhe. Mwenyekiti, ili Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar liweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Shilingi 147,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

SHUKRANI

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumaliza hotuba yangu naomba kuwashukuru wote waliochangia katika kuitayarisha hutuba hii. Shukrani za pekee na za utiifu mkubwa zimwendee Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Muhammed Shein kwa muongozo anaotupa ambao wizara imeuchukua na kuufanya kuwa ndiyo dira ya utekelezaji wa shughuli zake katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Saba.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani maalumu zimwendee Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Ofisa Mdhamini Pemba, Kamishna, Wakurugenzi wa Wizara yangu na taasisi mbali mbali na wafanyakazi wote kwa kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na uadilifu mkubwa. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, wamekuwa wakinisaidia sana katika kipindi hiki cha miezi yangu

mitatu kutekeleza majukumu yetu. Pia nawashukuru Wenyeviti wa Mabaraza na Bodi mbali mbali kwa kusimamia vyema taasisi zetu na kunishauri kwa busara.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuishukuru Kamati yako ya Mifugo, Uwezeshaji, Habari na Utalii hasa mwenyekiti wake ambaye kwa kweli aliwahi kuwa Naibu Waziri katika wizara hii, uzoefu wake umenisaidia sana, wametoa mchango mkubwa sana katika shughuli zetu za wizara zetu na imetusaidia sana katika kuweka vizuri bajeti ya wizara yangu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwashukuru wafanyakazi na wanamichezo, wasanii, washiriki wa utalii na wananchi wote kwa Unguja na Pemba kwa mchango wao katika kufanikisha shughuli zao wizara. Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa ni mwizi wa fadhila kama sitoshukuru Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ushirikiano mkubwa waliotupa kwa mahitaji ya fedha hasa wakati wa dharura.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kushukuru kwa namna yake Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China hasa Balozi wake Madam Chin Ching kwa misaada yao katika sekta ya habari, michezo, utamaduni na utalii.

Aidha ninaishukuru Serikali ya Misri, Oman, India, Korea, Dubai, Iran, Ujerumani, Japan, Uingereza na Marekani kwa mashirikiano na misaada yao ya kitaaluma na ya kihali katika fani ya habari, utamaduni, utalii na michezo.

Vile vile ninapenda kuwashukuru mashirika ya kimataifa ya *UNICEF*, *UNESCO, ADB, UNDP*, Jumuiya ya Ulaya na *JECA*, pia naomba kushukuru kampuni inayotengeneza vinywaji wa *Grand Malt*, pia hoteli ya *Ocean View, Zantel, Vodacom, Tigo* na Shirika la Mfuko wa Taifa wa Hifadhi Jamii ya Tanzania kwa kutuunga mkono katika kufanikisha mashindano yetu mbali mbali katika sekta ya michezo na utamaduni.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani za pekee ziende kwa timu zangu za Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kunyakua kombe la NSSF kwa upande wa mpira wa miguu na netball jambo ambalo lilileta faraja kubwa kwa wizara na Zanzibar kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani nyengine za pekee ziende kwa timu za Judo kwa ushindi wa jumla wa Afrika ya Mashariki na Kati kwa kupata medali 14 za dhahabu, Zanzibar Heroes kwa ushindi wa tatu wa VIVA World Cup na timu ya vijana kunyanyua vitu vizito kwa kupata ushindi wa tatu huko Uganda.

Vile vile ninapenda nimpongeze mtoto Hemed Bakari kwa kushinda mashindano ya watoto wenye ulemavu wa akili katika mbio za mita mia nne na kunyakua medali ya dhahabu katika mashindano hayo ya dunia yaliyofanyika huko Ugiriki.

Aidha nimpongeze mchezaji wa soko Adamu Nditi akiwa Mzanzibari wa mwanzo kuweza kusajiliwa na timu maarufu ya Chelsea. Hii ni fahari kwa Wazanzibari wote. (Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi pamoja na Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na uvumilifu. Aidha ninatanguliza shukurani

zangu kwao kwa michango yao watakayoitoa ninaamini kwamba watanielekeza na kuniongoza na baadae kuijadili hotuba hii. Ninaamini kabisa michango hiyo itasaidia sana wizara yangu katika kutekeleza malengo yake ya mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, wizara Waheshimiwa Wajumbe ni wizara yao na wananchi wao na majimbo wanayowawakilisha, sekta za habari, utamaduni na michezo zimegusa maisha ya Wazanzibari wote hasa michezo.

Mhe. Mwenyekiti, najua wewe binafsi ni mpenzi mkubwa wa mchezo pia wengi wa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ni wapenzi wa michezo. Kuna wengine miongoni mwa wajumbe hawa huwa ni wachezaji wenyewe, nawaona katika michezo na viwanja mbali mbali. Kuna wengine hupenda kucheza katika viwanja vikubwa na wengine hupenda kucheza katika vile viwanja ambavyo wanaita indoor games, wote wanacheza vizuri na ninawapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninaliomba sasa naomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni nane milioni mita tisa na tisini na sita kwa kazi za kawaida na shilingi milioni mia sita kwa kazi za maendeleo. Pia liiidhinishe kukusanya mapato ya shilingi bilioni moja, milioni mia saba na hamsini na nane na laki mbili kwa wizara yangu kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Asha Bakari Makame (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Uwezeshaji, Habari na Utalii) Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma na mwenye kurehemu ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako tukufu kwa minajili ya kujadili bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ili kuleta na kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka 2012/2013.

Kabla sijaendelea Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba nichukue nafasi hii kutoa pole kwa wale wote ambao waliofikwa na msiba mkubwa wa tarehe 18, tunawaombea marehemu wote awalaze mahala pema peponi Amin. Na pia wale waliofiwa wote Mwenyezi Mungu awape moyo wa subra.

Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kutoa pongezi na shukurani maalum kwa Mhe. Waziri na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na watendaji wote wa Wizara hii, kwa jitihada wanazozionesha katika kutekeleza majukumu yao na kushirikiana bega kwa bega na kamati hii kila wanapohitajika kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi kamati yetu imekuwa ikifanya kazi kwa mashirikiano makubwa yanayoleta tija na ufanisi wa hali ya juu. Hivyo nichukue fursa hii basi kuwapongeza na

kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa umahiri na umakini wao mkubwa wakati wa kupitia bajeti ya wizara hii.
Naomba niwatambulishe kwa majina Wajumbe kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Asha Bakari Makame Mwenyekiti
2. Mhe.MohamedSaidMohamed M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Mzee Ali Mjumbe
4. Mhe. Asaa Othman Hamad Mjumbe
5. Mhe. Salim Abdalla Hamad Mjumbe
6. Mhe. Abdi Mosi Kombo Mjumbe
7. Mhe. Viwe Khamis Abdalla Mjumbe
8. Mhe. Kazija Khamis Kona Mjumbe
9. Ndg. Asma Ali Kassim Katibu
10. Ndg. Haji Khatib Haji Katibu

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la faraja kuona kuwa kwa mwaka huu wa fedha unaomalizikia 2011/2012, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo imevuka lengo la kukusanya mapato ya yaliyokadiriwa kwani Wizara hii ilikadiriwa kukusanya mapato ya shilingi bilioni moja mia mbili na kumi na mbili milioni na laki nane ambapo hadi kufikia Aprili, 2012 wizara ilikuwa imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni moja mia tatu, kumi na tisa milioni laki tatu na tisini na nane elfu mia nne na thalathini na moja.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii imekusanya sawa na asilimia 109. Kwa mnasaba huu kamati inawapongeza viongozi na watendaji wa Wizara hii kwa kusimamia vyema na utekelezaji mzuri wa majukumu yao ya kazi ilivyopelekea Wizara hii kuvuka lengo la kukusanya mapato na hivyo kuongeza zaidi mapato katika mfuko mkuu wa Serikali.

Aidha kamati inatoa wito kwa viongozi na watendaji kuendeleza ari na juhudi katika kazi zao ili nao mwaka huu wa fedha 2012/2013 waweze pia kupata mafanikio zaidi katika ukusanyaji wa mapato kama ilivyokuwa kwa mwaka uliopita.

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya habari ina umuhimu katika nchi yoyote hapa duniani, kwa vile ndio sekta inayobeba jukumu muhimu la kutoa habari, kuelimisha, kuburudisha na kufahamisha jamii juu ya masuala mbali mbali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Pamoja na mchango mkubwa wa sekta binafsi katika nyanja hii. Sekta hii imebeba na Shirika la Utanganzaji Zanzibar (ZBC), Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti ya Serikali, Tume ya Utangazaji na Chuo cha Uandishi wa Habari.

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya malengo yaliyopangwa na Shirika la Utangazaji Zanzibari katika mwaka wa fedha 2011/2012 ni kuhamisha mnara wa masafa kati ya kutoka Chumbuni kwenda Bungi ili kurahisisha ndege kutua kwa usalama ambapo katika utekelezaji wake umeelezwa kuwa shirika limefanikiwa kuhamisha mnara huo pamoja na kujenga nyumba za kisasa za wafanyakazi huko Bungi. Kamati imeshuhudia ujenzi wa mnara huo unaogharamiwa jumla ya shilingi milioni mia tatu na kuona kuendelea vyema ambapo asilimia 75 ya ujenzi huo umekamilika.

Aidha kamati inatoa indhari kwa Wizara kuwa makini katika kuhakikisha kuwa ujenzi wa mnara huo unafanyika katika kiwango kinachokubalika pamoja na kuhakikisha kuwa fedha halisi zilizotengwa kwa ujenzi kutumika kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Utangazaji ni chombo kilichoundwa kimsingi kwa ajili ya kusimamia vyombo vya utangazaji vya Serikali na vya binafsi vinavyoainishwa hapa chini kama ilivyoelezwa kuwa kwa mwaka 2012/2013, tume hii imepanga kutekeleza malengo kadhaa yakiwemo ya kuratibu shughuli za utangazaji wa digital nchini kwa kutoa muongozo na maelekezo ya kitaaluma kuhusu taaluma hiyo mpya pamoja na kuandaa kuendesha kampeni ya kitaifa ya elimu wa umma juu ya mageuzi ya teknolojia ya utangazaji nchini.

Aidha Tume inatarajia kupatiwa jumla ya shilingi milioni mia moja kama mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mradi wake wa kuimarisha mawasiliano kutoka analogue kwenda *digital* kama inavyooneshwa katika kasma elfu saba mia nne ziro ziro moja.

Kutokana na malengo hayo pamoja na kutengwa kwa fedha hizo na zile za mkopo zinazofikia dola za Marekani thalathini na nane milioni zinatarajiwa kutolewa na Benki ya Exim ya China. Bado suala la mageuzi ya matumizi ya teknolojia ya *analogy* kwenda katika digital ni jambo linalokabiliwa na changamoto kubwa hususan wa ufahamu mdogo wa wananchi katika masuala ya digital.

Hivyo ni jukumu la Serikali kujidhatiti zaidi na kufanya maandalizi mazuri na ya nyaraka ikiwa pamoja na kutenga fedha nyingi zaidi zitakazowezesha utoaji wa elimu ya kutosha kwa digital kwa wananchi wote wa Zanzibar hasa ukizingatia kuwa ifikapo tarehe 31 Disemba, 2012 nchi yetu inatakiwa iwe imeshaingia kikamilifu katika kutumia teknolojia ya *digital* na kuachana na teknolojia ya *analogy* ambayo tumeizowea kuitumia kwa miaka mingi sasa. Msukumo mkubwa zaidi wa Serikali unahitajika.

Juu ya suala hili la kuleta matumaini kwa wananchi hadi hivi sasa hakuna hata majaribio yaliyofanyika ya kuweza kurusha matangazo kwa kutumia teknolojia ya digital kutokana na kukosekana kwa miundombinu ya teknolojia hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kuunganisha televisheni ya Zanzibar (TVZ) na Sauti ya Tanzania Zanzibar na kuunda Shirika la Utangazaji Zanzibar ili kuimarisha huduma ya taasisi hizo na kuleta ufanisi zaidi katika kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha 2012-2015 Shirika linaombewa jumla ya shilingi bilioni mbili milioni kumi na sita, mia mbili na ishirini na nne kwa matumizi ya kawaida na shilingi milioni milioni mia moja kwa kazi za maendeleo ili kutekeleza malengo yake mbali mbali pamoja na mafanikio kadhaa yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo ya shirika katika mwaka mwa fedha unaomalizika. Kamati inapenda kusisitiza kuwa bajeti ya mwaka huu iende sambamba na ufanisi wa utoaji wa habari kwa wananchi, viongozi na watendaji wa shirika hili hawana budi kubadilika kiutendaji na kufanya kazi zao kwa kufuata sheria, taratibu na maadili ya kazi zao hususan ya uandishi wa habari. Ni vyema kwa watendaji wa shirika hili kufanya uchanganuzi mzuri wa kutambua ipi ni habari na ipi si habari ya kutangazwa na kuoneshwa.

Aidha Serikali kwa upande wake inapaswa itoe msukumo maalum wa kibajeti kwa shirika hili ili kukuza zaidi ufanisi wake wa kazi ikiwa ni pamoja na kuinua ubora wa vipindi vinavyoandaliwa na shirika hili ili viende sambamba na kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia inayoikumba sekta hivi sasa. Kwa kutekeleza yote hayo shirika litaweza pia kupunguza malalamiko ya wasikilizaji na watizamajii wake na hivyo kulifanya lengo la kuundwa kwake kufanikiwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, utalii ni sekta kiongozi inatupatia nchi yetu fedha nyingi za kigeni, ndio inayotegemewa sana kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umaskini pamoja na kusaidia upatikanaji wa ajira hasa nchini kwa Wizara hii. Kamisheni ya Utalii, Chuo cha Maendeleo ya Utalii na Shirika la Utalii ndizo taasisi zilizopewa jukumu la kupanga, kusimamia, kuendeleza utalii na kuitangaza Zanzibar ili sekta hii iende sambamba na sera ya mikakati ya Serikali katika malengo makuu, kuimarisha uchumi wa taifa na kupunguza umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Utalii kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012 imefanikiwa kutekeleza malengo mbali mbali iliyopangiwa ikiwemo kushiriki katika maonesho mbali mbali ya kitaifa na kimataifa kwa lengo la kuitangaza Zanzibar kiutalii. Hata hivyo, kamati imeona kuwa ipo haja kubwa ya Wizara na serikali kwa jumla kulipa mkazo maalum suala la kufanya utafiti wa kina juu ya mbinu ya kupata masoko ya utalii kwa kuyaendeleza yaliopo na kuibua mengine mapya yatakayowezesha kupata watalii wengi zaidi wa daraja la juu kutembelea hapa nchini.

Aidha bajeti kubwa zaidi inapaswa itengwe katika kutangaza Zanzibar kimataifa kama wanavyofanya nchi za wenzetu ikiwemo nchi ya *Seychelles* ambayo hutenga fedha nyingi sana kuimarisha masoko ya utalii na kuitangaza nchi yao kiutalii.

Aidha kwa vile utalii ni sekta inayogusa maeneo mbali mbali ni vyema uimarishwaji wa maeneo hayo pamoja na miundombinu inayohusiana na sekta ya utalii iende sambamba na kasi ya ukuaji wa mchango wa sekta hii katika pato la taifa.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti ya Kamisheni ya Utalii kwa mwaka 2012/2013 ni shilingi bilioni moja mia tatu na kumi na nane milioni kwa kazi za kawaida na inatarajiwa kukusanya shilingi bilioni moja mia mbili na mbili milioni kwa mwaka wa fedha unaomalizikia 2011/2013. Kamisheni ilikaridiwa kukusanya shilingi mia nane na arobaini na mbili milioni ambayo imefanikiwa kupata shilingi mia tano na tisini mbili elfu nne mia nne mia moja na sabini na mbili sawa na asilimia sitini na tano.

Hivyo ni vyema kwa Kamisheni hii kufanya juhudi zaidi za kuhakikisha kuwa mapato yanayokadiriwa kukusanywa yanafikia kwa asilimia kubwa zaidi kwa kuandaa mikakati madhubuti ya kuziba nyaya yoyote inayoingia uvujaji wa mapato unaotokana na kamisheni hii.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyokumbuka kuwa katika kikao cha Aprili, 2012 Baraza lako tukufu tulipitisha marekebisho ya sheria ya utalii Na. 6 ya mwaka 2009. Marekebisho hayo yalilenga katika kufanya utalii uwe endelevu na wenye tija zaidi kiuchumi na kijamii na kufutilia

mkazo ulindaji wa silka, mila na desturi ya Zanzibar kwa kubeba dhana pana zaidi ya utalii kwa wote.

Ni matumaini ya kamati hii kuwa bajeti inayoombwa na Kamisheni ya Utalii kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 itawezesha kuelimisha hayo ya utekelezaji kikamilifu yale yote yaliyoainishwa katika sheria hiyo. Hususan suala la kulinda, kuendeleza na kukuza utamaduni wa kiasili wa Zanzibar kama ni sehemu ya bidhaa ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Utalii ni shirika la Serikali ambalo hufanya shughuli mbali mbali za utalii hapa nchini ikiwemo kuongeza huduma bora kwa watalii wanaoshughulikiwa na shirika. Aidha kama inavyofahamika kuwa katika mwaka 2011/2012, malengo ya Shirika la Utalii hayakuweza kutekelezwa kutokana na kwamba kwa kipindi kirefu shirika hilo halikuweza kufanya shughuli zake na kwamba Serikali inaendelea kufanya tathmini kama shirika hilo lina misingi ya kuendelea au laa.

Mhe. Mwenyekiti, tarehe 19/12/2011 katika kazi za kawaida Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ilipata nafasi ya kutembelea hoteli za Wete, Chake-Chake na Mkoani Pemba zinazomilikiwa na Shirika hili ambazo zimekodishwa kwa kampuni ya *Multinational Marketing*. Kutokana na hali mbaya zinazokabili hoteli za Wete na Mkoani, kamati iliagiza Shirika la Utalii kuzirejesha hoteli za Wete na Mkoani mikononi mwa Serikali, kwani hadi sasa mkodishwaji ameshindwa kuziendeleza.

Kwa mnasaba huo ninapenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kuona hali ya hoteli hizo na kuanza kutekeleza agizo la kamati yetu kwa kuagiza mkodishaji huyo anyang'anywe hoteli ya Wete kama ambayo taarifa ya agizo lake ilivyoambatanishwa katika gazeti la Zanzibar Toleo Nambari 3777 la tarehe 7 Juni, 2012.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeendelea kusisitiza juu ya kupatiwa upya kwa mikataba ya ukodishwaji wa hoteli za Pemba zinazomilikiwa na shirika hili, kwani hoteli hizo ni raslimali muhimu zinazoweza kuingiza mapato mengi zaidi kwenye serikali yetu pindi zinapotumiwa na kuendelezwa vizuri kwa maslahi ya nchi yetu na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Utalii ni taasisi iliyopewa jukumu la kutoa taaluma itakayowezesha kujenga raslimali watu wenye ujuzi, taaluma stadi zinazokabili katika viwango vya kimataifa ili kuimarisha sekta ya utalii hapa nchini. Hivyo basi, kamati inashauri Wizara kukipa muongozo na msukumo maalum chuo hiki katika mwaka wa fedha 2012/2013, ili kutimiza azma ya kutoa wahatimu bora na watakaondoa vijana wa nchi katika janga sugu la ukosefu wa ajira.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mafanikio mbali mbali yaliyofikiwa katika chuo hicho ikiwa ni pamoja na kukuza taaluma, walimu wake pamoja na kuimarisha mitaala na miundombinu ya chuo hicho. Katika mwaka wa bajeti unaomalizikia kamati imeona kuwa bado kuna haja kubwa kwa Serikali kutoa msukumo zaidi kwa chuo hicho ili kiweze kusomesha fani za juu zaidi katika kiwango cha shahada ili kiwe na hadhari kubwa zaidi kitaifa na kimataifa.

Aidha kamati inapenda kuikumbusha Serikali kuhusu suala zima la tishio la mmomonyoko wa ufukwe uliokaribu karibu kabisa na chuo hicho unaosababishwa na mawimbi ya bahari. Tatizo hilo linahitaji uchunguzi wa kitaalamu na bajeti mahususi itakayoweza kulipatia ufumbuzi wa kudumu kabla haijatokea athari zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sote tunafahamu kuwa michezo hujenga afya bora, hudumisha udumu na urafiki miongoni mwa wanamichezo na pia hutangaza nchi na kuimarisha mahusiano ya nchi hususan kimataifa na kitaifa. Ninapenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya kamati kutoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kuiwezesha timu yetu ya taifa ya mpira miguu ya Zanzibar Heroes kushiriki katika mashindano ya kombo la dunia kwa nchi zisizo wanachama wa FIFA yaliyofanyika mwanzoni mwa mwezi wa Juni mwaka huu huko nchini Iraq.

Aidha, kamati inatoa pongezi za dhati kwa timu yenyewe ya taifa ya Zanzibar Heroes kwa kuweza kushika nafasi ya ushindi wa tatu katika mashindano hayo yaliyoshirikisha nchi tisa na kuidhinishia ulimwengu kuwa vijana wa Kizanzibari wapo imara katika fani hii ya mpira wa miguu.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa taasisi zisizo za michezo hapa nchini zikiwemo Kamisheni ya Utamaduni na Michezo na Baraza la Taifa la Michezo limejitahidi kuelekeza malengo yake katika bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012. Bado sekta hii ya michezo inakabiliwa na changamoto nyingi zinazohitaji utafiti na mipango ya kina ili kuweza kuzipatia ufumbuzi wa kudumu.

Baadhi ya changamoto hizo ni kukosekana kwa viwanja vya michezo kama mpira wa meza ambao ni table tennis na vyenginevyo kwa Unguja na Pemba. Uvamizi wa viwanja vya michezo, kukosekana kwa *program* maalum ya kuibua vipaji vya michezo pamoja na ushirikishwaji hafifu wa wachezaji wa vyama vya michezo vya Zanzibar katika mashindano ya kimataifa. Hivyo kamati imeshauri kuwa bajeti za taasisi hizi za kusimamia michezo zilenge katika kuzitatua changamoto hizo kwanza kwani kunachangia kwa kiasi kikubwa huduma ya maendeleo ya michezo hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ina furaha ya dhati kwa kupata fursa ya kujionea ujenzi wa kingo za Hoteli ya Bwawani ambayo ilikuwa inakabiliwa na tishio la mmomonyoko wa ardhi. Haya ni matokeo ya uongozi imara wa Mhe. Waziri ambaye amezingatia malengo ya wizara yake na maagizo ya kamati kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Tunaipongeza Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kutekeleza agizo hili la kamati kuinusuru hoteli ya Serikali ambayo ni Hoteli ya Bwawani kutokana na uharibifu mkubwa unaonekana na nguvu za maji ya bahari. Hatua inayofuata ni kuendeleza ujenzi huo kwa eneo zima zinalozunguka hoteli na kufanya matengenezo kila haja ya kufanya hivyo inapotokea.

Mhe. Mwenyekiti, kila nchi katika dunia hii ina historia yake na kielelezo muhimu katika historia ya nchi hii ni mambo yake ya kale, yakiwemo magofu, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na taasisi iliyopewa jukumu la kuenzi, kuhifadhi na kuendelea historia ya

Zanzibar kwa kutumia makumbusho, magofu na mambo ya kale. Hivyo utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi ni jambo muhimu sana ili kuhifadhi uridhi wa historia na utamaduni wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa ninapenda kuwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa uvumilivu wao na kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa wakati wote wa uwasilishaji wa hotuba hii.

Aidha ninapenda kuwaomba wajumbe wako wachangie bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kwa utulivu na umakini na hatimaye kuipitisha.

Kwa niaba ya kamati yangu ninaunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaondoka na mimi kwa sababu nikishakukaa kitako nitakuwa sipati kuchangia yale machache niliyonayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninachukua nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa muda mfupi wa miezi yake mitatu ambayo aliteuliwa na Rais, kwa kweli ameonesha umahiri na umakini wa utendaji wake wa kazi.

Mtu lake mpe akiwa na sifa yake mpe, hana sifa mchafue. Kwa hivyo mimi ninachukua nafasi kwa kweli kumpongeza sana Mhe. Waziri, hongera sana. Matumaini yangu kwamba uzi huo huo uliotoka nao kwenye mfumo wa uvuvi utakuja nao Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. (*Makofi*).

Lakini pia nichukue nafasi hii kwa sababu huu uzio wa ukuta wa Hoteli ya Bwawani ni miaka mingi sana kwa kweli. Nimpongeze sana Mhe. Waziri na niipongeze sana hoteli hii, kwa sababu fedha hizi zimetoka katika mfuko wa Hoteli ya Bwawani ni shilingi thalathini na moja milioni. Nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wafanyakazi wa hoteli hii.

Aidha pia pongezi nyingi sana niwape Wizara nzima kwa jumla kwa jinsi wanavyomsaidia Mhe. Waziri kufanya kazi zake vizuri. Kama si wao basi Mhe. Waziri kwa sababu ni mpya amekwenda miezi mitatu tu, basi kama si wao Mhe. Waziri asingeweza kufanya kazi zake vizuri, wangembabaisha wakamtia huku na kumtoa huku ikawa kama kipindi kilichopita *inshallah hewalla*, lakini kwa kweli niwashukuru sana wafanyakazi.

Lakini nitamuomba Mhe. Waziri tujali mambo ambayo watu wanafanya tafiti mbali mbali. Kuna tafiti hapa zimefanywa na wadau kuhusu sheria ya vyombo vya habari. Mimi ningekuomba Mhe. Waziri watu wanapofanya tafiti na wanapojitolea kutaka serikali iweze kuwasaidia, nitakuomba sana kwa sababu sisi tulihudhuria semina hiyo na kwa kweli mimi nimepata taarifa kuwa wamekuletea wadau taarifa zao ambazo kwa miswada kutungwa sheria, si wao watakaotunga sheria ni sisi, ni Wizara ambayo ndio inayoweza.

Nakuomba sana Mhe. Waziri awaite wadau hawa au ile taasisi ambayo inayohusika iwasikilize na kama kweli kutokana na kifungu cha 18 (2) cha Katiba ni kweli kuna haki za habari, kuna

haki za mtu kupata habari. Kwa hivyo nitakuomba sana Mhe. Waziri suala hili ulichukue ili tuweze kipindi tunachopita kama ni kufanya *process* zote basi tuweze kupitisha sheria hizi mbili ambazo wenzetu wamefanya kwa nia safi kabisa.

Na mimi nichukue nafasi hii ya mwisho Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Balozi wa China kwa kweli kipindi kifupi tu alichokwenda Mhe. Waziri kwa miezi mitatu na kwa vile tulikuwa naye katika safari hizi, wamekuwa hivi sasa ni marafiki zake sana, ameomba nafasi kwa kweli za kusoma, hakuna kusoma muda mfupi wala mrefu, madhali kusoma ni kusoma vipindi vifupi wafanyakazi 20 Balozi wa China wamewapatia watu wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwenda kujifunza mambo hayo.

Baada ya kusema mambo hayo, nichukue tena nafasi hii nimshukuru sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri jinsi wanavyoleta mashirikiano na kamati yetu pamoja na wafanyakazi wote. Naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe baada ya kwisha kumsikiliza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati na kwa vile muda umetuacha nyuma, tuwaombe basi wale wajumbe ambao wataanza kuchangia sasa kujitahidi kila mjumbe atumie dakika 20 ili tuweze kuwa wachangiaji wengi kwa msinigi wa kwamba kesho asubuhi tukijaaliwa kufika hapa tuweze kuendelea na majumuisho.

Kwa kuanza basi tutaanza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, baadae atafutiwa na Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninakubaliana na wewe kwa kuweka kanuni kando badala ya kupewa dakika 30 na kupewa 20 sina tatizo nazo, lakini panapohusika utanisaidia kidogo.

Kabla ya hapo sijaanza kuchangia ni lazima tukubaliane kuwa tuwapongeze hasa hawa ndugu zetu timu yenye ulemavu kwa kutuletea dhahabu hizo na hasa akiwemo mwanamama. Mimi ninatoa pongezi sana na ninamuelekea Mheshimiwa Makamu wa Pili ningemuomba sana ni faraja sana akipiga nao picha na kuwaalika futari japo siku moja ili na wao akawapongeza.

Ninaamini hivyo Makamo anafanya kitu kama hicho na hasa hususan kutokana na wenzetu na maumbile yao walivyo na kutuletea hiyo *gold medal* ninawashukuru sana na hata wananchi wa Jimbo la Kitope wanawaunga mkono kwa kitendo hicho.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ninakwenda katika hali ambayo ya kuchangia hotuba hiyo ya Mhe. Waziri kama alivyoelezwa hapo na Mhe. Mwenyekiti ambaye bado ni mpya na Wizara hii lakini ni mrithi wa mambo ambayo yaliyoachwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiingia katika ukurasa wa 21. Sitaki mimi nisokotane naye sana mimi Mhe. Waziri lakini kama sikumuonesha ubovu wake atakuwa si mzuri. Lakini ni lazima nieleze yale mabovu yaliyokuwemo ili aweze kuyatekeleza azidi kuwa mzuri zaidi kama alivyosifiwa na Kamati yake.

Mhe. Mwenyekiti, hasa hapa katika ukurasa 21 tunapokwenda kwenye mnara huo wa Bungi. Mhe. Mwenyekiti, leo mimi ninataka maelezo tu hapo wala sitaki maneno mengi. Kwa taarifa za chini chini tu nimesikia kwamba jengo limekwenda vizuri haraka haraka ambapo hata mwenyewe Mhe. Rais kafurahishwa sana.

Lakini ninataka nimuulize Mhe. Waziri huo mnara wetu lini utakamilika na kama ikiwa kuna muda ambao waliekeana wa utekelezaji ufike muda fulani na kama umesimamishwa, hebu aniambie ni sababu gani ambazo zilizotupelekea kuweza kusimamishwa pengine kwa upungufu wa fedha au nini au baadhi ya vifaa. Naomba sana hilo aje kunielezea ili nisiweze kuja kumzuilia fungu lake hapa awe mzuri kutokana alivyosifiwa na Kamati.

Niende ukurasa wa 42 Kamisheni ya Utalii. Mhe. Mwenyekiti, hii Kamisheni ya Utalii niseme kama ni uti wa mgongo sasa hivi kwa kutupa faraja ya mambo ya kututafutia fedha za nje. Lakini Mhe. Mwenyekiti, maslahi yake ya wafanyakazi ni madogo mno tofauti na sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, siku zote huwa tunasema hapa kuwa maslahi na kwa kusema vile ni kwa sababu tunapenda sana wafanyakazi wetu wawe na maslahi mazuri ili wafanye kazi kwa uadilifu. Hali ya nchi yetu tunaielewa, vitega uchumi hivi sasa vimekuwa kidogo, uchumi unapungua. Pamoja na hayo tunapokuwa hawa tukiwaongeza fedha Kamisheni hii ndio itakuwa katika hali nzuri.

Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hawa watu ambao wanaotutafutia fedha nyingi sana na masoko makubwa ya nje, halafu leo tukiwapa maposho kidogo kwa kweli haistahiki. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, hata ule usafiri wao naona hauridhirishi. Kwa kweli ninaomba sana katika majibu yako mazuri yatakayofanya nikuunge mkono ni moja hilo kuwatafutia usafiri wa uhakika na ambao tunaokwenda nao kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, tuende katika maonesho, Kamisheni hii inafanya kazi nzuri sana kwa kwenda kuvipeleka vipeperushi katika nchi za wenzetu kwenye maonesho ya kibiashara ya utalii. Lakini kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kutokana na bajeti inakuwa ni upungufu sana. Kwa kweli inasikitisha Mhe. Mwenyekiti, kuwa kuna mashindano sitini basi kwa kweli yanashindikana kupata thuluthi tuseme labda robo yake au nusu, kwa sababu hao wenzetu wakiwa na bajeti nzuri, wakiwezeshwa vizuri Mhe. Mwenyekiti, hawa ndio wanaotuletea utajiri. Kwa sababu huko nje kuna masoko ndio watakaokwenda kuyatangaza, sasa hivi tuna ushindani kwa masuala haya ya kibiashara na wenzetu. Sijui tuna tatizo gani au kuna ubakhili gani wa kuweza kuwaongeza vifungu au kuwapa bajeti yao kwa wakati unaotakiwa na kuwaruhusu kwenda katika kupiga debe huko nje katika maonesho haya ya kiutalii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli inasikitisha sana, tuna asilimia ndogo sana. Wewe ukiuliza mikutano yao kama inatimia pengine mitatu, safari zao walizokwenda au nne, tumeshakosa soko kubwa sana hapa. Sasa hivi soko kubwa ni la Wachina na Warusi, tumezubaa na fedha zenyewe hazipo.

Kwa hivyo, mimi ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, hebu tuwe *serious* na masuala kama haya, tunaamua kuweka hii kamisheni basi tuiweke na tuwe *serious* katika kuwatafutia mafunzo. Laa tunaamua kuiondoa basi tuiondowe, kwa sababu moja kati ya vitu vya kutafutia uchumi ni hiki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme ukweli, nimeshatembea nchi nyingi sana. Mhe. Mwenyekiti, kila ninapokwenda, nimeanzia Barcelona Wachina kibao, nimekwenda *Venice* Italy Wachina kibao, nimekwenda Ufaransa Wachina kibao na nimekwenda Austria Wachina kibao na nimemalizia Ujerumani kwa kuingia Zurich Wachina kibao, seuze leo Zanzibar wangeweza kuwezeshwa hawa, basi hawa wote soko tungelikamata. Sasa soko kuu la Watalii ni Machina. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, katika mambo yetu haya tuwe *serious* kabisa katika kuyafanya haya ili tuendelee vizuri katika masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mgongano wa sheria sasa hivi kati ya manispaa na wewe kamisheni yako. Hebu tuiweke sawa, kwa sababu hawa katika ulipaji wa leseni tunawayumbisha hawa wananchi wetu, hebu tu-s*tick* na sheria moja. Hizi sheria ikiwa kila mtu atakuwa na sheria yake za kodi, tunawaweka pabaya wananchi, tunawapa mzigo mkubwa sana. Hebu tukubaliane, tuweke kodi moja tu, hata kama ikiwa kubwa lakini kuwe na kodi moja tu. Sasa leo huyu manispaa ana yake, atakuja na mwengine ana yake na wewe una yako, tunakwenda wapi na tutawasaidia vipi hawa wafanyabiashara ndogo ndogo. Mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hili suala hebu tulisaidie sana.

Halafu kuna kikosi cha *patrol*, hebu nikuulize hiki sasa hivi hakina bajeti, nani mdhamini sasa hivi. Hebu Mhe. Waziri ukija hapa naomba sana uniambie kwamba kikosi hiki cha patrol kiko chini ya nani mdhamini sasa hivi, ili tuone bajeti yake ikoje. Naomba sana Mhe. Waziri unisaidie hilo, na uje kunijibu vizuri.

Vile vile suala la Bodi, Bodi imekwisha wakati wake au kama haijaanzishwa muda umeshafika sasa wa kuanzishwa, pengine Mhe. Rais ameshatia saini, muda kwa mujibu wa sheria tayari sasa hivi inatakiwa kiwepo hicho kitu, sijui sababu gani siku 21 zimeshatimia sasa hivi tangu Mhe. Rais asaini. Hebu tuwape sasa hivi fursa tuchaguwe hao viongozi watakaounda Bodi ili kuweza kuendesha, nayo bodi ina umuhimu wake. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kitengo hiki tukipe baraka tusikifanyie masihara kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika ukurasa 48 kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Utalii. Kwanza mimi niwapongeze sana walimu, nawapongeza sana walimu kwa jitihada zao za kuwasomesha vijana wetu. Siku moja mimi nilikwenda katika mdahalo mmoja, niseme mdahalo lakini ndio hivyo hivyo kati ya Wizara ya Mhe, Haroun hapo, Mhe. Waziri alituita siku hiyo tukenda pale, lakini kilichojitokeza pale ni malalamiko makubwa sana kuwa hatuwatumii wale ambao wanatoka moja kwa moja chuoni kabisa, wanakwenda kuwatafuta watu wengine na hili ndio tatizo ambalo linatukwaza sasa hivi. Ndio maana tunakosa wale ma PO wazalendo, hatari yake inakuwa kama hivi, kwa sababu hiki chuo hatukitumii.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri kuwa mkali sana na suala hili, chuo kitumiwe kuna walimu wazuri tu, sisi tunawaona hapa wanakuja kutuletea vitu vyao vinakuwa vitamu, tunanyang'anyiana hapa waheshimiwa, kutokana na ustadi wao ndio wale wale wanafunzi sio watu wengine. Sisi wenyewe tuna kipimo kizuri, kwa sababu humu waheshimiwa wote hapa mnakula vyakula vitamu na *standard*. Hakuna hata mmoja aliyepinga, akasema kuwa vyakula walivyopika wanafunzi hawa sio vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, leo tunawasomesha vizuri, wanagharamia wazee wao au pengine Serikali inagharamia, hatimaye wanaishia kwenye vijoblesi, tunawaweka wapi hawa. Twende kwenye mahoteli, nitafika huko kwenye mahoteli halafu tuangalie viwango vyao na idadi yao wako wangapi. Mhe. Mwenyekiti, mimi saa nyengine ninakuwa mkali, lakini sitaki niwe mkali Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna vitu tunavianzisha kwa nia nzuri tu, lakini hatimaye tunakwenda kuharibu. Sasa hapa ndio kitu kinanisikitisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika ukurasa wa 53 kuhusu Shirika la Utalii. Mhe. Mwenyekiti, shirika hili, nijiulize bado lipo au halipo kwa sababu naona miaka mingi sana sijalisikia hili. Mhe. Mwenyekiti, zamani walikuwa na mabasi mazuri, wakitoa sera zao vizuri na mashirikiano mazuri. Lakini hatimaye naona sioni faida yake, sijui kwa sababu gani. Naomba sana shirika hili kama lipo naomba uniambie kama lipo au limefutwa tujuwe vipi. Kama lipo basi kwa nini tusilikuze au kwa nini tusiwarejeshee heshima yao kama huko nyuma, imekuwa leo mkanganyano tu hawatambulikani naona wamo tu watu. Shirika hili ndio linahistoria zaidi ya kuweza kumtangaza mtu na kumsifia mtu. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hili shirika lipewe nguvu, kama alivyokuambia mwenyekiti wako naomba na hilo ulisimamie ulipe nguvu ili kuweza kusimamia masuala hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naingia ukurasa wa 57 kuhusu hoteli ya Bwawani. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hoteli ya Bwawani tumeitupa sana kusema ukweli, nilitegemea mimi hoteli ile katika *center* iliyokuweko pale itakuwa ni *five star*, lakini hata hivyo haimo katika *standard*, sijui niseme iko katika *standard* ya aina gani hoteli ile. Tumeiwacha, tunaivuruga wala hatuthamini kitu chetu kabisa, hiki kitu mimi ndio kinaniingiza uchungu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naingia uchungu na mambo mengi katika nchi hii, inaniuma sana nchi hii. Kitu kama kile Mhe. Mwenyekiti, Serikali ikafanya kwa jitihada zake kwa makusudi, iko sehemu nzuri sana hoteli ile, lakini tumeiwacha ovyo na tumeifungulia maofisi yaliyokuwa hayana msingi wowote. Haina heshima ya kusema kuwa ni hoteli ya kimataifa, ile ni mfano kama hoteli nyengine za Kilimanjaro Kempisky kule Dar es Salaam, ndio *center* kama ile, tunaiwacha tu.

Mhe. Waziri kama huna pesa sema tukutafutie pesa sisi tukupe ili uifanyie matengenezo ile hoteli, *serious* kabisa sio kitu cha mchezo. Lakini ubaya zaidi, tuingie ndani mule kwenye hoteli, wafanyakazi wake. Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wako kwa muda mwingi sana wamefanyakazi pale, wengine wana si chini kama miaka 14, kama nitakosea utanifanyia masahihisho, lakini haiwezekani isiwe hivyo, hata ile mikataba yao imekuwa ya kimipango mipango, sijui miezi sita, sijui mwaka mmoja. Hebu Mhe. Mwenyekiti, tukae vizuri, mimisitaki siku hizi kusema tuunde kamati teule, kwa sababu nakuaminini mawazo ya mawaziri mnatekeleza wajibu wenu kabisa, mko *serious*. Kila mkikosolewa nyinyi ndio mnapata speed ya kwenda mbio na ndio inavyotakiwa kiongozi akubali kukosolewa ili atekeleze wajibu wake ndio inavyotakiwa. Sio tena unakosolewa wewe unaanza kuvimba mashavu kama paka wa Bwawani, haiwezekani hiyo.

Naamini Mhe. Waziri nitakapokuambia masuala haya utawasaidia sana tu. Mhe. Waziri hawa watu wasaidiwe, kama kulikuwa kuna fedha zao nusu nusu, hebu tuwapeni fedha zao zikamilike ili waweze kufanya kazi zao kwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, turudie tena tusiwakasirikie vijana wetu. Lakini isitoshe Mhe. Mwenyekiti, sio hoteli hii ya Bwawani, namuomba sana Mhe. Makamu akusaidie ripoti ile ya hoteli ya Venta kule kwetu Kiwengwa inasikitisha sana, hebu mheshimiwa lichukulie kifua hili. Sasa naingia kwenye jimbo, hoteli ile kuna wananchi wamekopa pesa nyingi, wengine wanatishiwa amani kupelekwa mahakamani, wengine wamehasimiana, lakini mpaka leo hatujapata jibu ya hoteli ile ya Venta. Kama Serikali imeshindwa kuwatekelezea, wafanye tathmini wale wananchi wanaodai walipwe angalau vile vijumba kila mtu awe na chake, itakuwa ni *solution* ya ugomvi. Kwa sababu yule mwananchi atakapopewa kijumba chake, akakitia thamani akakiuza kile kile ili aweze kulipa makodi ya watu, vyengine vyovyote tunawaweka wapi hawa. Kwa kweli mheshimiwa tuna dhana nzuri Serikali, lakini baadae sijui inatekeleza wapi, sijui niseme kwa watendaji, sijui kwa nani, kwa kweli tunawasumbua wananchi na ndio njia moja ya kuwaondoshea umaskini. Wananchi wa Zanzibar mimi nashangaa sana kuambiwa maskini na sipendi kutumia neno hilo kuwa wananchi wa Zanzibar kuwa ni maskini hata kidogo, kwa sababu uchumi tunao Zanzibar.

Kwa hivyo, mimi naomba sana hili suala Mhe. Waziri nenda kwa Mhe. Makamu aliendeleza vizuri sana suala hili, lakini nafikiri alishindwa na sheria tu, lakini alikuwa mkali, tulikwenda ziara tukaona lile jengo jinsi linavyoharibika. Leo halifai jengo lile hata kidogo. Sasa mimi naomba tusaidiwe sana. Halafu isitoshe tunaomba sana Mhe. Waziri, kuwa mkali sana na suala la asilimia la Wazanzibari kufanya kazi kwenye mahoteli na hasa wale waliokuwa katika ukanda ule wa hoteli wasaidieni sana, kwa sababu wananchi kwa mfano wamekwenda sehemu kwa mfano kama ya Kiwengwa. Kiwengwa wamefunga njia, wametoa mambo yao yote na hatimaye wale wanakuwa wanafukuzwa, hawafai hawafai kwa nini.

Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Waziri kwa hili suala uliangalie na ulifanyie kila la heri. Kwa hivyo, naomba sana wananchi wangu wakubalike kuwapa kazi katika maeneo ambayo yaliyokuwa ukanda, wale wananchi wote waliokuwa chini ya mahoteli, sio wakae wanuse harufu tu za vyakula, waende wakafanye kazi wenyewe na wapewe heshima. Leo Kitope nzima ile mahoteli kibao, vijana wanatembea tu mitaani hawana kazi yoyote kwa sababu gani, nini maana ya kuwekwa mahoteli yale.

Mhe. Waziri naomba mimi na wewe tufanye ziara ili tuhakikishe ni asilimia ngapi za wananchi wa Kitope wanafanyakazi kwenye mahoteli, niko tayari mimi mheshimiwa. Siotuwaachie tu hawa vijana wetu wahangaike, sisi ndio tuwasemee humu na mimi nitaendelea kuwasemea humu kwa sababu mheshimiwa naiona dhiki wanayoipata wale wananchi wetu, tuwaondolee umaskini kwa kupitia bajeti hizi.

Kwa hivyo, mimi nasema niko *serious* kwa suala kama hili, nitakamata bango ili nihakikishe wananchi wanaondokana na umaskini katika nchi yao, sio kwenye ardhi ardhi yao.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika utamaduni na michezo. Mhe. Mwenyekiti, utamaduni wetu tunauelewa, naomba sana tuzidishe utamaduni wetu na hasa katika masuala ya majengo yetu yale ya kizamani ambayo tunafadhiliwa na UNESCO. Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wanafanya hivi, kwa mfano Ujerumani wanakuwa na *special day* katika zile *street* wanaweka sehemu za viji-*show* ili watu wanakuja kutoka nchi mbali mbali, wanatizama zile *show* halafu

wanatizama na yale majengo yenyewe. Mhe. Mwenyekiti, pale unapata kujitangaza vizuri sana. Naomba sana hili suala tulikamate na hapa naingia katika ukurasa wa 65 kuhusu makumbusho ya kale. Nimsifu sana muhusika wa mambo haya kama ni Mkurugenzi anajitahidi hivi sasa hata yale Makumbusho *Alhamdulillah* yanatizamika, lakini tumuwezeshe kwa sababu huyu sasa anayo kazi kubwa ya kuelimisha jinsi gani mambo yetu tuliyokuwa nayo ndani ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu kule nje wanakwenda kuangalia kama vile China kuna ukuta mkubwa ule, Ujerumani kuna nyumba walipigana Marekani na Wajerumani, mtu anakwenda kutizama ile risasi jinsi gani iliingia kwenye ule ukuta.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zingatia muda.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, namalizia lakini bado kidogo. Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ya Makumbusho ya Kale naomba sana wasaidiwe, ili awezeshwe huyu mhusika aweze kufanya kazi zake kwa uangalifu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kuhusiana na mambo ya michezo yetu ya ridhaa. Kwa kweli nilisema hapa kwamba wanamichezo wetu walipewa nafasi za kwenda nje. Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba hichi Chama cha Riadha hatujakitendea haki. Kwa mfano, nilisema hapa kwamba uchaguzi na Mhe. Waziri aliyepita na kuniahidi na kuniambia ataniarifu katika uchaguzi wake, sasa wewe sijui utaniambiaje na hapo ndipo nitakapokuwa mkali.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema fedha za Mhe. Rais Mstaafu wa Zanzibar Dkt. Amani Abeid Karume aliwaahidi kuwapa fedha zao, kwa kweli fedha hizo mpaka leo hawajapewa kulikoni? Kwa mfano, wakati mwengine wanakwenda katika Mashindano ya Kimataifa wanaambiwa nauli toa mwenyewe na posho jidhamini mwenyewe na ukirudi tu *immediately* unapewa fedha zako na mpaka leo bado hawajapewa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, Chama hichi zamani kilikuwa kizuri na tulikuwa tukiwaleta Suleimana Nyambui, Filbet Bai na wengine tukiwaleta hapa Zanzibar na wananchi wa Zanzibar wakifarajika na michezo hii, lakini leo hichi chama kimeuliwa kabisa. Kwa hivyo, kitu cha mwanzo Mhe. Mwenyekiti nataka uchaguzi ufanyike *immediately* kabisa ndipo nitakapopitisha kifungu hichi.

Kwa kweli kifungu hichi cha Sera na Utafiti ni kigumu hichi, kwa sababu *include* na hiyo ndio utafiti wenyewe ndio huu. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima na ninamjua Mhe. Waziri anatikisa kichwa kama anapungwa pepo, kwa kuwa ni mtekelezaji. *(Makofi)*

Kwa hayo, machache Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa nataka niilinde heshima yako, chama hichi kipewe haki zake. Kwa mfano, leo tumeoneshwa hapa jinsi gani mtoto alivyokuja na madeli zake, tumeonesha sifa nzuri, sasa kwa nini na hichi tusikipe uwezo wake pamoja na majukumu yake. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kwamba uchaguzi ufanyike na wakati atakapokuja Mhe. Waziri anieleze kwamba siku ya Jumatano inayokuja uchaguzi utafanyika Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia siungi mkono hoja mpaka aje kunijibu vizuri na Mhe. Waziri ni mwenzangu atanijibu vizuri. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe, naomba mambo mawili yazingatiwe. Kwanza tuzingatie muda na halafu Wajumbe wazungumze na kiti na wala wasizungumze na Waziri. Tuendelee na sasa anafuata Mhe. Nassor Salim Ali na Mhe. Ashura Sharif Ali awe tayari. *(Makofi)*

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi hii ya kuchangia Hotuba hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya, kwa kweli ni ya kupongezwa, yaani anaendelea na ile ile ya kasi zaidi, ari zaidi na nguvu zaidi ambazo tumeziona kwa muda huu mchache. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza kijana wetu Ahmed Bakari, ambaye ameweza kutuletea medali hii ya Mashindano ya *Olympic* Maalum yaliyofanyika kule Ugiriki. Kwa kweli tunampongeza sana na tunamtakia kila la kheri na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu amzidishie zaidi. *(Makofi)*

Vile vile nichukue fursa hii kuipongeza Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Baraza la Michezo na *ZFA* kwa ujumla kwa kuweza kufanya uchaguzi wenye haki na ukweli wa kuweza kumpata Rais mpya wa *ZFA* kwa kuweza kushinda kwa kishindo kwa asilimia 96.3, hivyo nawapongeza sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nianze na Sekta ya Habari. Sekta hii ni muhimu na waandishi wa habari ndio wanaotupa mambo mazuri yanayofanyika nchi mbali mbali pamoja na sehemu tofauti na hata leo naona mambo yamekuwa yananoga hapa, yaani ukiangalia katika *screen* kuna mabadiliko kwa waandishi wa habari. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti, waandishi wa habari bado hawajatendewa haki, yaani Serikali bado haiwafanyii mambo mazuri waandishi wa habari. Mhe. Mwenyekiti, nathubutu kusema hivyo, kwa sababu hivi karibuni kulikuwa na safari za nje mbali mbali kwa Mawaziri na Wenyeviti, ambao walikuwa wanafanya safari katika nchi za China kule.

Jambo la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, katika safari zile hawakuwemo waandishi wa habari na ukiangalia kwenye Sekta hii ya Habari hususan katika Idara ya Habari Maelezo ni kitengo muhimu sana. kwa kweli ni kitengo muhimu na wanafanyakazi usiku na mchana na kutupa habari mbali mbali, lakini wakati zinapotokea safari kama hizi basi waandishi wa habari wale huwa hawaangaliwi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri afanye kila mipango pamoja na njia kuhakikisha kwamba waandishi wetu hawa, basi na wao wanapata safari zile zinazoandaliwa na Serikali kwa Mawaziri au Rais ama wengineo. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niingie kwenye Sekta ya Utalii. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze Kamisheni ya Utalii, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya juzi tu katika ile ajali. Mimi kwa kushuhudia Mhe. Mwenyekiti nilifika pale Hospitali ya Mnazi Mmoja, kupitia Kamisheni ya Utalii wakiongozwa na Mkurugenzi niliwakuta pale hospitali wakiwahudumia wale majeruhi, watalii ambao waokuwepo pale na wao ni miongoni mwa waliokuwemo kwenye ile meli ambayo ilizama juzi.

Kwa kweli ni jambo la kupongezwa sana, kwa sababu hata watalii wengine ambao watapata taarifa zile basi watakuwa wanaingia imani na kuweza kuongeza nguvu za kuja watalii katika nchi yetu.

Pia niipongeze Kamisheni ya Utalii kwa kuwa karibu katika ajali ile. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, juhudi kubwa zimefanywa na Kamisheni ya Utalii, haya yote yametokana na uongozi mzuri wa Waziri wetu mpya kwa kuweza kusimama kitete katika kuongeza kasi ya kuleta maendeleo na kukuza utalii Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kufurahisha kwamba Zanzibar tumepata tunzo maalum, ambayo tunzo hii imetoka kule Urusi. Lakini haya yote ni juhudi ambazo zimefanywa na Wizara pamoja na Kamisheni ya Utalii.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri au ningetaka kujua tu kwamba Wizara yake katika kuendeleza na kupata tunzo nyengine katika nchi mbali mbali imejipanga vipi, ili kuweza kupata tunzo nyengine ambazo zitatuletea sifa nchi yetu na kuweza kuendeleza zaidi utalii wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna utalii wa wageni kutoka nje pamoja na ule wa ndani. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri anauendeleza na kufanya mikakati imara ya kuweza kuendeleza utalii wa ndani, kwa sababu nao utalii wa ndani una faida zake, kama vile kuongeza tija. Kwa mfano, wenzetu Tanzania Bara wafanya mikakati mikubwa sana ya kuendeleza utalii wa ndani.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Utalii. Mhe. Mwenyekiti, chuo hichi ni muhimu sana kwa vijana wetu, kwa sababu katika kuendelea chuo kile vijana wetu wataweza kupata ajira katika mahoteli mbali mbali na tumekuwa tukilalamika kwamba vijana wetu hawapati ajira kwenye mahoteli na wanaajiriwa vijana kutoka nchi mbali mbali za majirani zetu.

Lakini tukijipanga vizuri katika kuwasomesha vijana wetu, basi naimani kwamba vijana wetu wanao uwezo huo na kuweza kupata ajira kwa ajili ya kujiendeleza na kutatua tatizo hili la ajira katika nchi yetu.

Sasa niinge kwenye Sekta ya Utamaduni. Mhe. Mwenyekiti, sekta hii kwanza nianze na suala la Mchezo na Mpira wa Miguu. Kwa kweli Mchezo wa Mpira wa Miguu takriban miaka 7 au 8 iliyopita mchezo huu hapa Zanzibar ulikuwa umekufa kabisa. Nathubutu kusema haya kwa sababu sote ni mashuhuda, lakini kutokana na juhudi za Waziri wetu wa Habari mpya imeanza kuleta sura nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tayari dalili zimeonesha na hivi juzi tu timu zetu ambazo zimeshiriki katika mashindano na mama yangu hapa Mhe. Asha Bakari Makame

alizungumzia kuhusu Timu yetu ya *Zanzibar Heroes*, ambayo ilishiriki katika Mashindano yale ya *VIVA* World Cup na iliweza kupata nafasi ya tatu. *(Makofi)*

Vile vile tena Timu yetu ya Vijana wenye Umri wa Miaka 20 ambayo ilishiriki Mashindano kule Burundi, nayo pia iliweza kushika nafasi ya tatu. Mhe. Spika, Club yetu ya Mafunzo ambayo ilishiriki Mashindano ya *Challenge* na walitolewa nusu *finally*, tena walitolewa kiume kwa sababu ilifika wakati wa kupigwa mikwaju ya *penalty* na kuweza kushindwa kwa magoli 5 kwa 4. Kwa hivyo, ni juhudi ambazo zinaonesha kwamba kuna matumaini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ukija katika upande wa Soka la Wanawake. Kwa kweli soko hili linasikitisha sana, kwa sababu ulimwengu wa leo kokote unakokwenda Soka la Wanawake linakua, lakini ukija kwetu linadidimia.

Kwa hivyo, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja atupe majibu, kwa sababu katika kuendeleza Soka la Wanawake kuna mratibu mmoja ambaye tupo naye hapa Zanzibar na amekuwa akisafiri nchi mbali mbali, kama vile South Africa, Ethiopia, German na hivi karibuni alikuwa Cameroon.

Lakini safari hizi ambazo amesafiri mratibu huyu bado hatujaona faida zake, sasa sijui Mhe. Waziri wakati atakapokuja hapa atueleze faida na mikakati gani ambayo imefanywa katika kuendeleza Soko hili la Wanawake.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la viwanja. Katika kitabu chake Mhe. Waziri amesema kwamba anayo mikakati ya kuendeleza viwanja mbali mbali ukiwemo Uwanja wa Amani.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Uwanja wa Amani tumekuwa tukilia sana Waheshimiwa Wawakilishi, wapenzi wa mpira wa miguu Zanzibar wadau mbali mbali, kwa kweli ni aibu kwa Zanzibar kukosa uwanja wa kisasa. Kwa mfano, hivi juzi katika Mashindano ya Ujirani kulitokea aibu kubwa sana, kwa sababu mashindano yalifanyika pale lakini mwisho timu zimegomea kucheza mchezo pale, kutokana na ubovu wa uwanja na mchezo ule ikabidi ukafanyike Dar-es-Salaam.

Mhe. Mwenyekiti, tunaelekea katika miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya 1964. Sasa sijui Mhe. Waziri atakapokuja hapa atatueleza nini kuhusu mikakati kuhakikisha kwamba itakapofika mika 50 katika Sherehe zetu za Mapinduzi Matukufu ya 50, basi uwanja ule uwe tayari na kuweza kufanya sherehe zetu pale na mashindano ambayo tutakuwa tunasherehekea miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja tunamuomba atupe maelezo sahihi ya kuhakikisha kwamba uwanja ule unatengenezwa na unakuwa uwanja wa kisasa na unaweza kufanyiwa mashindano mbali mbali yakiwemo ya ndani na yale ya kimataifa.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu uwanja au Kijiji cha Michezo cha Dole. Kwa kweli tumekuwa tukipata taarifa mbali mbali kuhusu kiwanja kile na Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohmmed Shein katika hotuba zake aliahidi kwamba atahakikisha kuwa anaendeleza michezo

kwa kuweza kujenga viwanja vya kisasa pamoja na majengo yale vya kijiji cha michezo, ambacho tayari kimeshaanza kule Dole, lakini mwenendo wake ni wa kusuasua.

Kwa maana hiyo, Mhe. Waziri atakapokuja sijui atatueleza mikakati pamoja na mipango gani ya kuhakikisha kile Kijiji cha michezo kule Dole kinaendelezwa na lini hasa kijiji kile kitakuwa tayari kwa ajili ya kuendeleza vijana wetu wenyewe vipaji, kwa sababu kijiji kile kinaendeleza vipaji mbali mbali ikiwemo soka, riyadha na michezo mingine.

Aidha Mhe. Mwenyekiti, katika taarifa ya Mhe. Waziri kuhusu Baraza la Taifa la Michezo ametueleza huku, kwamba Wizara imo katika mikakati mbali mbali katika kufufua na kuendeleza michezo ambayo imekufa na nampongeza sana kwa bidii zake hizo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna Mchezo wa *Cricket*, ambao ulipendwa sana hapa Zanzibar na wananchi mbali mbali walianza kucheza mchezo huu, ingawa Mhe. Ismail Jussa Ladhu ndiye Mlezi wa Mchezo huu wa *Cricket* na wapo watu mbali mbali ambao wanaoucheza mchezo huu, lakini mchezo huu umekufa. *(Makofi)*

Jambo la kusikitisha zaidi Mhe. Mwenyekiti, Chama cha Mpira wa *Cricket* Tanzania *TCA*, kiliwahi kutoa vifaa vya michezo kwa ajili ya mchezo huu. Kwa kweli vifaa vile vimepotea na wala hakujulikana nani amepewa.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja aje na jawabu la kutueleza kwamba vile vifaa vimepotelea wapi na kuna mikakati gani ya kuhakikisha, kwa sababu gani hapa imeelezwa kwamba moja katika michezo ambayo Wizara imejipanga kuiendeleza na kuifufua ni Mchezo wa *Cricket*.

Lakini vifaa vyake ambavyo vimetolewa kwa ajili ya mchezo huu vimepotea katika mazingira ambayo hayaeleweki. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja atupe jawabu ya upotevu wa vifaa hivi vya Mchezo huu wa *Cricket*.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nije katika suala zima la Kocha yule Misri ambaye tulipata msaada kutoka Serikali ya Misri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, unazo dakika 5 za ziada.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, tunakumbuka Kocha wa mwanzo ambaye alikuja hapa Zanzibar ni Kocha Badrudine, ambapo mchango wake mkubwa tumeuona na ameweza kuibua vipaji mbali mbali kama vile wachezaji Canavaro**,** Agrey Moris**,** Solembe na wengine, ambao leo wamekuwa wachezaji wakubwa Tanzania na wanacheza timu za Taifa za Tanzania (*Taifa Stars* na *Zanzibar Heroes).*

Lakini baada ya kuondoka Kocha yule akaja Abdul-Fatah, ambaye yupo kwa muda mrefu na bado hatujaona matunda yake. Kwa mfano, tumekuwa tukimuona akishiriki katika vilabu tofauti kama vile Mafunzo, KMKM, *Zanzibar Heroes* na nyenginezo. Kwa kweli suala hili bado na ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze hasa sababu gani zilizomfanya kwamba asiingie katika kuinua vipaji vya vijana wetu kama vile miaka 16, 17 na 18 kama ambavyo alikuwa anafanya Kocha Badrudine**.**

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja atueleze ni sababu gani, ambazo zimemfanya kwamba Kocha huyu awe hashiriki sana katika kuinua vipaji vya vijana wetu na akawa anashiriki kwenye vilabu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naheshimu muda wako na mimi nitaunga mkono hoja baada ya kupata maelezo ya Mhe. Waziri. Kwa hiyo, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa anafuata Mhe. Ashura Sharif Ali na baadaye Mhe. Ismail Jussa Ladhu naye awe tayari.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Subuhanahu Wataalla aliyetujaalia uhai na uzima tukawepo hapa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Vile vile nikushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri wa uwasilishaji wake mzuri. Pia nimshukuru Mhe. Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wake kwa jinsi ya utayarishaji wa hotuba hii. *(Makofi)*

Baada ya utangulizi wangu huo Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nianze mchango wangu katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Nimeianza idara hii kwa sababu ninalo jambo ambalo linanisokota kidogo nataka kulielewa. Mhe. Mwenyekiti, hapa ninazo taarifa zinazosema kwamba kuna wafanyakazi 7 na wengi wa wafanyakazi hao ni wanawake niseme kuwa labda wamefukuzwa au wamesimamishwa kazi, lakini bila ya utaratibu maalum. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Waziri suala hili kwa upande wangu lilinishtuwa sana, kwani wafanyakazi hao waliitwa katika kikao na baada ya kikao hicho waliambiwa kwamba wasihudhurie tena kazi na wala hapakuwa na mkataba au barua iliyoonesha hilo na hivi sasa wafanyakazi hao wapo nje.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nikishangazwa nikiona kwamba Idara hii ya Utumishi na Uendeshaji, kuwa imenipa maajabu kwani utaratibu wa kazi unafahamika pamoja na usimamishaji wa kazi utaratibu upo, lakini hawa walipewa kauli ya kwamba huyo aliyewasimamisha na yeye amepewa kauli kwamba wao iwe kazi basi.

Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja hapa basi anipatie majibu ya kina, ili niweze kuelewa kwamba sasa Sekta ya Umma katika kazi inakwenda kwa mtu binafsi maamuzi yake, hivi ni vyema tuelewe haki za watu hawa na hatima yao na kama haikuwa hivyo, basi kwa sababu Sekta inayohusika ni ya Utangazaji nitalizuia fungu hilo, kwani sitajua mishahara ya hao itakwenda wapi.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye Shirika la Utangazaji Zanzibar. Kwa kuwa utangazaji na upataji habari ni jambo la msingi, wanatufanyia mambo mengi na tunapata taarifa

zao, ambazo ni nzuri na tunashukuru sana. Lakini kwa kuwa na sisi tupo katika dunia na tarehe ya mwisho ya Mfumo wetu wa *Analogy* ni tarehe 31 Disemba, 2012 na sisi tupo katika dunia.

Kwa hiyo, hapa naomba niiulize Wizara imejipanga vipi kuona na sisi katika wakati huu wa *Science and Technology* tunajiunga na Mfumo wa *Digital*, ili kwenda sambamba na ulimwengu wakati utakapofika. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba alitueleza Mhe. Waziri kuwa amerusha vipindi 18 kwa jamii, lakini je ufahamu huu wa jamii, hali ambayo utekelezaji wake bado haujapata nafasi na pia bidhaa ambazo zitatumia huu mfumo wa *Digital* ni utaratibu maalum wa urushaji au upatikanaji wa matangazo.

Lakini kwa wananchi wetu kwa sasa hivi vifaa vinatumia utaratibu maalum, kwa kweli vifaa vingi ambavyo vinaletwa hapa kwetu hivi sasa havina utaratibu huo. Sasa sijui Mhe. Waziri atakuja kuniambia nini kuhusu suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika ukurasa huu wa 35 kuhusu Tume ya Utangazaji. Kwa kweli nawapongeza sana ndugu zangu hawa kwa juhudi pamoja na kazi zao wanazozifanya na uthibitisho wa hayo ni kusikia Wizara mbali mbali kusema kwamba zimerushiwa matangazo yake, vipingi 17 nyengine 10. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba huu ni utekelezaji mzuri wa shughuli zao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, imezoeleka taasisi nyingi za serikali pale ambapo wanakwenda kupeleka matangazo yao, basi huwa wanapeleka na kuondoka na kutaka matangazo yao yatoke tu. kwa hiyo, ninaziomba taasisi zote za serikali, ili kuiwezesha tume hii kufanya shughuli zake vizuri, basi taasisi zile ziwe zinalipa kwa lengo la kuwawezesha wafanyakazi zao kwa ufanisi.

Sasa naomba niingie kwenye ukusara wa 53 kuhusu Shirika la Utalii. Mhe. Mwenyekiti, shirika hili ni chombo cha mwanzo kabisa hapa kwetu kushughulikia utaratibu mzima wa utalii. Chombo hichi kwa sasa kinaambiwa kipo katika kipindi cha mpito na kushindwa kuhimili shughuli zake. Kwa mfano, kuna tafiti zinafanywa, ili kukiona kwamba kitaweza kuendelea au laa.

Lakini ni ukweli usiofichika kwamba shirika hili lilikuwa linajitegemea na kujiweza kabisa. Kwa mfano, shirika hili lilikuwa na mali zake ambazo likitumia na kujiendesha na kwa bahati mbaya sana mali hizi zimegawanywa tena zipo na tunajua na tunafahamu hili. Mhe. Mwenyekiti, ili shirika hili liweze kujiendesha, ni vizuri basi Vitega vyake Uchumi vya Serikali virejeshwe pale, ili shughuli zake ziendelee.

Mhe. Mwenyekiti, imezoeleka mno mambo mengi ya Serikali hurithiwa kabla hata ya kufa. Kutokana na hali hiyo, naomba vile Vitega Uchumi vya serikali ambavyo vimegusa katika sekta hii virejeshwe na shirika lipo, lipewe huo ndio ukweli. Mhe. Mwenyekiti sasa niende katika ukurasa wa 41 huu unagusia sekta ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya utalii kwa sasa tunaiita ndio sekta mbadala kwa ajili ya pato la taifa. Sekta hii inahitaji tafiti za kina, inahitaji kujielewa na kufahamu Zanzibar ni Visiwa. Ardhi yake ni ndogo inahitaji utaratibu mzuri wa matumizi mazuri ya ardhi hiyo kwa manufaa ya Wazanzibari kama dhana inavyoonekana kusema ya kwamba utalii kwa wote. Hivyo basi

tumeona ardhi nyingi zinatumika katika hoteli ya mahoteli mbali mbali yakiwa sio yale mahoteli yana kiwango.

Mhe. Mwenyekiti, umefika wakati wa kujipanga tukajiamulia, tukajua tunauhitaji utalii wa aina gani hapa kwetu Zanzibar kwa maslahi ya Wazanzibari wote. Tumejipangaje kwa ajili ya utalii wa daraja la kwanza kwetu Zanzibar ambao utaleta tija na manufaa makubwa kwa Serikali na wananchi wake kuweza kuneemeka. Hili Mhe. Mwenyekiti la kufanya tafiti naunga mkono na nasema kwamba Mhe. Waziri nafasi hii uitumie na utuoneshe kwamba sasa tunataka kuelekea wapi katika utalii wetu badala ya kuwa na pupa kama tulivyoanzisha mwanzo. Tunahitaji utalii tukavamia vamia na hatimaye migogoro mingi ya ardhi imejitokeza kwa sababu kama hizi.

Mhe. Mwenyekiti, ni vizuri kuona kwamba tunazitumia kanda zetu za bahari na sehemu nyengine vizuri kwa maslahi ya Wazanzibari wote. Utalii huo uwe na neema tuone kwamba Wazanzibari wanafanya kazi nao katika mahoteli hayo bila ya ubaguzi, bila ya unyanyasaji. Lakini pia kuweza kufanya kazi na kupata manufaa ya utalii wenyewe kwa kuweza kujinufaisha kwa kuweza kuzalisha mambo ambayo yanahitajika katika utalii huo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende ukurasa wa 57 kuhusu Hoteli ya Bwawani. Hoteli ya Bwawani ni Hoteli ya Serikali, ambayo iko chini ya Wizara hii ya Habari na Utalii. Hoteli hii ni hoteli ya kihistoria maana ndiyo yetu. Jambo ambalo hapa linanishangaza ni kuona hoteli hii ya serikali vigezo vyake haviridhishi katika hali iliyo. Pamoja na mengi yaliyofanywa lakini ili iweze kuhimili na kwenda katika soko la ushindani ni lazima hoteli hii iboreshwe. Hoteli hii kuna wageni ambao waliwahi kwenda ikafika mahala hata hiyo sabuni ya kupelekwa chooni ikawa haipatikani, ni aibu.

Pia wafanyakazi wa hoteli hii nakuomba Mhe. Waziri uje unambie ni wangapi wafanyakazi wa kudumu na ni wangapi wafanyakazi wa *daily pay* tuweze kuwajua. Mpaka sasa sisi tunapiga kelele katika mahoteli ya nje kwamba watu wawe na mikataba, wawe na utaratibu, lakini na hoteli yetu ya Serikali mpaka leo inawalipa watu kwa siku, ni aibu. Ipo haja ya kusimamiwa na kuona kwamba hoteli hii inakwenda kwa utaratibu unaokubalika.

Mhe. Mwenyekiti, sasa basi niende katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii. Tuliigusa dhana ya utalii mwanzo. Dhana hii kwetu sisi Wazanzibari ikasema ni lazima iyende kwenye matayarisho, tukawa na Chuo chetu cha Maendeleo ya Utalii, chuo hichi kinazalisha vijana, kimekuwa ni chemchem ya kuona kwamba watakuwa na kiwango na uwezo wa kushindana na kuweza kupata ajira katika hoteli mbali ambazo zipo katika nchi yetu.
Mhe. Mwenyekiti, kwa uwelewa wangu kwamba chuo hichi kimejiunga *NACTE* lakini kina usajili wa muda. Hebu niambie Mhe. Waziri ni lini chuo hiki kitapata usajili wa kudumu, na kuna sababu gani za msingi ambazo zinasitisha kutokupata usajili wake wa kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende basi katika Kamisheni ya Utamaduni na Michezo. Mhe. Mwenyekiti, mila na utamaduni hii ni sifa maalum inayokuwanayo taifa mila na utamaduni huo ukawa ni kivutizi kwa wageni, watalii na pia kujitambulisha katika utaifa. Hili basi kama ndilo pamefika pahala sasa tunapoteza mila na utamaduni wetu hili lazima tulikubali.

Mhe. Mwenyekiti, ukitaka kuangalia hilo kama ni kigezo, mgeni anapotoka nje kuja Zanzibar anatamani sana kuona utamaduni wa Wazanzibari uliozoeleka tangu asili. Cha kushangaza na cha kustaajabisha hapa kwetu sasa Zanzibar huwezi kumjua mgeni wala huyo mwenyeji wenyewe. Ukenda kwenye mavazi ni mtihani, tulikuwa na mavazi yetu ya asili ukionekana na kanzu, kofia na koti unajulikana kwamba hayo ndiyo mavazi ya Kizanzibari. Wangependa wageni waone na waweze kufurahia hilo. Maana wao walipokuja hapa kwetu wamekuja kuliona hilo.
Hebu tujiulize vipi sasa tunalisimamia hilo. Wengependa wawaone wanawake wamevaa mabaibui yao yao yale ya kiasili, ndio tunajitangaza kibiashara kwa sababu huo ndio utamaduni wetu. Leo wanakuja wageni na sisi hatuna tofauti. Utalii huo utakuja wapi na utapata nguvu na sote tumekuwa sare.

Napenda kusema kwamba umefika wakati sasa wa kukumbuka mila zetu, tamaduni zetu, vyakula vyetu, pishi zetu kuwapa wageni wetu kuona kwamba sisi ni watu na ustaarabu wetu. Tunakwenda Mahotelini vyakula vya utamaduni wa Kizanzibari havipo. Hakuna hoteli ambayo anaambiwa mzungu kaja kapikiwa ugali wa muhogo. Niliwahi kumsikia Mhe. Mussa kwenye hoteli yake alitayarisha ugali wa muhogo. Ndio vyakula vyetu, aende akute viazi vikuu na visheti, ndio vyakula vyetu. Tunajitangaza kibiashara na wanaona hasa utamaduni wa Mzanzibari ni huu na hivi ndio vyakula vyao.

Hivyo basi nimuombe sana Mhe. Waziri ni lazima usimamie na uone katika sekta hiyo basi kunatayarishwa watu maalum katika kuufufua tena utamaduni wa Kizanzibari, wageni hawataki kuona hayo mambo ya kiulaya mambo hayo kwao yapo na kote duniani, haya yetu sisi ndio mageni. Historia zinatuonesha na tunajua sote na tunafahamu sote, hivyo basi nikuombe lazima usimamie kwa kina utaratibu huu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niingie ukurasa wa 68, niliguse Baraza la Kiswahili. Kiswahili cha Zanzibari sasa kinapotea, nyote ni mashahidi. Mtu unamsikia anasalimia “Mambo” je, hicho ndio Kiswahili chetu, tumepoteza mpaka lahaja za Kimakunduchi, Kitumbatu, pamoja na Kipemba. Huo ndio utamaduni na pia hiyo ndicho Kiswahili chetu. Leo imefika mahala lugha zimeingia ndani ya lugha, tunashindwa kupata ladha ya kumjua huyu ametokea wapi, huwa tunajuana wenyewe kwa maneno. Mgeni akija tu akikuuliza akikusikia tu anakujua hawa ni Wamakunduchi, anajua hasa mpaka kitongoji alichotokea, hawa ni Watumbatu, hawa ni Wapemba, zinakuja lahaja. Lakini leo wote wameziondoa, hazipo na hata mtu wa Makunduchi hasemi sasa hivi Kimakunduchi maana akisema atachekwa. Maalim Haruna yeye humsikia kidogo akifurahi.

Mhe. Naibu Spika, ni vizuri kuwafunza vijana wetu utamaduni huu na kujua hasa hichi Kiswahili chetu cha Kizanzibari. Najua Mhe. Mwenyekiti, umekaa tayari kwa ajili ya kunisimamisha lakini niseme kwamba kwa hayo niliyoyasema nitazuia kifungu kile cha Shirika la Utangazaji mpaka Mhe. Mwenyekiti atakaponiruhusu au atakaponieleza vyema ili niweze kumuelewa, nitamruhusu na palipabakia naunga mkono hoja sehemu iliyobakia asilimia 80. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema zake za uhai na uzima wa afya tukiendelea na kazi zetu hapa.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba niungane na wenzangu waliompongeza Mhe. Waziri sio tu kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake ya bajeti lakini pia kwa mabadiliko makubwa ambayo tumeyaona katika Wizara yake katika kipindi kifupi ambacho ameteuliwa kuiongoza wizara hii.

Mhe. Waziri, ndugu yangu Mhe. Saidi Ali Mbarouk ameleta matumaini mapya kwamba sasa sekta ambayo inasimamiwa na Wizara hii itapata mabadiliko makubwa sana. Naomba nimpongeze lakini nimwambie kwamba asije akageuka mgema, tukamsifu tembo akalitia maji, hasa Ramadhani hii. Kwa hivyo nimuombe kwamba ajitahidi na aendeleze kazi ambayo ameianzisha katika Wizara yake.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kama kawaida yangu kabla ya kuingia katika maudhui ya hotuba hii naomba nianze kwa kuombe maelezo katika vifungu kadhaa, vya matumizi akija Waziri anisaidie. Kwanza naomba anipe maelezo katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji katika fungu la Mishahara 211100 ambapo katika buku la awali mishahara ilikuwa miambili na hamsini milioni (250,000,000) lakini katika marekebisho imekuwa mia tatu tisini na tano milioni na laki tatu (395,300,000). Nilikuwa naomba anieleze nini kilichopelekea kufanyiwa marekebisho hayo ambayo wametuletea.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika fungu la viburudishaji ukurasa wa 5 wa marekebisho na ukurasa wa 610 katika kitabu ambapo fungu hili limeongezeka kutoka milioni tatu laki sita mwaka jana (300,600,000) mwaka jana hadi milioni 16 mwaka huu. Naomba maelezo vile vile katika fungu la Safari katika idara hiyo hiyo ya Utumishi na Uendeshaji ambapo fungu hili limeongezeka kutoka milioni sabi na tatu laki nane thamanini elfu hadi kufikia milioni 100 kwa mwaka huu wa fedha unaoombewa.

Pia nimuombe Mhe. Mwenyekiti, anipe maelezo katika fungu la thamani fungu 220600 katika fungu dogo la mazulia, mapazia na makapet ambapo mwaka huu imeombewa shilingi 20 milioni. Nilikuwa naomba maelezo ya fungu hili. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti naomba maelezo katika fungu la Matengenezo ya Ofisi fungu 220700 ambapo mwaka huu limeombewa milioni 200 nilikuwa naomba kusaidiwa ni matengenezo gani ambayo yanakusudiwa kufanywa yatakayogharimu shilingi milioni 200. Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate maelezo katika fungu la Mafunzo, fungu 221100 ambapo mwaka jana ilikuwa milioni 28 mwaka huu limeombewa 60 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji naomba vile vile Mhe. Waziri anisaidie maelezo kuhusiana na Idara ya Habari Maelezo. Hapa fungu la mafuta na vilainisho limeombewa milioni 14 nilikuwa naomba anisaidie kwamba Idara ya Habari Maelezo ina gari ngapi ambazo zinahitaji kiwango hichi cha mafuta na *diesel* zilizotajwa pale.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba maelezo katika fungu la posho maalum katika Idara mbili, Idara ya Makumbusho ambako kuna shilingi ishirini milioni, laki sita elfu kumi na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo posho maalum ni shilingi hamsini na moja milioni, laki tano na elfu

kumi. Nauliza hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu fungu hili katika Idara tofauti limekuwa likibadilika katika Wizara tofauti. Kwa hivyo nilikuwa naomba nisaidiwe maelezo yale. Kwa sababu kama ni posho maalum analipwa Mkurugenzi nilikuwa nikitegemea wakurugenzi wote Serikali nzima wangekuwa wanafanana.

Vile vile katika Kamisheni ya Utamaduni na Michezo katika fungu la matengenezo ya Afisi kuna matengenezo madogo ambayo ni shilingi 23 milioni. Nilikuwa naomba pia hilo Mhe. Waziri anisaidie maelezo. La mwisho katika fungu la Wizara katika hiyo hiyo Idara au Kamisheni ya Utamaduni na Michezo kuna fungu la Mikutano ya Ushirikiano wa Kimataifa ukurasa 635 ya buku hili, ambalo mwaka jana liliombewa shilingi mia moja milioni laki nne, mwaka huu limeombewa mia moja kumi na tano milioni. Nilikuwa nataka kujua Mikutano ya Ushirikiano wa Kimataifa inayogharimu fedha zote hizi, ni mikutano gani.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikiacha fungu la Wizara naomba nije katika fungu la Kamisheni ya Utalii fungu Nam. 31. Naomba akija Waziri anisaidie maelezo katika utawala Unguja fungu la Malipo Baada ya Saa za Kazi ambapo mwaka huu limeombewa 40 milioni kutoka mwaka jana milioni kumi na laki nane. Vile vile Posho la Vikao na Kamati ambapo mwaka huu limeombewa shilingi tisini na mbili milioni, laki moja ishirini na saba elfu ukilinganisha na 30 milioni za mwaka jana. Fungu jengine nililoomba maelezo katika Kamisheni ya Utalii ni fungu la Viburudishaji ambapo mwaka jana ilikuwa milioni 3 mwaka huu ni shilingi ishirini milioni laki tano na elfu kumi na mbili. Vile vile fungu la Safari Mhe. Mwenyeki, kwa ujumla wake ambapo mwaka jana lilikuwa mia moja sabini na tisa milioni laki saba, thalathini na mbili elfu, mwaka huu limeombewa mia tatu na tisa milioni, laki moja arubaini na mbili elfu.

Nilikuwa naomba nipewe maelezo kama ambavyo naomba maelezo katika fungu la ununuzi wa mashine na zana katika suala zima la ununuzi wa gari. Naona Kamisheni mwaka 2009/2010 ilinunuliwa gari ikapewa milioni 33, mwaka jana ikaomba milioni 40 kununua gari, mwaka huu tena imeombe milioni 45 kununua gari. Nilikuwa naomba kujua wanahitaji gari ngapi ili kuweza kufanya shughuli zao. Kwa nini fungu hili limekuwa likiombewa fedha kila mwaka.

Mwisho kabisa katika mafungu Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate maelezo katika fungu la ruzuku, fungu 263100 la Kamisheni ya Utalii kuna fungu dogo la Uimarishaji wa Utalii na Masoko ambapo mwaka jana liliombewa shilingi sabini na nane milioni, laki mbili hamsini elfu. Mwaka huu limeombewa shilingi sabini na tisa milioni, laki tatu sitini na moja elfu na huko nyuma kumekuwa na thamanini na mbili milioni, thamanini na tano milioni, nilikuwa naomba maelezo fungu hili linahusika na nini. Kama ni fungu la Safari tayari linafedha za kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo Mhe. Waziri akija anisaidie ili niweze kuridhika kumpitishia mafungu haya. Kinyume chake ikiwa maelezo hayatoniridhisha nahofia nisije nikamzuilia mafungu rafi yangu Mhe. Said Ali Mbarouk.
Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika maudhui ya hotuba. Maeneo yapo mengi Mhe. Mwenyekiti lakini kwa sababu ya uchache wa muda nitaomba niende kadiri nitakavyoweza kuyapata katika muda huu uliobakia.

Mhe. Mwenyekiti naomba nianze na mimi katika sekta ya habari. Kwanza nataka nipongeze katika muda mfupi huu nimeona mabadiliko katika vyombo vyetu hivi, hata katika kiwango cha

picha zinazoonekana katika televishen ya ZBC, lakini hata matangazo ya redio, kwa hivyo hilo nataka nimpongeze. Vile naipongeza *quality* inavyoongezeka ya gazeti la Zanzibar Leo. Kuna mafanikio tunayaona, tunampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake, tunaomba waendeleze tuone kweli vyombo vyetu vinazidi kuongezeka kiwango ili viweze kuingia ushindani na vyombo vyengine vya katika eneo hili la Afrika Mashariki nap engine hata katika ulimwengu Mhe. Mwenyekiti.

Pamoja na pongezi hizo yako maeneo ambayo bado yapo malalamiko. Nashukuru yale mambo tuliyoyazungumza mwaka jana Waziri wa Habari ameyashughulikia. Wafanyakazi walikuwa wanalalamikia stahiki zao mbali mbali, posho zao, wengi amewashughulikia. Lakini kuna moja Mhe. Waziri aendelee kulishughulikia wale ambao wanadai madeni yao kutokana na safari ya Uholanzi. Hili bado tunaendelea kulilalamikia nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija atwambie kwa nini wanaendelea kusumbuliwa wakati walikopwa kwa kuambiwa iwakopeshe Wizara wakati huo na mpaka leo fungu hili bado halijalipwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile naomba maelezo kwa Mhe. Waziri wa Habari, katwambia anakusudia kuligeuza jengo la zamani la Studio za Rahaleo kuwa kituo kipya cha sanaa hizi. Lakini waliokuwepo pale wamehamishiwa katika Studio iliyokuwepo katika jengo la Radio hivi sasa. Sasa kuna wataalamu wanatwambia kwamba Studio ile ni katika Studio ambazo zina ubora nzuri sana ilikuwa timetupwa tu. Sasa kwa kugeuzwa kuwa ni Afisi ya muda je, Waziri haoni kwamba anaweza akapoteza fedha nyingi kutokana mitambo iliyokuwepo pale na mashine zilizokuwepo pale kwa sababu tu kaamua kuigeuza studio ile kuwa ni Ofisi. Nilikuwa naomba hilo anipe maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile naomba anisaidie maelezo bado tunaripotiwa kwamba pamoja na ufanisi unaoonekana katika Shirika la *ZBC*. Lakini ufanisi ungekuwa mkubwa zaidi kama kungekuwa kuna uongozi unaoelewana. Tumepewa malalamiko bado sana kwamba Mkurugenzi wake Mkuu na Wakurugenzi wake hawa wawili bado kila mmoja anang'ang'ania madaraka matokeo yake wafanyakazi wanaumia na ufanisi unakosekana. Kila mmoja anatafuta vipi atapata tija binafsi badala ya kuwa na tija ya utendaji katika Shirika hili. Naomba hilo akija anisaidie kuna nini katika ZBC hata ikawa mgogoro wa uongozi haumaliziki baina ya Mkurugenzi Mkuu na Wakurugenzi wake ambao amewaweka.

Nimpongeze Mhe. Waziri wa Habari kwa hatua ya kutuahidi kwamba amekusudia kubadilisha *record* ya vipindi vya zamani ili kuviingiza katika *CD*, naamini kakusudia na *DVD* vile vile. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Waziri anambie je, na ile hazina ambayo tulikuwa nayo ya vipindi vingi vya tangu asili wanakusudia pia kujumuisha katika hifadhi hii mpya ili visipotee kwa sababu vingi ndiyo vina historia ya Zanzibar tangu wakati ule TVZ ilivyoanzishwa mwaka 1974.

Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi na kusikia kwamba kuna mafunzo hapa yanatolewa na *Dutch Welle* kwa mashirika hayo. Pia nilikuwa namuomba Waziri afanye mawasiliano na *BBC* pamoja na hali ngumu ya uchumi waliyonayo Waingereza. Mimi wakati fulani tulipokuwa katika Tume ya Muafaka tuliwahi kuwasiliana na *BBC* na mimi nilifanya safari wakati huo na nilikuwa tayari kusaidia vyombo vyetu ili kuviongezea nguvu na hata kuwasaidia kuanzisha vipindi cha kisasa vitakavyokuza mijadala na demokrasia katika nchi yetu. Nimuombe Waziri na hilo pia akipata

nafasi awasiliane hata Balozi wa Uingereza hapo Dar-es-Salaam au tuone tunaweza tukasaidiwa vipi.

Niungane mkono na hotuba ya Kamati waliokuwa wametaka kuwasaidia watangazaji wetu hasa wale wanaokuja katika televishen, kwa sababu wanatakiwa wakitoka pale wawe *presentable* ile taswira yao ipendeze. Wengi wanakuja pale mavazi yao hayaridhishi mara nyengine. Si kwa sababu hawapendi kupendeza lakini kwa sababu uwezo ni mdogo nadhani kuna haja ya kuyaangalia hayo Mheshimiwa.

Vile vile katika eneo hili naomba Waziri akija anisaidie hapa kataja hii *Star Times* ambao wamepewa kazi ya kusaidia katika kuondoka katika mfumo wa *analogy* kuja katika mfumo wa *digital*, nilikuwa naomba maelezo kwa nini imechaguliwa Kampuni hii. Kwa sababu hili mara nyingi tumekuwa tukivamia Makampuni yanayotoka China lakini nchi yetu tayari hivi sasa imeshuhudia miradi mingi ambayo imefadhiliwa tena kwa mkopo wa masharti nafuu lakini baadaye unakuja kuta kiwango cha gharama kinaongezwa sana ile nafuu uliyoipata katika riba inakuwa haina maana yoyote. Nilikuwa naomba anieleze na ile *Star Times* kwa nini wamepewa wao.

Mhe. Mwenyekiti, nipongeze hatua ya kutaka kufanyia marekebisho Sheria Nam. 5, lakini mimi ningachosema Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri badala ya kuangalia kufanya marekebisho Sheria Nam. 5 ambayo Tume ya Nyalali iliita katika sheria kandamizi 40 zile, hebu waliangalie hili alilolisema Mwenyekiti wa Kamati kwamba kuna mapendekezo ya Wahusika wa Sekta ya Habari kwamba tuanzishe Sheria ya Uhuruu wa Habari Zanzibar, kwa nini Waziri asiliangalie hilo badala ya kuendeleza sheria ambayo imetajwa kwamba ni sheria kandamizaji ambayo inaendelea kuharibu sifa yetu nzuri katika suala hili zima la sekta ya habari hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nije katika Shirika la Magazeti. Shirika la Magazeti kama nilivyosema nalipongeza Zanzibar leo linaongezeka hadhi. Lakini katika hotuba yake katwambia kwamba wameongeza soko, sasa linafika katika maeneo mengi. Lakini nikitizama ruzuku inayoombewa bado iko katika kiwango kile kile. Sasa je, kuongezeka huku kwa soko hakujaongeza mapato kutokana na mauzaji ya magazeti na matangazo ambayo tunayapata.

Pia katika hilo nisaidie mwaka jana Mhe. Salmin Awadhi alisimama kutaka Serikali na taasisi mbali mbali nyengine za umma zilipe madeni ya matangazo ambayo yanatolewa katika Zanzibar leo. Je, madeni yale yamelipwa Mhe. Mwenyekiti, isiwe tunaendelea kuidhinishia ruzuku wakati kumbe inaweza kabisa kujiendesha lenyewe gazeti hili la Zanzibar leo.

Mhe. Mwenyekiti, katika Tume ya Utangazaji hapa nilikuwa ninamoja, kuna huu utaratibu wa kutoka katika *analogy* kwenda kwenye *digital*, tumesikia kwamba itabidi watu wote wanunue hivi kwa Kiswahili vinaitwa ving'amuzi, sijui kiswahi cha wapi hichi, niseme neno linalofahamika zaidi *decoders*. Sijui Wizara imejipanga vipi kutafuta *decoders* ambazo zitakuwa na gharama nafuu ili wananchi wetu waweze kuzimudu. Jana nilisikia Bungeni kulikuwa kuna mazungumzo pale kwamba kumbe unaweza ukawa na kifaa fulani ambacho kinaweza kikafanya nchi nzima ikaweza kufaidika na mabadiliko yale bila ya mwananchi mmoja kwenda kununua. Sina hakika mimi si mtaalamu wa mambo haya, lakini hebu Waziri akija anisaidie kwamba hilo linawezekana.

Mwisho kabisa katika Sekta ya Habari Mhe. Mwenyekiti, naomba Waziri akija anisaidie maelezo. Aiangalie sana ZBC katika upande wa Radio kuna wafanyakazi hawa 10 ambao wamekuwepo pale kwa muda mrefu sana wakitumika, hawakuajiriwa lakini waliahidiwa kwamba wakati ukifika wa kuajiriwa wataajiriwa. Lakini nasikitika zilipokuja nafasi za ajira hao wameachwa na badala yake wakubwa wa ZBC katika sehemu wa Radio wana watu wao tuo waliotumika kuwaajiri pale. Hawa ili kuwahalalalisha kwamba wamekosa kwa sababu ya kukosa sifa wamefanyiwa *interview* lakini baadaye wameachwa solemba. Hawa hata posho hawapewi, wameambiwa watalipwa kulingana na *story* wanayopeleka na *story* moja ni Shs. 3,500/- kama itachukuliwa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, haya hayaleti sura nzuri naomba Waziri akija anisaidie maelezo kwa nini tupitishe bajeti yao shirika hili kwa upande wa Radio ikiwa wanaonekana kwamba wana mambo ambayo hawaridhishi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nende kwenye sekta ya utalii. Katika sekta ya utalii kwanza mimi niseme nafurahi kwamba kadiri siku inavyokwenda tunaongeza idadi ya watalii ambao wanatembelea Zanzibar. Mimi bado naamini tunaweza kuongeza zaidi lakini pia kwa kuzingatia quality badala ya *quantitiy*. Sychells wameweka utaratibu kwamba wao wameweka kiwango cha watalii lakio mbili tu kwa mwaka. Lakini wame – *target* watalii wa daraja la juu ambao wanaingiza mapato makubwa katika nchi. Sasa sisi tumekuwa ni *mass of tourism* kila aina ya mtalii anaingia tu, lakini pengine kiwango cha fedha anachotumia ndani ya nchi ni kidogo mno kuweza kuleta tija katika nchi.

Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akija walitizame sana suala hili. Tuangalie nchi za wenzetu jirahi hapa Sychells, Mauritius, Malaysia, mashariki ya mbali kule, wanafanya nini ili kuweza kupata watalii ambao wapo daraja la juu. Katika hapa Mhe. Mwenyekiti nizungumzie suala la mapato yanayotokana na visa, bado Zanzibar inakosa mapato mengi kutokana na visa ambazo zinaombwa katika Afisi za Kibalosi za Nji za Nje, lakini sisi hatupati kitu. Tumelipigia kelele muda mrefu sana kwamba fedha hizi haziletwi Zanzibar, wakati watalii wanakuja Zanzibar. Waziri naomba akija anisaidie hili wamelifanyia kazi kiasi gani kuona wanaliondoa.

Lakini hata pale wanapokuja hapa wanaopata *visa* uwanja wa ndege, mara nyingi tumepiga kelele kuna utaratibu wa mtu kugongewa muhuri pale. Na kuna fununu Mhe. Mwenyekiti kwamba Wakuu wa Uhamiaji Zanzibar wana michezo yao wanacheza pale wao wananufaika kupitia mihuri ile ndio maana hawataki kuwa na *visa* ambazo zinafahamika ambazo unaweza ukazifatilia na kujua *visa* ngapi zimetoka na mapato kiasi gani yalipaswa yaingie katika nchi.

Mhe. Mwenyekiti pia naomba nimuhimize Waziri katika sheria tuliyoifanyia marekebisho hapa sheria ya Kamisheni ya Utalii tulipiga kelele sana kuhusu suala la ajira na Wazanzibari kunufaika na ajira ya sekta ya utalii. Sasa sisi tunataka kipaumbele kipelekwe kwa Wazanzibari wakati ule tulishindwa kutokana na wingi wa kura na tumeheshimu demokrasia, lakini tukaambiwa suala hilo litaingizwa katika kanuni. Sasa nimuombe Waziri katika kanuni wamezingatia kiasi gani kuwapa kipaumbele Wazanzibari.

Lakini hapo hapo Mhe. Mwenyekiti niseme kwamba kuna hili suala zima la unyanyasaji wanaofanya kazi katika sekta ya utalii. Yamezungumzwa sana tangu juzi tulipokuwa tukijadili hapa bajeti ya Wizara ya Kazi na leo naomba nimwambie tena aiangalie sana hoteli ya *Residence*. Tulimwambia hapa karibuni katika kuchangia mijadala ya ripoti za kamati kulikuwa na mfanyakazi mwanamke ambaye alidhalilishwa kwa kuvuliwa nguo zote, tulisema hapa Mheshimiwa akadhalilishwa sana. Lakini sasa lile sijui kama limechukuliwa hatua leo ninapewa kesi nyengine Mhe. Mwenyekiti kuna mfanyakazi anaitwa Suleiman Makame ambaye yuko sehemu ya *food and beverages*.

Huyu tarehe 11/7/2012 alipigwa na bosi wa sehemu *pastry* ambaye ni raia wa Mauritius anaitwa *Vadvela Ramswami.* Sasa mimi siamini hata kama umepewa agizo ikawa hujalitekeleza kama adhabu yake mtu anaweza kuchukua sheria mkononi akampiga mfanyakazi. Na huyu amechukua hatua mpaka amekwenda Polisi Makunduchi kupiga ripoti lakini hakuna hatua yoyote, na hii ndio dhana inayojengeka sasa kwamba wawekezaji wanaokuja na wafanyakazi wao wa nje hawa hawaguswi wako juu ya sheria. Kwa hivyo nilikuwa nataka maelezo katika suala hili Mhe. Mwenyekiti anaziangaliaje hoteli kama hizi kubwa lakini zinanyanyasa vijana wetu wa Kizanzibari si haki kabisa mtu katika nchi yake kuwa ananyanyaswa na mgeni. Mimi siamini kama nikenda Mauritius mimi nitapewa kipaumbele kuliko raia wa Mauritius aliyepo pale Mhe. Mwenyekiti, hili hatuwezi tukalikubali hata siku moja.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo naomba nigusie kidogo suala la hoteli ya Bwawani. Kama nilivyogusia katika suala la wafanyakazi walioko katika radio Zanzibar, lakini pia katika hoteli ya Bwawani kuna wafanyakazi ambao wamefanyakazi pale kwa muda wa miaka 14 tangu 1998, lakini hadi sasa wamekuwa wakipewa mikataba miezi sita sita mpaka leo hawajaajiriwa na karibuni wameambiwa hawajaajiriwa kwa sababu kitengo cha GSO kimesema wao hawana sifa, lakini wameshatumikia miaka 14. Hili ningeliomba Wizara lakini pia Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Utumishi wa Umma walitizame. Hatuwezi tukawatuma watu miaka 14 halafu leo unakuja kuwaambia hawawezi kuajiriwa Mhe. Mwenyekiti. Hawa naomba nipewe maelezo kwa nini wasiajiriwe kama ambavyo wengine wamepewa ajira.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilizungumza suala la Mji Mkongwe naomba nirudie tena katika suala la utalii, Mji Mkongwe ulipaswa uwe ni kitovu cha kuvutia utalii daraja ya juu hasa wanaopenda kufuatilia mambo ya historia. Lakini leo mji mkongwe umekuwa mji wa vinyago na tingatinga, naomba kumuomba tena Waziri akae na Kamisheni ya Utalii watazame hili linatuletea tija gani sisi? Badala yaku-*promote handcraft* za Zanzibar tuna-*promote handcraft* kutoka nje ya Zanzibar matokeo yake mapato yale na faida ile ya utalii inakwenda kwa wasiokuwa Wazanzibari, Wazanzibari sanaa zao zinakufa.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Utalii na mimi naomba maelezo kwamba kwa nini tuendelee kuliendeleza ikiwa kazi zake zote tumeshaziua kwa kuondosha vitega uchumi vyote ambavyo vilikuwepo pale.

Sasa haraka haraka Mhe. Mwenyekiti naomba nimalizie katika sekta ya utamaduni na michezo. Mhe. Mwenyekiti, katika sekta ya utamaduni na michezo, kwanza nitoe kilio cha wananchi wa mjimkongwe. Mhe. Mwenyekiti tumechoka tumechoka wakaazi wa Shangani na maeneo ya karibu pale Forodhani, kutokana na kelele zisokwisha kutokana na Ngombe Kongwe kugeuzwa

ndio pahala pa kufanyia shughuli zote za muziki katika nchi. Duniani pahala pa kufanyia muziki huwa ni *sound proof* unakuwako ndani. Lakini haiwezekani leo jengo limezungukwa na makaazi ya watu na ikawa kila siku ya Mungu kazi yao hawalali mpaka asubuhi kwa sababu ya kelele za muziki.

Mwaka jana nilisema Wizara itafute utaratibu ijenge ukumbi maalum kwa mambo kama yale. Lakini haiwezekani Forodhani, Ngome Kongwe ikawa ndio pahala pale. Leo pale ninaambiwa sehemu ya kuongozea meli pale wanapata tabu katika kuongoza meli kwa sababu sauti zinaingiliana pale hasa meli zinazoingia usiku, mradi imekuwa tafrani katika eneo lile Mhe. Mwenyekiti, hii mimi nasema kama mwakilishi wao nitaizuia bajeti kama Waziri hajanambia hasa ahadi lini shughuli hizo zitahamishwa katika Ng'ome kongwe nasema ni pahala pa historia mwaka mara moja kukiwa na tukio la ufunguzi pale linamalizika saa nne usiku si tatizo.

Lakini leo imekuwa kila *week end* kuanzia Ijumaa mpaka Jumapili, siku nyengine mpaka siku za kazi mpaka saa nane, tisa za usiku kunapigwa muziki hili Mheshimiwa sitaliruhusu kama mwakilishi wao. Mwaka jana nilisema sijaona hatua, mwaka huu nasema kama sijapewa ahadi hapa lini itaondoshwa, bajeti hii nitaizuia Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa ufupi suala la matengenezo katika sekta ya utamaduni suala la hii Idara ya Makumbusho na mambo ya kale katika majumba ya kihistoria haya, bado tunakuja tunasema hapa tunatoa ripoti tunazopewa na watendaji kwamba inatengenezwa nimuombe Waziri atembelee *Beit el Ajaib*, atembelee jumba la makumbusho la Kasri, ninafurahi lile la mnazi mmoja pale makumbusho ya zamani limetengenezwa, lakini haya bado hali yake ni mbaya sana. Mwaka jana kulikuwa kuna bajeti katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika fungu la MACEMP lakini ukitizama kiasi kilichoombwa na mategenezo yaliyofanyika hayaridhishi kabisa. Mhe. Mwenyekiti naomba hilo alitazame sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na mchango huo mengine nitawaachia wenzangu, naomba sana Mhe. Waziri akija anipe maelezo ili niweze kumpitishia bajeti yake. Ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na uzima ili niweze kutoa mchango wangu mfupi kwenye Wizara hii Mhe. Waziri Mhe. Said Ali Mbarouk. Mhe. Mwenyekiti nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuteuliwa kukamata nafasi hii ndani ya Wizara hii nyeti.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwenye hili ambalo Mhe. Jussa amezungumzia sekta ya utalii kwenye unyanyasaji wa wazalendo. Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia na tumesikia kwenye vyombo vya habari kwamba wazalendo wa nchi hii licha ya kukaribisha utalii lakini wamekuwa hawana raha wala hawana faida wanayoipata. Tumesikia jinsi gani vijana wetu wanavyovuliwa nguo na leo Mhe. Jussa anatwambia jinsi gani vijana wetu wanavyopigwa kwa sababu ya jeuri ya wawekezaji.

Lakini Mhe. Mwenyekiti mimi niseme tu kwamba kamati yako ya PAC iliwahi kufanya ziara katika hoteli moja inaitwa Konokono, kuna mbwa kule wanaitwa fisi mtalii kwa sababu ya jeuri alithubutu kumuamrisha mbwa wake akenda ndani ya miguu ya wawakilishi wako. Kamati yetu iliongozwa na Mhe. Omar Ali Shehe, mimi nilikuwepo kama mjumbe, mbwa aliidhinishwa kuja

ndani ya kundi la waheshimiwa kwa jeuri ambayo Serikali yetu imewapa wawekezaji wetu. Sasa Mhe. Waziri kama utalii kwa wote ni kufukuzwa na mbwa kwa jeuri basi utatusaidia. Lakini kama utalii kwa wote maana yake ni kuleta maendeleo basi wawekezaji hawa hawana maana. Kwa hivyo nataka unambie huu utalii kwa wote ni hii sehemu ya utalii kuamrisha mbwa wao kwenda miguuni kwa watu ndio utalii kwa wote? Au faida gani ambao Wazanzibari wameipata.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine niungane na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, nimuombe Mhe. Waziri kwamba akubaliane na wataalam wa Baraza la Habari juu ya kuanzisha sheria mpya na ya kisasa juu ya kutoa uhuru wa vyombo vya habari, na uhuru wa kupata habari Wazanzibari na Watanzania kwa jumla. Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi tu kwenda na sheria ambazo zinakandamiza sheria ambazo zimepitwa na wakati lazima tujipange na tuanzishe sheria mpya ambazo zitatoa haki kwa vyombo vya habari.

Mhe.Mwenyekiti, nikitoka hapo sasa niende kwenye Idara ya Utumishi na Uendeshaji na niende kwenye suala zima la maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Mwenyekiti nimpongeze Mhe. Waziri kwamba sasa lile posho la wafanyakazi wetu wa Radio na Televisheni wanalipata kwa wakati, ingawa kwa maoni yangu Mhe. Mwenyekiti, posho hili bado halimsaidii mfanyakazi ni posho dogo ambalo lazima Wizara waliangalie. Posho ambalo leo wanawapa wafanyakazi wetu kwa siku ni posho ambalo halendi na wakati hasa ukilinganisha kwamba wahudumu wengine wa Baraza la Wawakilishi wanapata posho zaidi ya hili. Kuna walinzi kuna madaktari, wanapata posho tofauti na wenzetu hawa wa vyombo vya habari posho ambalo wanapewa. Sasa kama ni Serikali kujenga hoja kwamba wafanyakazi wote wanaohudumia Baraza wapewe maposho ambayo yanalingana isiwe kuna mmoja anapewa kubwa zaidi na mmoja anakandamizwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna deni ambalo tumezungumza zaidi miaka mitatu mfululizo, kodi ya Wizara kwamba inawataka wafanyakazi wetu wale waliokwenda Uholanzi wapeleke vielelezo, bahati mbaya vielelezo hawana wamevitupa miaka mitano. Sasa ikiwa Idara nzima haina kielelezo mtu mmoja mmoja, kwa hivyo kosa la hili limeanza kwenye Idara, haiwajui ni nani kapelekwa Uholanzi ndio maana wamekosa vielelezo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti mimi ninawashawishi wenzangu kwamba leo tuzuie fungu hili la Idara ya Utumishi na Uendeshaji ili Mhe. Waziri awapatie maposho yao wale vijana wetu waliokwenda nje kwa ajili ya kufanyia kazi taifa hili, hoja kwamba hawana vielelezo si hoja ya msingi, kama wao hawana Idara yako mtupe. Na kama wewe Idara huna maana yake wewe ndio mzembe, kwa nini uliwapeleka watu nje leo huwajui. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nimuombe sana kwamba hoja ya kuwa vielelezo hawana si hoja ya msingi wamekosa wao maana yake wewe kwenye Idara yako unavyo tuletee wale watu walikwenda na paspoti, paspoti zipo, wale watu Wizara kama Idara inawajua kwa barua leo hoja ya kusema hawana vielelezo si hoja ya msingi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri awpatie maposho vijana wetu hawa ili tuwajenge imani, vijana hawa Mhe. Mwenyekiti wanafanya kazi kwenye taifa hili si busara kabisa kuidhinisha mafungu na maposho huku wenzetu wakalalamika. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mimi nimuombe ili nisizuie fungu hili nikuombe sana kwa busara zako, kwa huruma zako vijana wetu uwalipe posho lao. Hoja kwamba vielelezo hawana,

vielelezo umekosa wewe kwenye Idara aje akipate mtu mmoja. Idara yako ambayo ina mafaili kama Idara haina vielelezo, aje aipate mfanyakazi mmoja.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nimuombe sana hili leo tulimalize kwa amani bila ya kugombana. Haiwezekani Mhe. Mwenyekiti miaka 6 mtu hujampa haki yake. Watu wamekopa, watu wanabughudhiwa, watu wanadaiwa. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri hili tulimalize kwa kuwapa posho lao na wala hoja kwamba wakupe ushahidi, ushahidi mnawajua nyinyi ndio mliowapeleka na vyengine mtwambie labda mmewapeleka watu ambao sio.

Mhe. Mwenyekiti hoja nyengine ni Idara ya Mipango na Sera, tumeambiwa hapa kwamba walipitisha zabuni 12 ya miradi mbali mbali. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mradi mmoja ambao umepita kwenye zabuni ni uhamishaji wa mnara wa radio Chumbuni kwenda Bungi. Mhe. Waziri naomba utueleze mradi huu ulitengewa fedha mwaka jana, hadi hapa ninazungumza taarifa ambazo tunazo mradi huu haujakamilika, tatizo nini? Na taarifa ambazo tunazo mkandarasi hajakamilishiwa fedha zake, kwa hivyo mtwambie Mhe. Waziri kwa nini fedha zilitengwa na Baraza leo fedha hizi hazijakamilishwa na mradi ule umekwama, utwambie zilipotea wapi zile fedha.

Mhe. Mwenyekiti jambo jengine ambalo hapa niseme mlipojenga mnara huu Bungi kuna vipando vya wananchi muliviathiri, lakini makisio ya mwanzo ambayo yalikisiwa ni milioni sabiini na tano. Ninashukuru sana Mhe. Rais kwa kuona kwamba fedha nyingi taarifa ambazo zipo kwamba Mhe. Rais amesema fedha ni nyingi na wataalamu wakaambiwa rudini tena watu wa kilimo. Hatua ya pili wakapewa milioni 15. Mhe. Mwenyekiti, kumbe watendaji wetu wa Wizara hii husika na vipando hapa ndipo walipotuibia. Kwa nini makisio ya mwanzo wakatwambia sabiini na tano lakini makisio ya pili ni milioni 15. Watu wamelipwa na wameridhika, mimi Mhe. Mwenyekiti ninachukua nafasi hii sana nimpongeze Mhe. Rais kwa kuliona hili kwamba kumbe watendaji wetu wanakisia fedha nyingi kinyume na matarajio ya hali halisi. Na kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti nimuombe mimi Mhe. Balozi Makamo wa Pili wa Rais msimamizi wa Serikali awaonye watu hawa kwamba wasikisie makisio kwa maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka nizungumze kwa upana ni suala zima la Shirika la Utangazaji ZBC. Mhe. Mwenyekiti kuanzia siku ile ya maafa taarifa ambazo ninazo Mhe. Waziri aliagiza kwamba televisheni yetu ioneshe masaa 24 ni jambo la faraja ni jambo zuri, lakini ningetegemea kwamba uamuzi ule wa Mhe. Waziri uendelezwe. Leo nimefanya utafiti tangu Mhe. Mwenyekiti anazungumza televisheni haioni. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Asha Bakari anazungumza Wazanzibari hawamuoni kwa nini hawamuoni kwa sababu umeme umekatika. Lakini Masingini kuna genereta ambayo ni ya akiba kwa nini haikuwepo.

Mhe. Mwenyekiti ushahidi ambao nimeupata genereta ile imekosa betri ya laki moja na ishirini. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi ninashawishika kwamba kwa nini tuipe fedha milioni mia saba Idara hii lakini hamuwezi kusimamia betri ya laki moja na ishirini. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninawashawishi wenzangu kwamba tusiwape fedha. Ikiwa mtu hawezi kusimamia, hawezi kukopa betri laki na ishirini leo tumpe milioni 700 za Idara hawezi na hii ni kwa nini ni kwa sababu hiyo Mhe. Jussa aliyozungumza kwamba watu wanavutiana ngozi kila mtu yeye mkubwa, jarida lipo, mafuta yapo lakini betri ya laki na ishirini inashindikana. Leo Wazanzibari

hawana televisheni kwa sababu ya betri. Mhe. Waziri kwa nini tuwape fedha? Kwa nini tuwape fedha watu wazembe? Kwa nini tutoe fedha wale wote ni Wizara hao.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti mimi niwaombe wawakilishi wenzangu kwa dhati kabisa fedha tusiwape. Na badala yake mimi Mhe. Mwenyekiti nitatoa betri moja ya laki na ishirini ili tuwasaidie Wazanzibari waone ni aibu kwamba betri ya laki moja na ishirini imeshindikana, lakini mtu anakuja hapa tumpe mamilioni ya fedha. Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa nia safi kabisa Mhe. Waziri tuache uzembe huu hatuwezi maagizo ya Serikali kuyadharau kwa uzembe wa mtu na haya yamekuja kwa sababu watu wanagombania cheo. Mkubwa jamani athaminiwe mkubwa ni mkubwa. Na wewe mkubwa uwe na nidhamu kwa wadogo, hatimae mnatuathiri.

Sasa mimi Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wewe Idara yako imeshindwa kusimamia betri, leo nikuamini vipi nikupe mamilioni ya fedha, sikuamini. Kwa sababu kumbe hizi fedha haisimamii ipasavyo. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nikuombe baada ya kikao njoo uchukue laki na ishirini ununue betri ili Wazanzibari waone huduma hii ya Televisheni.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka niseme kwenye Idara hii wafanyakazi wetu hawana usafiri. Hivi karibuni Mhe. Waziri alitwambia gari lipo lakini lime-*overheat*. Lakini utafiti nilioufanya Mhe. Mwenyekiti, gari hili liko nyuma ya Idara wala maringi halina. Kwa nini mtudanganye kiasi hiki, bado kwamba gari lipo maringi halina huwezi kusimamia Idara yako kwa nini fedha upewe na huwezi kusimamia. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, bado ninajenga hoja kwamba hatuwezi kuwatoa wafanyakazi wetu usiku masaa 24 tukawasambaza Masingini Bungi na sehemu nyengine wakiwa na usafiri wa kudumu, kwa sababu gani kwa uzembe wa watu. Gari lipo ndani ya Idara, halina matairi, sasa Mhe. Mwenyekiti, ikiwa matairi yameshindwa kukopwa kwa nini upewe fedha?

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani wawakilishi tuwe makini na Idara hii tusiwape fedha kwa sababu hawawezi kusimamia fedha za walipa kodi, hawawezi kuwajali ile raslimali watu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo Mhe. Waziri akitoka kwenye kikao hiki saa nane na nusu *inshaalla* kesho ukija hapa uje na fedha za wafanyakazi wetu Uholanzi, vyenginevyo hatuelewani. Mhe. Mwenyekiti siungi mkono hoja mpaka nipate majibu Mhe. Waziri ya vitendo na sio hadithi, hadaa za Ole na sehemu nyengine Mhe. Mwenyekiti sitozikamata. Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii nitoe michango yangu kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo. Mhe. Mwenyekiti na mimi nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa uteuzi alioupata wa kushika Wizara hii, tunaamini kwamba mabadiliko yatapatikana makubwa kwa utendaji wake tunavyomfahamu. Mhe. Mwenyekiti kama ulivyotuelekeza tusirejee rejee lakini kuna mengine lazima turejee maana inabidi tuongeze chumvi tukienda tu yakishasemwa tuyaache, naona tutakuwa hatufiki.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 12 wa kitabu cha hotuba cha Mhe. Waziri kwenye Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili mimi nilikuwa nataka nigusie mahala ambapo katika kupita pita na kamati tuligundua kuna kitu kimoja

kinafanyika ambacho si kizuri. Tulitembelea minara ya televisheni kule Masingini, Mhe. Mwenyekiti kwa masikitiko makubwa kabisa pale, tulikuta tatizo pale kuna tajiri mmoja na yeye ana minara pale ya kuendesha mitambo yake sijui mambo ya *internet* na vitu kama hivyo. Lakini yeye alikuwa amekosana na watu wa umeme anadaiwa Shirika la Umeme huko akawa amekatiwa umeme wake.

Kwa hivyo yeye akachukua waya akenda akaunga kule kwenye televisheni Zanzibar. Kwa kweli sisi baada ya kufika pale na kuona kitendo kile, hatukuwa tumeridhika. Kwa sababu fedha anazozitumia ni fedha za walipa kodi zinaenda kutumika kwa mtu binafsi, ni kitendo cha kuwaonea wananchi wetu. Yewe ni biashara yake kule anafanya lakini umeme anaoutumia ni umeme wa televisheni Zanzibar. Kwa hivyo hebu Mhe. Waziri ili unitoe mashaka uje unipe maelezo, hatua ambazo mmechukua kwa mtu yule, na kama kuna deni ambalo mmelipa lile deni kama kuna *fine* ambayo mmemtoza uje unieleze hapa mmemtoza kiasi gani? Na ule umeme wetu pale ameutumia kwa kiasi gani, maana yake kwa hasira tu ilibidi tuukate pale pale tukaukunja na waya, halafu tukamwambia kama ana malalamiko aje huku aje atudai, lakini hatukuona malalamiko mpaka leo lakini tuliuita uongzi wa televisheni Zanzibar tukawaeleza hili na tukawataka wachukue hatua. Sasa Mhe. Waziri hebu naomba sana uje unisaidie maelezo katika kadhia hii. Nikishapata maelezo ya kutosha basi Mhe. Waziri hakuna wasiwasi tutaendelea mbele.

Mhe. Mwenyekiti nikiendelea mbele nije kwenye ukurasa 31 Shirika la Magazeti ya Serikali. Mhe. Mwenyekiti juzi mimi nilikwenda kwenye hili Shirika, lakini nilisikitishwa sana na ile hali ambayo niliikuta pale na nilipata malalamiko kwa watendaji na mimi mwenyewe nikaona ile hali halisi ilivyo, wamehamishwa, kutoka kwenye jengo ambalo wakitumia wamepelekwa jengo jengine ambalo halikidhi mahitajio yao na hii pia imesababisha siku mbili gazeti hili kutokuwa hewani. Ninafikiri Mhe. Waziri yeye mwenyewe ni shahidi kwamba kwa muda wa siku mbili gazeti hili halikuweza kutoka kutokana na matatizo ya kuhamishwa kwa ghafla.

Hebu Mhe. Waziri aje anisaidie kidogo maelezo tatizo ni nini mpaka akafika kuwahamisha watu hawa kutoka kwenye jengo ambalo walikuwa wakilitumia kuwapeleka jingo ambalo ni dogo zaidi kuliko kule ambako pia wakijibana. Maana huko mwanzo waliko kuwepo kulikuwa hakuwatoshi. Huko mlikowapeleka kama kule walikuwa wakitumia vyumba kumi huku mmekwenda kuwapa vinne, mmekuwa mmeenda kuwapunguzia zaidi. Hebu Mhe. Waziri njoo unisaidie hasa tatizo hasa ni nini mkakurupuka kiasi hiki kiasi kwamba mmefika mahala lile gazeti sasa limekuwa linatoka kwamba ni lazima litoke tu, lakini kama si vyenginevyo vyo vyote si uzalendo wa hawa watendaji basi gazeti hili sasa hivi lingekuwa haliko hewani mpaka hii leo.

Lakini nikiendelea mbele Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana Mhe. Waziri wa Habari alipokuwa akiwasilisha bajeti yake hapa alituzungumzia suala la ujenzi wa kituo kile cha utamaduni, mambo ya kurekodi muziki, mambo mengine mengine. Sasa katika hotuba yake Mhe. Waziri hapa, mwaka jana alitwambia ujenzi wa kituo, lakini mwaka huu ukarabati wa jengo la kituo. Sasa mimi napata shaka kidogo maana ujenzi huu ulikuwa ufanyike walikuwa wame-propose Tunguu au Chumbuni kitu kama hivi sina uhakika vizuri, lakini mwanzo walisema Chumbuni baadae wakasema Tunguu, sasa mwaka huu naona umekuwa ukarabati wa jengo uliokuwa studio ya zamani.

Sasa mimi Napata shaka kidogo, huku umetwambia unajenga, ujenzi wa kituo cha kisasa kabisa, lakini huku unakwenda kukarabati jengo la iliyokuwa studio. Sasa sisi huku unatuomba fedha za ujenzi wa jengo, kumbe wewe unataka kwenda kukarabati. Sasa Mhe. Waziri hapa kidogo nataka uje unisaidie maelezo ya kina yamekwenda vipi mpaka ukawa hujakipata kiwanja cha kujengea studio ya kisasa, matokeo yake unakwenda kuwahamisha watu wa gazeti ili uweze kukarabati kufikia yale malengo. Sasa kunaonekana kama kuna hadaa kidogo maana uonekane angalau umefanya au unatekeleza yake ambayo umeyaahidi, japo kwa kubana bana tu.

Sasa mimi naona hili si sahihi, kama ulituahidi unakwenda kujenga ujenzi wa kituo cha kisasa basi ulikuwa ukaanze ujenzi wa kisasa. Lakini unapokwenda kutukarabatia jengo halafu ukatwambia sasa kitakuwa kituo cha kisasa huku hata kama umewafukuza wanao wengine ili tu uonekane umefanya hapa Mhe. Waziri mimi kidogo sijakuelewa na ningekuomba sana uje unisaidie maelezo ya kutosha katika suala hili mpaka niridhike. Basi nikisharidhika Mhe. Waziri mimi hakuna wasiwasi bajeti yako hii nitaipitisha, lakini kama sikupata maelezo ya kina katika kadhia hii basi kidogo hapa nitakushika koo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee mbele kwenye ukurasa wa 42 Kamisheni ya Utalii. Mhe. Mwenyekiti mimi niipongeze Kamisheni ya Utalii kwa kazi nzuri inayofanya. Kama ujuavyo Mhe. Mwenyekiti, utalii ni sekta moja ambayo inaliingizia kipato taifa letu hili. Sasa ndugu zetu hawa au Kamisheni hii ya Utalii inajitahidi katika kazi zake. Na kweli mafanikio haya ya utalii yanayoonekana ni moja kati ya juhudi za Kamisheni hii. Lakini ukiitizama bado hatujaipa nafasi vizuri zaidi. Tunawapa majukumu mazito lakini tunawanyima fursa zaidi.

Kamisheni ya Utalii kwa kweli ina matatizo kidogo hasa katika usafiri, kwa sababu Kamisheni ni lazima ifanye *patrol* lakini usafiri ni hafifu, hawana magari pale, mimi nimeshakwenda pale, tumeshakwenda na kamati mimi mwenyewe ninakwenda pale. Katika mwaka jana nafikiria ndio wamenunua gari moja, gari moja hiyo hiyo apande Mkurugenzi wa Kamisheni, gari hiyo hiyo atumie Muhasibu kwenda benki, gari hiyo ikafanye *patrol*, gari hiyo hiyo ikashughulikie kesi. Sasa kwa kweli hapa pana tatizo ninamuomba sana Mhe. Waziri aiangalie vizuri Kamisheni, aiwezeshe iweze kufanya kazi zake vizuri zaidi.

Mimi nilikuwa na rai moja, kwa kuwa Kamisheni inakusanya na tukiangalia makusanyo yake ya mara hii yalivyooneshwa hapa yamevuka lengo kabisa, tuipe hongera sana Kamisheni kwa kuvuka lengo kubwa sana. Ninafikiri imekwenda mara moja na nusu ya kile ambacho kimekuwa kimekusudiwa ni kazi nzuri inafanyika. Sasa rai yangu Mhe. Waziri tuiangalie Kamisheni, kwa nini tusiwe tunawapatia asilimia ya kile ambacho wanakikusanya ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri zaidi kama taasisi nyengine zinazokusanya kwa mfano ZRB, ZRB wanakusanya lakini wanapewa asilimia. Wale Mamlaka ya Uwanja wa Ndege wanakusanya, wanapewa asilimia ya makusanyo kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao. Kwa nini Kamisheni na wao wanachokikusanya tusiwatafutie asilimia tukawapa.

Mimi ninafikiria Waziri wa Fedha yupo kama hayupo salamu atazipata, lakini Mhe. Waziri ningekuomba hili ulisaidie ili kamisheni hii iweze kufanya wajibu wake vizuri zaidi. Kwa sababu wanasema mcheza kwao kutunzwa na hawa wanacheza vizuri, kama wanacheza vizuri kwanini tusiwatunze hapana shaka Mhe. Waziri si mkaidi wa mambo kama haya nina hakika utalifikiria

vizuri hili uweze kuwasaidia hawa ili nao waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi kwa ufanisi zaidi na zaidi.

Mhe. Mwenyekiti mimi nasogea tena mbele kidogo kwenye ukurasa wa 1948 Chuo cha Utalii. Mhe. Mwenyekiti, hiki ni Chuo chetu kinasomesha vijana wetu na wengine kutoka nje ya kwetu katika fani hii ya utalii. Lakini mimi Napata shaka kidogo wa wahitimu hawa wanaotoka katika Chuo hiki kutokupata ajira. Sasa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atusaidie kuna uhusiano gani wa karibu baina ya hawa wawekezaji kwenye sekta hii ya Utalii na Chuo hiki cha Utalii kwamba hawa wanafunzi wanaotoka pale wakienda kule wanapata ajira au mna mausiano gani mnawasaidia vipi vijana wetu wanaotoka pale katika suala zima la ajira, hili nafikiri litakuwa linakuhusu wewe, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika mana naye yumo Maalim Haroun, mnawasaidia vipi kwa sababu chuo kinasomesha na tumekiweka makusudi kwa ajili ya kusomesha vijana wetu. Walimu wanajitahidi kutoa mafunzo pale, watoto wetu hawa wanapasi vizuri sana kabisa, lakini suala la ajira kidogo linakuwa tatizo. Sasa nilikuwa nakuomba Mhe. Waziri uje unisaidie sijui uhusiano wenu ukoje katika Sekta hii ya Utalii na chuo hiki. Wanashirikiana vipi katika kuhakikisha kwamba wanafunzi ambao wanatoka pale wanapata angalau kipaumbele katika ajira kwenye Sekta ya Utalii. Hilo ndilo nililoliona.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisogee mbele kidogo hapo kwenye ukurasa wa 53 Shirika la Utalii. Mhe. Mwenyekiti, mimi sijui niliite shirika au niite taasisi tu hii, kwa sababu katika kuendelea kuliita shirika mimi naona kama itakuwa halistahiki. Kwa sababu shirika lolote mimi najua linakuwa na bodi lakini shirika hili halina Bodi ya Wakurugenzi tena muda mrefu sana. Mwaka jana hapa tulipiga kelele sana tukasema sana juu ya shirika hili, tukapewa ahadi kemkem hapa lakini mimi naona hata moja haijatekelezwa. Tulikubaliana shirika hili litakuwa na bodi kama litaendelea kuwepo kwamba shirika, lakini kama litakuwa si shirika basi litafungwa hili. Mimi nakuomba sana Mhe. Waziri hebu tusaidie hili shirika bado lipo hai au ushaliuwa? Kama lipo hebu tusaidie lina wafanyakazi wangapi na lina nini na nini hizo shughuli zake hasa.

Kwa sababu ukitizama huku katika kitabu chako cha mwaka jana lina malengo yaliyojiwekea yatakayotekelezwa mwaka huu, lakini sasa hivi ukitizama hakuna hata moja lililotekelezwa. Sasa mimi napata shaka kuwepo kwa shirika hili, kama serikali imeamua kuliondosha au kulivunja shirika hili basi ni vyema wakalivunja ili tukajua halipo kuliko kuendelea kuliita shirika lakini hakuna kinachofanyika kama shirika. Kwa sababu kama hiyo bodi haikuteuliwa huyo Meneja wa Shirika hawezi kuiteuwa bodi yeye Serikali Kuu ndio inayoteuwa huko, Mhe. Waziri ndio unaeteuwa wajumbe sasa tatizo ni nini mpaka leo shirika hili linakuwa halina bodi linafanya kazi zake vipi hili, ni kuendelea tu kutumia fedha za walipa kodi kwa ajili ya shirika hili shirika ambalo sioni tijara inayoifanya ni hasara tu. Ni vyema mkaamua moja, ama kuliondosha ama kulihuisha.

Sasa Mhe. Waziri nakuomba sana utakapokuja kwenye majumuisho yako hapa uje unieleze nini hasa serikali mnakusudia juu ya shirika hili, kama mmeamua kulivunja basi ututangazie hapa kwamba umeshalivunja hili shirika na kama linaendelea kuwepo utwambie kwamba lipo lakini utueleze linakuwaje kwa sababu hata mwaka jana mmetwambia haya haya, sasa hebu mwaka huu naomba kidogo mbadilishe mje na kauli nyengine lakini ikiwa ya mwaka ule basi hili shirika katika sehemu ambazo nitakuwa nazuia basi ni shirika hili kuendelea kuwepo kwake mpaka nipate maelezo ya kina juu ya shirika hili.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie kwenye ukurasa wa 57 Hoteli ya Bwawani nitazungumzia kidogo sana kwa sababu wenzangu wameshazungumza. Kuna kadhia kubwa sana ya wafanyakazi katika Hoteli ya Bwawani, ni kweli wafanyakazi wale wapo pale miaka mingi lakini kwa kweli hawana ajira ya kudumu, wako wawili watatu wenye ajira lakini wako wengi wao hawana ajira ya kudumu. Kwa nini Mhe. Waziri hiki kitendo kinaendelea kuwepo ndio tushalalamika na mwaka jana pia tulizungumza hili, tulizungumza juu ya ajira pale mwaka jana katika Hoteli ya Bwawani mkatuahidi kwamba tutahakikisha ajira zao zinakamilika haraka iwezekanavyo. Sasa hebu utakapokuja Mhe. Waziri uje utupe utaratibu mzima mnaoutumia juu ya wafanyakazi wale wa hoteli ile.

Mhe. Mwenyekiti, umeharakiza ili nisiumalize ule muda ulionipa niingie kwenye mafungu, nimegundua kuna mafungu mengi hapa yanahitaji maelezo Mhe. Waziri, utapokuja unisaidie. Mhe. Ismail Jussa ameyasema mengi sana na mimi ninayarejea kidogo kwenye kasma ya 0201 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti *vote* 220500 hasa kwenye fungu la 220517 linahitaji maelezo yake ya kina. Tukienda kwenye 0301 Ofisi Kuu Pemba *sub vote* 220700 na 220701.

Mhe. Mwenyekiti (Mhe. Mamoud Muhamed Mussa): Mhe. Mjumbe zungumza taratibu ili Mhe. Waziri aweze ku-*quote* vifungu vyako.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakimbilia ule muda wako Mhe. Mwenyekiti, niachie niendelee kidogo kidogo lakini na muda nao uniachie niende nao basi.

Mhe. Mwenyekiti: *Inshaallah,* jitahidi akufahamu unachotaka kumuelekeza.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Anasikia vizuri Mhe. Waziri huyo. Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti Kasma 0201 niende kwenye Kasma ya 220500 kifungu 220517 Utayarishaji wa Mpango Bajeti shilingi milioni nane hizi. Mhe. Mwenyekiti, nataka maelezo yake hii utayarishaji wa Mpango Bajeti. Nikisogea mbele kwenye Ofisi Kuu Pemba Kasma 0301, nasogea kwenye Kasma 220700 Matengenezo Ofisi Nyumba, kuna Kasma 220701 Matengenezo Madogo ya Ofisi kuna shilingi milioni sitini na saba hapa, lakini mwaka jana ulikuwa na shilingi 13 milioni na mwaka huu unataka shilingi sitini na saba za matengenezo madogo ya ofisi.

Nikisogea mbele kwenye Kasma 311200 Ununuzi wa Mashine na Zana kwenye *sub vote* 311203 ununuzi wa *Honda*, Vespa na *Ciao* mwaka jana alikuwa na shilingi milioni kumi kanunua *Honda*, Vespa na *Ciao* na mwaka huu anataka shilingi milioni tano kwa ajili ya Vespa, *Honda* na *Ciao*. Kwa hivyo, kila mwaka ananunua *Honda*, Vespa na *Ciao* nilikuwa nataka maelezo kidogo kwenye hili. Na kwenye Kasma 311205 Ununuzi wa Friji shilingi milioni sita na laki tano.

Nikisogea mbela kwenye Kasma 0401 Utumishi na Uendeshaji kuna fungu la 220200 viburudishaji, kwenye *sub vote* ya 220201 Chakula na Vinywaji kwenye shilingi milioni kumi na sita. Nilikuwa nataka maelezo katika hili.

Nasogea kwenye *vote* ya 220500 Vifaa na Huduma nilikuwa nahitaji maelezo katika *sub vote* ya 220504 Vifaa vya Kompyuta kuna fungu la shilingi milioni kumi na tano hapa lakini mwaka jana

alikuwa ameomba shilingi milioni nane, mwaka juzi shilingi milioni saba. Kwa hivyo kila mwaka kuna mamilioni kwa ajili ya vifaa vya kompyuta inaonekana hizi kompyuta zako zina matatizo. Sasa hebu tusaidie maelezo, si vyema ukanunua mpya kabisa kuliko kuwa unanunua vifaa tu, mana hili fungu ni kubwa mno. Sasa nilikuwa nahitaji maelezo katika hilo.

Halafu nikienda kwenye Kasma hiyo hiyo kwenye *sub vote* ya 220507 Ufukizaji. Mwaka jana uliomba shilingi milioni moja na laki sita kwa ajili ya ufukizaji lakini mara hii unataka shilingi milioni tatu na laki mbili kwa ajili ya ufukizaji. Sasa hebu tusaidie kidogo mwaka jana shilingi milioni moja laki sita zilikutosha lakini mara hii umetaka mara mbili ya ile sijui una jengo jengine unataka kwenda kufukiza au vipi.

Nije kwenye fungu 220515 hapo hapo kwenye vifaa vya michezo kuna shilingi milioni thelathini na tano, mwaka jana zilikuwa shilingi ishirini na tano milioni kwa michezo katika idara moja tu hiyo ya utumishi na uendeshaji.

Nikitoka hapo nasogea chini kidogo kwenye *vote* ya 220600 kifungu kidogo 220601 Ununuzi wa Mapazia. Kila mwaka ofisi hii unanunua mapazia, mwaka juzi ulikuwa na shilingi milioni kumi na nne ununuzi wa mapazia, mwaka jana shilingi milioni mbili, waka huu umetoka umekwenda kwenye shilingi milioni ishirini kwa ajili ya mapazia tu. Sasa hebu Mhe. Waziri uje utusaidie ufafanuzi katika fungu hili, mapazia haya kila mwaka unayonunua ina maana mwenzetu imekuwa kama kila sikukuu unabadilisha.

Nikisogea kwenye Kasma ya 220700 Matengenezo ya Ofisi na Nyumba, nije kwenye *sub vote* 220701 Matengenezo Madogo ya Ofisi. Mwaka jana uliomba shilingi milioni kumi na tatu na laki tano, mwaka huu unahitaji shilingi milioni kumi na tano kwa matengenezo madogo ya ofisi. Lakini wakati huo huo kwenye fungu la 220702 unahitaji shilingi milioni mia mbili kwa ajili ya matengenezo makubwa. Sasa hapa una matengenezo makubwa, lakini wakati huo huo utakuwa na matengenezo madogo, ofisi hiyo hiyo moja matengenezo mawili kwa wakati mmoja itakuwaje. Naomba maelezo katika mafungu haya.

Nikiendelea mbele Mhe. Mwenyekiti, nisogee kwenye Kasma 263100 kwenye *sub vote* ya 263178, tuko pamoja Mhe. Waziri? Kuna Ushauri Nasaha, *HIV* shilingi milioni kumi na nne. Naomba maelezo katika fungu hili.

Halafu nikishuka chini yake kidogo hapo kwenye Misaada ya Kijamii *vote* 272100, tusogee kwenye *sub vote* 272108 Kusaidia Shughuli za Kiuchumi na Jamii mwaka jana uliomba shilingi milioni kumi na tatu na laki moja, mwaka huu unaomba upewe tena shilingi milioni tano kwa ajili ya shughuli hizo naomba maelezo yake. Ningependa unipe hizi za mwaka jana ulivyozitekeleza hata ukawa unaomba hizi nyengine katika shughuli hizo za kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, nikisogea tena katika fungu 311200 niende kwenye *sub vote* ya 311203 Ununuzi wa *Honda*, Vespa na *Ciao*. Hapa napo mwaka jana aliomba shilingi milioni tano, mwaka juzi shilingi milioni nne na laki nane, mwaka huu anaomba tena shilingi milioni tano kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivi. Hivyo Mhe. Waziri hebu tueleze hasa shida ya vifaa hivi ulivyonavyo unataka kiasi gani, labda vespa kumi, kumi na mbili na hizo *ciao* ngapi, manaake kila mwaka fungu hili unaliomba tena.

Mhe. Mwenyekiti, nishuke chini yake hapo hapo 311205 kwenye Ununuzi wa Friji. Mwaka jana ulinunua friji la shilingi milioni laki tano, mwaka huu unahitaji shilingi milioni tatu nyengine kwa ajili ya friji. Hapa nataka maelezo vile vile Mhe. Waziri.

Nije tena chini yake kidogo hapo 311207 Ununuzi wa Kompyuta, kila mwaka hapa unanunua kompyuta Mhe. Waziri tukianza mwaka juzi ulikuwa una shilingi milioni kumi na moja laki saba, mwaka jana shilingi milioni kumi na mbili, mwaka huu unahitaji shilingi milioni kumi na tano. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja utupe maelezo kidogo katika mafungu haya niliyokueleza ili tuweze kukurahisishia kukupitishia bajeti yako kwa wepesi zaidi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Kasma 0701 Idara ya Habari Maelezo, nayo imenishitua kidogo. Kwenye *sub vote* ya 211110 Posho Maalum nalo kidogo limenishitua hapa kuna shilingi milioni kumi na nane laki nne na elfu thelathini kidogo Mhe. Waziri nilikuwa nataka maelezo yake hizi au uchanganuzi wake vizuri ili niweze kujiridhisha.

Lakini nikisogea chini kidogo hapo kwenye *vote* 211200 *sub vote* 211202 Ununuzi wa Sare. Nilikuwa nataka kujua hizi sare sijui ndo kwa wafanyakazi wa Idara ya Habari wote manaake pana fungu dogo tu la shilingi milioni moja na laki tano, naomba maelezo yake vizuri ili nijiswafi nafsi na niweze kukupitishia vizuri bajeti hii usiwe na wasi wasi rafiki yangu.

Nikisogea mbele kwenye *vote* ya 220600 Samani na Ofiri katika Idara hii ya Habari Maelezo kuna *sub* voite ya 220601 kwenye ununuzi wa mazulia na kapeti, nayo hii imejirejea kama ile ya kule kila mwaka kuna fedha hapa unazoziomba kwa ajili hii. Sasa sijui hizi ofisi unahama hama kila siku kwa ajili ya kubadilisha au laa, nilikuwa nahitaji maelezo pana shilingi milioni tano hapa unahitaji kwa ajili ya shughuli hiyo. Kwa hivyo, naomba maeleoz yake hiyo.

Lakini wakati huo huo nikishuka chini kidogo kwenye *vote* ya 220700 *sub vote* 220702 Matengenezo Makubwa ya Majengo unaomba shilingi milioni saba. Sasa nahitaji maelezo yake na hizi ili tuweze kuona namna ambavyo fedha hizi utavyozihitaji na matumizi yake.

Mhe. Mwenyekiti, nikisogea mbele kidogo

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe tuzingatie muda.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Umeniomba Mhe. Mwenyekiti, niende kidogo kidogo ili asikie Mhe. Waziri na nilikuwa najua utanambia tu muda. Naomba Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima ya kiti chako unipe muda tena kidogo nimalizie malizie au tukubaliane kwamba kila fungu ambalo ninaliona lina kasoro wakati wa kuja kutoa mchanganuo nikiwa sikumpata vizuri bsi buti iendelee kama kawaida. Tukikubaliana hilo Mhe. Mwenyekiti, mimi nikae kitako.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa tumekuelewa, umuandikie lakini Mhe. Waziri.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniruhusu hilo nitaandika. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, siungi mkono hoja mpaka nipate maelezo ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti: Tujitahidi tuzingatie muda na wengine waweze kuchangia jamani. Ahsante.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nami kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri. Nichukue nafasi ndogo tu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia mchana huu kuwepo hapa kuendelea na shughuli zetu. Pia nikushukuru wewe kidogo kwa kunipa nafasi hii na nimpongeze Waziri kwa mara ya kwanza kuwa waziri wa wizara hii na kuwasilisha bajeti yake hapa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na Shirika la Utangazaji, hapa limetajwa kuwa majukumu yake ni kutoa habari, kuelimisha, kuburudisha na kuhamasisha jamii juu ya masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi nchini petu tunavyo vyombo kadhaa vya habari, lakini Shirika letu la Habari ikiwemo Televisheni na Redio hana ndio ya mwanzo kuwepo kabla ya mengine yote. Na niseme haya ndio mdomo wa serikali, yote Serikali yanayofanya yanatangazwa na vyombo hivi. Lakini tujue kwamba hivi sasa kuna vyombo kadhaa televisheni, magazeti, redio za watu binafsi ambazo zinafanya kazi hapa nchini petu Zanzibar. Kwa hivyo, kuna ushindani mkubwa wa habari, ningeomba serikali isijekuwa mkiani ikashindwa na vyombo hivi vilivyochipua juzi na hawa wapya wakaja wakachukua nafasi kubwa kuliko Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kumetajwa kitu kutoa habari ningeviomba vyombo vyote vya habari vya Serikali na taasisi binafsi vihakikishe kuwa wanapotoa habari watoe habari za kweli bila kupotosha jamii.

Mhe. Mwenyekiti, vyombo vya habari vinaweza vikaiweka jamii pamoja kutokana na habari zao wanazotoa, vyombo vya habari wanaweza kuisambaratisha jamii kulingana na habari zao wanazotoa. Kwa hivyo, kila chombo cha habari lazima kiwe makini kuhakikisha kwamba umoja huu tuliofikia hapa, malengo yaliyofikiwa kamwe yasibaguliwe au yasipanguliwe na vyombo vya habari.

Mhe. Mwenyekiti, CCM huwa inahubiri sera yake moja kuwa ni amani na utulivu, *CUF* tunasema sisi tutanunua amani kwa bei yoyote ile, ukiwaweka pamoja hawa wote wawili wanataka amani na kwa kiwango fulani tumeifikia. Sasa kazi ya vyombo vya habari katika kutoa habari na kuelimisha jamii tuhakikishe kuwa haya maendeleo yaliyofikiwa ya utulivu katika nchi yanadumu na yanaendelea kusiwe na habari ambayo itasababisha mtengamano baina ya jamii, baina ya mtu na mtu, baina ya chama na chama na kadhalika. Lengo ni kuimarisha na kujenga.
Mhe. Mwenyekiti, shunguli nyengine ya vyombo hivi ni kuburudisha, pia kwenye burudani hizi kwa hapa Zanzibar ningeliomba ziende na misingi yetu na tamaduni zetu za Kizanzibari. Pale tunapoburudia kwa sababu burudani ni michezo ya kuigiza, ngoma, nyimbo na kadhalika. Sasa haya yote iwe hayakiuki misingi ya utamaduni wetu wa Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya vipindi tunavyovitazama ingawa tumeshazowea tunakaa na wake zetu na watoto wetu wengine wakiume, lakini yanayotokea pale mmoja wapo hujitia haja kuondoka kumbe kaona kitu ambacho hakuridhika nacho. Na hivi vinatolewa na vyombo vyote vya serikali na vile vya binafsi bila ya kuzingatia utamaduni wa watu wa nchi hii. Kwa hivyo, ningeviomba vile vya serikali na Serikali kwa ujumla wizara hii kwa sababu ndio msimamizi mkuu wahakikishe kuwa jamii tunailea katika maadili yetu ya kizanzibari wala sio maadili mengine ya Magharibi au kwengineko.

Mhe. Mwenyekiti, ili haya yapatikane lazima hiki Chuo cha Habari kiwe ni chuo makini kinachoelimisha waandishi vyema, watu wa magazeti na wengineo ili wanapoajiriwa na kwenda kazini waweze kufanya kazi hii kwa ufanisi na mahitaji ya Wazanzibari yalivyo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kidogo tu juu ya Kamisheni ya Utamaduni na Michezo. Katika kuhitimisha Mhe. Waziri alisema takriban sote tunapenda michezo wala kauli yake haina doa, sote tuliomo humu kila mmoja ni mchezaji ama anapenda au anapenda kutizama michezo. Kwa hivyo, kule kupenda tu ni sehemu ya kuwa mchezaji, ukicheza ni mchezaji ama mchezo huu au mwengine lakini kila mmoja wetu anapenda michezo.

Idara ya Michezo Mhe. Mwenyekiti, imeonekana inatilia mkazo zaidi mchezo wa Mpira wa Miguu kuliko mwengineo wakati ambapo ziko *games* chungunzima ambazo kwa sasa zimeachiwa hazishughulikiwi, sasa nazo hizi zitiliwe mkazo ili kuimarisha afya za vijana wetu. Ningeomba baadhi ya michezo sio ngoma za utamaduni lakini michezo kama riadha, mpira wa miguu, *tennis* na nyenginezo zikarejeshwa maskuli kwa sababu kule ndiko kwenye watoto au vijana wenye uwezo wa kujifunza michezo na hatimaye kuendelea. Kwa hivyo, ningeomba wizara hii Mhe. Mwenyekiti, ishirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kufunza michezo katika skuli zetu kuweza kukuza vipaji vya watoto wetu ili tuweze kutoa wachezaji bora wa michezo yote ambayo tumeikubali.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwa upande wa utamaduni. Tungeomba kuwa mafunzo ya utamaduni ambayo tutayaonesha katika vyombo vyetu vya habari yalingane na Uzanzibari wetu. Kwa sisi Wazanzibari asilimia yetu kubwa tuko Waisilamu, kwa hivyo wizara hii kwa mara nyengine tena ishirikiane na Wizara ya Elimu katika kutoa mafunzo mbali mbali kwa vijana wetu katika kuwafundisha maadili bora ili hatimaye wawe raia wema wa nchi hii watakaoweza kuendeleza silka, mila na utamaduni wa Mzanzibari. Hii isiwe siku za maonesho tu, kuwa tuna utamaduni wa Kizanzibari lakini iwe ni jambo la kuendelea linalofunzwa, sio ngoma. Kwa kawaida vyuo vyetu huwa vina mashindano ya usomaji wa Quran, Khadithi na mengoneyo katika Mwezi wa Ramadhan. Idara hii ya Utamaduni tuchukulie kuwa na dini ni sehemu ya Utamaduni kwa hivyo washirikiane na vyuo hivi katika kuikuza taaluma hii na hata pale wanapoweza pia na wao wasaidie katika kutoa motisha.

Mhe. Mwenyekiti, tukifanya hivyo hatimaye tutaweza kujenga taifa la Wazanzibari lenye heshima, lenye malezi mema ambalo litaweza kututoa katika dimbwi kubwa ambalo hivi sasa tayari tumeingia katika uvutaji wa madawa ya kulevya, kuvaa nguo ambazo haziridhishi na kusuka nywele kwa wanaume ambapo ni kinyume na maadili yetu ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii kwa ujumla wake ina mambo kadhaa ambayo yakitekelezwa yanaweza yakalifikisha taifa hili pahala pazuri. Kwa kuwa ni suala linahusu utamaduni pamoja na kuwa na uhuru wa kila mtu kufanya atakalo ambalo havunji sheria. Kuna mambo Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa huvunji sheria ndio kuvunja sheria, lakini kufanya anavyotaka na akawa havunji sheria, mtu kutembea nusu uchi, kwa nini havunji sheria.

Lakini sisi tunaona kila mtu ana uhuru wa kufanya anavyotaka mara nyengine anafanya vile anavyotaka almuradi havunji sheria, havunji sheria ipi? Kwa kweli suala la mavazi Mhe.

Mwenyekiti, ni tatizo, tena tatizo sugu, tunatumia kipengele kwa kila mtu ana haki ya kufanya anavyotaka almuradi havunji sheria, lakini hii sheria ambayo haivunjwi haisemwi ni sheria gani?

Kwa sababu haikusemwa ni sheria gani kila mtu atakwenda anavyotaka. Sisi hapa kama kungekuwa hapakuwa na sheria maalum kuna watu wangekuja na mini skirt humu. Lakini atleast humu ndani labda kuna sheria maalum ya kuvaa vyenginevyo watu wangekuja na vivazi vya mini skirt, wengine wangekuja na fulana za timu wanazozipenda. Lakini kutokana na sheria iliyoekwa ya Baraza, kila mtu anakuja na nguo ambayo kimtazamo haivunji sheria ya hili Baraza.

Lakini huyu mwananchi huko nje ni kuwa havunji sheria ipi katika kivazi alichovaa. Nchi ina sheria gani ya mavazi. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naomba mimi nikae ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Jitahidi kujali muda wako.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ninakushuru kwa kutumia muda wako kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, Muumba mbigu na ardhi na viliomo ndani yake. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Rais kwa kumuona Alhaji Said Ali Mbarouk kwamba ndio kifaa cha kufanyia kazi wizara hii. Katika hilo tuliomba sana watendaji wa Wizara hii, kwanza niseme mimi ni mjumbe wa kamati hii. Tuliwaomba watendaji wamsaidie Mhe. Waziri, wampokee kwa imani lakini ile dhana ya Mhe. Rais kumpeleka pale iweze kufikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, karibuni tulipokuwa tunaipitia bajeti hii kama kamati, tulimpa yale machache ambayo kama wajumbe tulikuwa tunayasikia yananong'onwa. Huko Bungi mnarani kuna nini na hii jenereta ya Masingini kuna yepi.

Mhe. Waziri bado sisi tuna imani kwamba unaweza lakini ukija ukishindwa kumtoa kepu kwenye ukucha, jitayarishe kukata mguu. Hiyo ndio lugha ambayo tunakueleza wazi, hatutokutizama usoni wala hatutotafuna maneno. Kazi ni kwako mwenyewe pale ambapo unahisi aah! hapa ni pa Rais mwenyewe, mpelekee watu wake.

Baada ya kusema hayo nije kutia baraka tu ndani ya Wizara. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ni kubwa. Pesa ya kutumia ili wizara iweze kuonekana ni kidogo na zenyewe kuingizwa kwake ndivyo hivyo hivyo tena, hadi Aprili mpaka Aprili, kutoka Aprili hadi hapa tulipo hatujui pameingia nini.

Lakini kwa ujumla chini ya Katibu Mkuu wa Wizara hii kunafanywa kazi vizuri, ya kibinadamu ya hapa na pale yataendelea kuwepo. Ya makusudi Mhe. Waziri unaona. Ya kibinadamu yanajulikana.

Idara ya Mipango, Sera na Utumishi nikupongezeni kwa dhati na Mhe. Waziri nenda na utamaduni wa kuwafundisha wafanyakazi kadri utakavyomudu, hao ndio watakaokusaidia wewe lakini na taifa hili.

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya habari ina vikorombwezo vingi. Lakini Mhe. Waziri nikiulize munasema munakwenda kwenye majaribio ya teknolojia ya *digital*. Hivyo mambo yameshakamilika ama bado ni ile ile transmitter. Maana hii bajeti ulipoisoma watu wameisikia.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, michezo ni ajira. Kiwanja cha Amaan kilijengwa kwa fahari kubwa ndani ya Afrika ya Mashariki. Mhe. Waziri ndugu yangu juzi tulipokuwa tunasikia kuna mashindano fulani yameahirishwa kwa ubovu wa uwanja wa Amaan hatukufurahi. Tulijisikia aibu na wengine tulikuwa ugenini tukashindwa kujikunjua. Hebu Mhe. Waziri tueleze kuna nini.

Kiwanja cha Amaan kwa sasa Zanzibar na kiwanja hiki si karibuni sana lakini kilipata matengenezo makubwa ya ndugu zetu wa China. Sasa maradhi ni yale kwamba tukishasaidiwa wenyewe tunajisahau. Mpaka leo kinashindwa kutumika lakini jengine kwa kiwanja hicho hebu Mhe. Waziri tulizungumza sana hili kama kamati kwamba kiwanja hiki kuendelea kukifanyia shughuli zetu za sherehe tunakimaliza, hakihimili vishindo vile.

Tukasema tuhamie uwanja wa Mao-Tse-Tung na pale twende na michezo ya yale ambayo yatakayoweza kufanyika. Hili limefikia wapi? Mwenzangu mmoja kakumbusha kwamba tuna sherehe za miaka 50 inshaallah, tunakwenda wapi au tunakwenda kukimaliza kiwanja cha Gombani Pemba. Tukivimaliza vyote tutaelekea wapi. Mhe. Waziri haya ni ya kuyatafakari.

Lakini jengine katika eneo la michezo ninataka nikwambie Mhe. Waziri na Wazanzibari kwamba Adam Nditi, huyu ana wenzake wengi hapa Zanzibar na leo tunajivunia amesajiliwa Chelsea. Lakini ilikuwa tuhesabu zaidi ya watano hadi sasa, tumewapoteza. Vipaji vipo na tena vingi Zanzibar. Wenzetu wa Afrika Mashariki na Kati wanalijua hilo lakini watu wanasema, “Penye miti wajenzi mtihani”.

Mhe. Mwenyekiti, vile viwanja vya humu mitaani mwetu tunamuoishi, watoto wanavitumia viwanja vile ndio mule munamoibuka vile vipaji, na mule ndipo wanapoonekana. Hebu wapeni fursa watoto wacheze kwenye maeneo haya ya wazi, wakubwa waachieni musivichukue viwanja. Tunapoteza vipaji hivi vya watoto kwa kujisahau kuona kila kitu ni wakubwa, si hivyo. Hawa watacheza wapi. Una pesa zako kasri kajenge hata baharini una pesa wewe, unachukua hata humu musimochukulika.

Tatizo jengine la Serikali kuwa na nguvu ya soda, yakurupuka hatimaye kimya. Basi watu wameshajenga imani ni mambo ya kawaida hakuna linalofanyika. Watu wanajenga wanapotaka, pa kujengwa nyumba hapajengwi, pale pa kulima ndio panajengwa almuradi hatuna utaratibu, hatujui tuseme nini.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais analisemea sana suala la kubadilika. Hebu jamani tubadilike. Lakini kwa sababu ni mwenye busara sana, ninadhani afikie pahala atumie meno yake, vyenginevyo tutaendelea kubaki nyuma, tutaachwa kwenye suala la maendeleo Zanzibar tutaachwa nyuma.

Sekta ya michezo ni ajira, ajira ya mtu mmoja mmoja, familia na taifa kabisa. Sisi tunapoteza tu vijana hivi hivi kwa ubinafsi tulionao. Hata kama mtu anaonekana huyu anafaa nayo kuna vurugu kupata hiyo fursa ni balaa hata afike. Watachukuliwa watu hata uwezo wao au sifa hawana, ubinafsi huu mpaka lini.

Mhe. Waziri haya ni mambo bado yapo na watendaji wako wapo wanatusikia. Tutakapoyaona yanatokea, maana yake ni makusudi yamefanywa, unyanyue kucha na wewe sasa. Niipongeze sana Tume ya Utangazaji kwa kazi nzuri na hasa pale matokeo yanapotokea lakini Mhe. Waziri bado tunaendelea kuwaombea vijana hao kwa kazi zao ngumu katika mazingira mazito, maslahi yao ni muhimu ili na wao wajisikie.

Haraka haraka Mhe. Mwenyekiti, niingie sekta ya utalii. Sekta hii ina kamisheni, ina chuo na Hoteli ya Bwawani. Dhamira kuu ya Serikali ya utalii ni suala zima la kuendeleza uchumi wa kitaifa, lakini dhana ya Mkuza ifikiwe. Mhe. Mwenyekiti, muda mrefu tunautumia na tunaendelea kuutumia kwamba bado Zanzibar hatujafaidika na sera hii ya utalii.

Sasa haitokuwa vyema kila inapofika kipindi cha bajeti tunakuja kuimba nyimbo hiyo hiyo. Nadhani ingefika wakati sasa tukaambiwa tumefanya lipi ili mtalii anapoondoka kwao Ulaya ama Uingereza ama China, tunaanza kufaidika mpaka anatua Zanzibar na mpaka ile siku anaondoka. Huu ndio utalii tunaohitaji wenye tija. Utalii huu wa kuja kumuuzia soda ameshafika Uroa na wale wanaouza bia, hatujafaidika sana sisi.

Lakini bado mtalii huyu mwekezaji apple bado anaagiza kutoka Afrika Kusini na samaki wakati bahari hii iliyotuzunguka. Hapana bwana haifai. Samaki kama wa baharini hatujafika, samaki wapo wa kufugwa huku juu ardhini. Kwenye sekta ya uvuvi tufike mahali watu wa Jambiani nyinyi mutatuletea changu tu, hawa huku pweza tu, ndio utalii tunaoutaka wa hii Mkuza.

Mama anayeweka mboga mboga achukue mboga zake apeleke hoteli pale soko liwepo. Ndio Mkuza utakwenda sambamba na utalii. Vyenginevyo tija kwenye utalii bado. Ni sekta muhimu tunaitegemea lakini bado mazao yetu ya viungo, mkazo ni upi kuhakikisha kwamba tunakwenda sambamba na sera hii.

Mazao ya kilimo, mifugo Mhe. Mwenyekiti, haya ndio maeneo yetu sisi hatuna kwengine. Ni lazima tuboreshe kwa namna ya kusindika mazao haya kwa kilimo na mifugo ili wananchi wetu wafaidike na hoteli hizo. Leo wananchi wanalalamika kuna hoteli na ardhi wameshaziuza na serikali haikusimamia katika hilo.

Leo imekuwa ni balaa tupu. Pakupita huko kwengine kwenda kwenye shughuli zao za kuzalisha hawana, makuta ya mahoteli yamesongamana. Ni makosa yalitokea lakini sasa tusiendelee kufanya makosa. Tujifunze kutokana na makosa hayo.

Mhe. Mwenyekiti…

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika 5 za ziada.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Ninamaliza sana kwa jitihada kubwa.

Mhe. Waziri hebu *inshaalla* utakapokuja kuhitimisha, niwaombe waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili waendelee kuichangia hii Wizara, wenye mashaka watoe, mwa kusukumwa Mhe. Waziri asukumwe, mwa kuulizwa kwa kasi aulizwe na hatimaye tumpitishie hii pesa. Mhe. Waziri wa Fedha tunakwambia kwamba pesa ni kidogo, mambo aliyokuwa nayo Mhe. Waziri ni mengi makubwa na ni muhimu. Tunakuomba uitizame hii wizara kwa jicho la huruma, jicho la mafanikio. Kupata kwake ndio kupata kwetu. Sera ni nzuri, utekekezaji uende sambamba na dhana iliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, ndugu yangu Wizara ya Fedha nasema amethubutu na ninadhani ataweza. Sasa katika kusonga mbele ampe hizi pesa zote anazohitaji Mhe. Said Ali Mbarouk.

Baada ya kusema hayo ninakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe sasa ninamshukuru Mhe. Jaku kwa dakika chache kama ulivyoomba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mwanzo kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Allah subuhana wataallah aliyeniwezesha hapa nikasimama na nikaweza kupumua kwa muda huu. Huu si uwezo wangu wala nguvu zangu au akili yangu. Hii neema yake Subuhaana wataallah.

Vile vile sina budi kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii kuchangia mawili matatu. Kama kawaida nilivyokuomba nitachukua kama dakika zangu tano ama sita.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri ni Waziri wa mwanzo kumfahamu mimi kwa kipindi kifupi tu kukaa katika sekta ya michezo akaweza kuleta mabadiliko ya haraka kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya. Tumeshuhudia timu yetu ya taifa ya vijana ilivyofanya kipindi kifupi tu na akafika waziri wa mwanzo akatoa ahadi kwa wachezaji kuwapa vespa. Sijapata kumuona hata waziri hata mmoja kwa kitendo hiki. Vile vile tumeshuhudia timu ya Mafunzo yake ikafanya ubabe wake katika Kombe la Kagame. Hizi zote ni nasaha na pongezi za Mhe. Waziri kutokana na malezi mazuri

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitahitaji maelezo ya kina vile vile kuhusu timu ya Malindi ya Zanzibar mpaka leo inapigwa tikitaka na danadana haijapangiwa ratiba. Ni sababu gani Mhe. Waziri timu hii wakati imeshagharimika kwa muda mrefu. Hapa Mhe. Waziri naomba unisaidie mchezo ni gharama na sisi tunatoka katika michezo, imegharimika kwa muda mrefu timu ya Malindi ikidai haki zake kila kona, mwisho wake ikaangukia Mahakamani. Kuna chombo zaidi ya Mahakama Mhe. Waziri na ukilinganisha Zanzibar inaendeshwa kwa misingi ya utawala bora. Kitengo hiki kinaleta sera gani kitaifa Mhe. Waziri.

Baada ya hapo nitoke nielekee Mhe. Mwenyekiti, katika sekta ya habari. Ninahitaji maelezo ya kina Mhe. Waziri Serikali ya Zanzibar inashindwa vipi kupeleka waandishi Bungeni ambapo Wajumbe wako wamekuwa wakilalamika kuwa Wabunge waliopelekwa kule hawafanyi kazi. Sasa kama kula hawajaenda waandishi kuja kutanganza huku, ndugu zetu wa Bara hawahitaji

maendeleo yetu. Tumekuwa tunapigwa mzigo sisi Wabunge. Waandishi wote utakuta Bungeni wakifanya kazi hizo. Sasa tunachozungumza sisi hakifiki huku na hakijulikani. Kwa nini wasipelekwe waandishi. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa nitahitaji maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nielekee kwenye sekta ya utalii ukurasa wa 42. Mhe. Mwenyekiti, sekta hii ina umuhimu mkubwa lakini bado kasoro kubwa katika usimamizi wake hasa ukusanyaji wa mapato. Mhe. Mwenyekiti, mfumo wa ukusanyaji mapato yake huu umeshapitwa na wakati kwa kuangalia vitanda tu.

Sasa hivi kunahitajika vitu muhimu kwa kuangalia mapato kutokana na vitanda kuwa wageni wangapi wamekuja, hapa kuna mtihani. Lazima tupate database, sehemu ya uwanja wa ndege na sehemu ya bandarini, tukajua wageni wangapi wameingia katika ukusanyaji wa mapato.

Halafu kuna mchezo wa kukatwa vichwa. Huu mchezo ambao si mzuri, mapato yanavuja sana hapa.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, kwa miaka mingi tulikuwa tukipokea takwimu za watalii wanaoingia nchini lakini hatuambiwi mapato yanayopatikana. Nitaomba Mhe. Waziri akija hapa anieleze watalii wangapi wametembelea Zanzibar mwaka jana na kiasi gani cha mapato kimepatikana. Kwa vile ni mataifa gani yanaongoza katika sekta ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha jengine kuna sera ya utalii kwa wote inalenga kulinda na utamaduni na kuendeleza sekta ya utalii. Jee, serikali inachukua hatua gani ya kudhibiti biashara ya ukahaba unayofanywa na wanawake kutoka nje ya Zanzibar ambayo imekuwa kero sana kwa watalii wetu. Hii Mhe. Waziri nitahitaji maelezo ya kina ukahaba umekuwa mwingi kwa wanawake kuwafuata watalii.

Nikitoka hapo nije katika hoteli ya Bwawani kwenye ukurasa wa 57. Mhe. Mwenyekiti, hoteli hii imebeba jina la historia ya Zanzibar hii kwa kuzingatia hoteli ambayo ni yenye status kubwa. Hoteli hii inakabiliwa na uchakavu mkubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, ukiingia ndani utakuta mende, vyoo vyake kule Pemba Bar havitaminiki, hata wanachotumia ZFA. Kwa hapa Mhe. Mwenyekiti, nitahitaji maelezo hata usafi huu unahitaji bajeti kiasi gani maana yake.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nitahitaji makampuni mangapi yaliyopangisha jengo lile na akina nani na kwa thamani ya shilingi ngapi. Lile jengo lina kodi nyingi tu mule kwa hivyo nitahitaji.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko mengine kuhusu gazeti letu la Zanzibar Leo. Kuna vijana wapo karibu miaka minne pale hawajapata ajira mpaka leo wakiwa wanahangaika tu, wanakuja watu nyuma yao wakaajiriwa kwa kisingizio cha digrii na diploma. Hapa Mhe. Waziri nitahitaji maelezo. Vile vile wanakisiwa shilingi laki moja kwa mwezi, kweli pesa hii itakidhi kuendesha maisha haya Mhe. Mwenyekiti.

La mwisho kuna michezo yetu Mhe. Mwenyekiti, inapoteza thamani yake hatuioni, kama mchezo wa ng'ombe Pemba sasa hivi umekuwa adimu sana kuonekana kisiwani Pemba. Kuna mchezo wa *kick boxer*, huu mchezo hauna tofauti Serikali umeupiga marufuku sijui kwa sababu gani. Mchezo wa judo na karate una tofauti gani na mchezo huu. Hapa nitahitaji maelezo kabisa.

Hata akisema na kukaribia kulia basi kuna jambo. Hapa Mhe. Waziri nitahitaji maelezo ya kina kabisa kwa nini kuna mchezo wa *kick boxer* ukafutwa wakati kuna mchezo wa judo na *karate* unaendelea.

la mwisho kabisa alilozungumza ndugu yangu Mhe. Jussa wa Jimbo la Mji Mkongwe, kwa masikitiko makubwa na kwa unyonge na kwa kutilia maanani mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, kwa sauti ya chini kabisa Mhe. Waziri, pale sasa hivi Ngome Kongwe imekuwa balaa kweli kweli. Nakuomba ufuatilie.

Sasa tulipigia kelele kuhusu vitendea kazi kwenye mnara uliopo pale *signal tower*, hawana vitendea kazi. Leo panapigwa ngoma pale, kuna meli inataka kuingia, mawasiliano hawapati *signal tower* hajui amfahamishe vipi. Mhe. Waziri hili sitoona uvivu kwa hili nitaungana na mheshimiwa ndugu yangu Mhe. Jussa.

Kuna meli zinapata shida ya mawasiliano kutokana na disco na ngoma zinazopigwa pale, majirani kutopata nafasi ya kulala. Halatu tunaambiwa Mji Mkongwe unalindwa mambo chungu nzima. Huu ndio Mji Mkongwe kweli unaolindwa kuna bughdhi watu, wale watu hawana haki katika nchi hii. Hapa Mhe. Waziri hapana msalie Mtume ndugu yangu, panapouhai ikifika kwenye majuumuisho utanieleza kwa kina kabisa, kwa sababu wananchi wanateseka, maisha ya watu yamekuwa reheni, vitendea kazi signal tower hawana. Sasa wanakwenda kwa kubahatisha tu, wasubiri ngoma ipungue ili meli iingie gatini. Kwa hapa Mhe. Waziri naomba unipatie jawabu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache sitounga hoja mpaka nitakapopata maelezo ya kina.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe idadi ya wachangiaji mpaka hivi sasa tuliyonayo ni kubwa mno, lakini muda wetu hauturuhusu.

Nawaombe basi Waheshimiwa Wajumbe wale ambao watakosa kuchangia kwa kusimama na kutoa maelekezo yao hapa, watoe mchangio wao kwa kumuandikia Mhe.Waziri ili atakapokuja kutoa majumuisho hiyo kesho aweze na wao kuona jitihada zao vile vile.

Labda niwataje tu baada ya Mhe. Jaku kumaliza ni nafasi ya Mhe. Wanu ambaye ataendelea, baada ya Mhe. Wanu ataendelea Mhe. Hamza, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Farida Amour Mohamed, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Abdi Mosi, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Viwe Khamis, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Abdalla Mohamed Ali.

Tuendelee na Mhe. Wanu.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Lakini pili Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hotuba kwa ufanisi na umakini mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitapita haraka haraka ili angalau ni-save dakika 10 na mwenzangu apate.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia naomba nianzie na Shirika la Utangazaji. Shirika hili katika malengo ambayo walipaswa kutekeleza walisema kwamba, "Kuimarisha usambazaji wa habari kwa kufungua ofisi Dar es Salaam".

Mhe. Mwenyekiti, *out come* ya lengo hii ni kwamba mafanikio yamepatikana kwa upande wa redio tu kwamba *ZBC* Redio imepata mafanikio kwa kufungua ofisi hii na kwamba ikiwa ni pamoja na kipindi cha kutoka magazetini ambacho kinarushwa kupitia *ZBC*. Nilikuwa ninamuuliza tu Mhe. Waziri kwamba jee, kwa upande wa *ZBC TV* kuna mafanikio yoyote ambayo yamepatikana kupitia ofisi hii iliyofunguliwa Dar es Salaam na kama hakuna jee, wizara ina mpango gani kwamba wa kuhakikisha kuwa ile ofisi iliyofunguliwa inanufaisha shirika lote, kwa maana ya kamba *ZBC* Redio na *ZBC TV*.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, nalipongeza shirika kwa kumpata mtaalamu kwa kutumia lugha za ishara. Lakini nilikuwa na swali tu dogo kwa Mhe. Waziri kwamba ni sababu zipi zinazopelekea kwa mtaalamu huyu hatiwi siku hizi katika televisheni. Kipindi cha nyuma tulikuwa tunamuona kwamba yupo pale pembeni upande wa kulia anakuwepo lakini baada ya hicho kipindi alipotea ndio kwanza ninamuona leo katika usomaji wa bajeti hii.

Kwa hivyo nilikuwa ninamuuliza tu Mhe. Waziri kuna sababu zozote ambazo zinapelekea kwamba huyu hayaekwi na kufanya hivyo haoni kuwa wanawatengwa walemavu wasiona na wasiosikia.

Hapo hapo Shirika la Utangazani Mhe. Mwenyekiti, ninakumbuka katika bajeti iliyopita tuliwaombea hawa wafanyakazi wanaofanya kazi wanaorusha vipindi katika Baraza letu, hawa waandishi wa habari wanaochukua *moving camera*. Tuliwaombea kwamba hawa anagalau kuwe na posho wanapewa kwa sababu hawa wanashinda kutwa, asubuhi, mchana na sisi, jioni tukirudi wapo hapa, wanachezea baridi kama tunavyoichezea sisi. Kwa hivyo tuliwaombea kwamba Mhe. Waziri awafikirie angalau kuwe na posho maalum ambao hawa wawe wanapewa.

Sasa ninamuomba Mhe. Waziri akija kufanya majumuisho aje atwambie, jee kuna posho maalum ambalo wametengewa kwa sababu kama sisi tunavyoshindwa hapa na wao wanashinda hapa kutwa nzima. Nikimaliza hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba niingie sekta ya utalii.

Sekta ya utalii mimi niseme tu hapa kwa ujumla kwamba nilikuwa ninaiomba Wizara ijishajihishe utalii wa ndani. Ninakumbuka kuna siku nilimuuliza Mhe. Naibu Waziri swali kwamba wizara imejipanga vipi kuona kwamba inashajihisha utalii wa ndani na tusiwe sana tunategemea watalii kutoka nje ili wenyewe wazalendo iwe angalau mara moja au mbili mtu anafanya utalii wa ndani.

Mhe. Naibu Waziri akanijibu kwamba sera ipo. Lakini nilikuwa ninauliza kwamba utekelezaji wa sera hiyo umefikia kiasi gani au una mafanikio gani yamepatikana katika kushajihisha utalii wa ndani.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naomba niingie kwenye Hoteli ya Bwawani. Mhe. Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Mhe. Mwenyekiti, ninaipongeza sana kwa hatua iliyofika hoteli hii. Mhe. Mwenyekiti, kuna msemo unaosema kwamba, *a journey of thousand step* inaanza na *one step.* Kwa kweli hoteli hii imeshaanza kunyanyua mguu, hiyo *one step* imeshaanza.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa anawasilisha alitwambia kwamba mwaka jana hoteli hii ilitakiwa kujitegemea wenyewe. Ninashukuru kwamba katika lengo alilojipangia hoteli hii atleast wametimiza asilimia 85 ya lengo ambalo wamejipangia. Hii ni hatua kubwa ambayo wameichukua Mhe. Mwenyekiti.

Pia Mhe. Mwenyekiti, sisi waswahili tuna dhana kwamba mtu hata afanye mema mangapi, lakini baya moja huharibu yale mema yote aliyoyafanya. Nilikuwa nasema hivi kwa sababu hoteli ya Bwawani kuna malalamiko ya wafanyakazi. Kwa hivyo, niwape ushauri tu uongozi wa hoteli ya Bwawani kwamba pamoja na mema yote ambayo wamefanya, lakini wahakikishe kwamba maslahi ya wafanyakazi wanayasimamia na kwa kuwa wameweza kujiendesha wenyewe, basi nina hakika kwamba hawashindwi kusimamia maslahi ya wafanyakazi na naamini kwamba hili litatatuka.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo hoteli ya Bwawani, naomba niingie katika Kamisheni ya Utamaduni na Michezo. Mhe. Mwenyekiti, katika hili naomba niipongeze timu ya walemavu wa akili iliyoshiriki katika mashindano ya *Special Olympic* yaliyofanyika Athens. Timu ambayo Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa chini ya uangalizi wa mwanamama, na amefanyakazi nzuri sana na hatimaye wamerudi nyumbani na medali ya dhahabu. Kwa hivyo, nampongeza sana mwanamama huyu, kwani wangapi hapa wanaondoka kwenda kwenye mashindano, wanakabidhiwa bendera na wanarudi na bendera tu hawarudi na chengine chochote, kile walichokabidhiwa ndio wanachorudi nacho. Lakini namshukuru mwanamama huyu wamekwenda Athens ametuosha uso, angalau Zanzibar nayo imerudi na medali ya dhahabu.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze mtoto yule ambaye ameshiriki mashindano hayo ni mlemavu wa akili. Lakini ametuwakilisha Zanzibar ipasavyo. Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuombe Mhe. Waziri kwamba walimu wa timu hizi za watoto walemavu, namaanisha marefa wale, kwamba wawe wanawaangalia kwa jicho la huruma Mhe. Mwenyekiti, kocha ambaye anafundisha watu wenye akili zao na kocha ambaye anafundisha timu ya watoto wenye ulemavu wa akili ni tofauti, wale watoto wana uangalizi wa ziada ambao huyu kocha anatakiwa pia atowe. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri awaangalie walimu wa wanafunzi hawa kwa jicho la huruma sana na kama kuna maslahi ambayo walimu hawa wanapatiwa, basi yale ya wanaofundisha watoto wenye ulemavu basi yawe tofauti na yale ya wale wanaofundisha watoto wenye akili zao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nilisema mwanzo kwamba na-*save* muda ili na wajumbe wenzangu angalau wawili au watatu wapate naunga mkono hoja, ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nataka na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nizungumze machache kabisa katika Wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme

kwamba katika bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa upande wa televisheni na redio, kuna vitu naweza kuvikataa. Tunashangaa wananchi wetu leo wanatuambia mbona hatuwaoneni, leo hampo hewani, tunaambiwa umeme umezimwa Masingini, jenereta ipo lakini haifanyikazi. Sasa nadhani Mhe. Waziri hii ni kasoro kubwa sana, tutakuja kuhitaji maelezo ya kutosha. Kwa sababu vyombo vya habari ndio kitu ambacho kinatakiwa kithaminiwe katika nchi na kwa bahati nzuri serikali yetu tumeanzisha Wizara ya Katiba na Sheria na Utawala Bora. Moja katika sifa ya utawala bora ni uwazi, uwazi bila ya vyombo vya habari uwazi utapatikana wapi.

Mimi nadhani Mhe. Waziri leo ungechunguza kila pahala ukahakikisha kwamba leo wizara yako inazungumzwa, basi kila pahala uwe umejitayarisha. Lakini nataka niseme kuna baadhi ya watendaji wanatuvunja moyo. Sasa kama ilivyokuwa sisi hatuko tayari sasa hivi mtu yeyote kutuharibia, basi na wewe uwe mkali ili mtu yeyote asiweze kukuharibia. Mhe. Mwenyekiti, nitakuja kuhitaji maelezo ya kina kwa nini wananchi wetu leo wamekosa haki yao ya kupata habari.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niwapongeze sana Baraza la Habari kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini bado Mhe. Waziri katika bajeti ya mwaka jana nilisema kwamba wenzetu wameleta mapendekezo yao Serikalini, wameisaidia kazi Serikali wakaleta mapendekezo yao ya mswada wa habari, basi mpaka leo mswada ule umekaliwa Wizarani.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe jawabu kuhusu mswada wa habari na wa haki ya kupata habari. Kwa sababu mwananchi kama hawezi kupata habari atapata wapi habari, kwa sababu kila kitu kinatakiwa kiwekewe sheria. Sasa nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, atakapokuja Mhe. Waziri aje anipe ufafanuzi vipi ule mswada wa sheria ya habari uko wapi, kama hajajitayarisha basi sisi kwa kushirikiana na wadau wa habari tuko tayari tutauandaa mswada ule tutauleta ili tuweze kupata haki ya kupata habari. Wananchi wetu wanahitaji habari na wanahitaji ukweli na uwazi.

Mimi nataka niwapongeze wenzetu kwa upande wa Tanzania Bara. Wenzetu sasa hivi wamepiga hatua, hatua iliyopigwa baada ya kufa yule msanii Kanumba, sasa hivi wamejaribu kurekebisha sheria ya hati miliki. Nadhani na hapa kwetu ipo, mimi nafikiri tuifanyie maboresho zaidi.

Vile vile waziri siku ya maziko yale alikwenda akatoa kauli kwamba atahakikisha mswada wa habari unaletwa ndani ya Bunge, nadhani sasa hivi wako katika hatua ya mwisho. Mhe. Waziri mimi nakujua wewe ni mtu makini umeshawahi kuwa mjumbe wangu wa kamati ya uchumi na fedha, tumeshasafiri nje ya nchi na tumeshaona wenzetu wanavyofanya katika mlalamikaji mkubwa ulikuwa ni wewe, mimi nikiwa Mwenyekiti wako. Sasa hivi nataka nione ule umahiri wako. Mhe. Mwenyekiti, mambo haya watu wanasema, leo uko mbele kesho uko nyuma, watu ndio wanavyokwenda.

Kwa hivyo, wala msione kwamba sisi tuliokuwepo huku nyuma tumenuna, tunataka huko mbele sasa mfanyekazi kama ile tuliyokuwa tukifanyakazi pamoja. Mhe. Waziri naamini utatujibu na Mswada wa Habari tunategemea katika Baraza linalokuja tunategemea mswada huu utakuja.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwa upande wa maslahi. Mhe Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri, bajeti yetu hii tunajua ndio tumeshaipitisha na tukishapitisha katika fungu katika Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, basi huna ujanja mwengine wa kuweza kuboresha. Lakini bado naomba uangalie *scheme* ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na waandishi wa habari ili maslahi yao yaweze kuongezwa.

Mhe. Waziri kama kuna fungu lolote ulililoficha humu basi naomba na kama kuna vifungu ambavyo waheshimiwa wameviona ona tukifanyamarekebisho basi kitu cha mwanzo tuangalie maslahi ya waandishi wa habari. Mhe. Waziri haipendezi kumuona mwandishi wa habari kila siku suti hiyo hiyo ndio anayosomea taarifa ya habari, suti hiyo hiyo katika sherehe mbali mbali. Hao wanatakiwa tuwajenge ili na wao wajisikie wawe na hamu ya kutoa habari. Leo waandishi wetu wa habari wamekuwa kama omba omba, ukiwa na taarifa tena, tuchukuweni.

Sasa leo Mwenyekiti, unapokuwa na sherehe unakwenda unam-*tip* mwandishi wa habari, atakuja kuandika maneno ya kwako wewe na sio ile *action* iliyotokezea pale. Mwandishi wa habari anavyotakiwa, hata mimi kama nimemchukua jimboni kwangu, wananchi wamenisema vyengine, basi waseme vile walivyosema wananchi, sio ninavyotaka mimi. Lakini kama waandishi hawa hatukuwajenga basi mimi naamini wataendelea kuchukua *tip* na watakuwa wanatumiliwa. Sisi tunataka waandishi wasiwe watu wa kutumiliwa, tunataka wawe watu ambao wana uwezo wa kutoa habari kama vile taaluma yao inavyosema.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nije kwenye upande wa redio. Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna tatizo, mwenyekiti katuambia tusirudie rudie, lakini mimi katika mtu ambaye nitazuwia fungu kwa upande wa redio ni mimi. Mzee Jumbe alipoanzisha Baraza la Wawakilishi alisema hii ngome ya wananchi. Ngome hii ya wananchi mpaka yule mnyonge wa mwisho ambaye chakula cha leo hakijui, sisi ndio watetezi wao.

Mhe. Mwenyekiti, kuna vijana wetu mnawatumia na wanaandika habari siku nyingi. Kwanza nataka nianze na watu wa mawio, sijui watu wa mawio kama mna mikataba nao au wanakuuzieni tu habari. Hili tulikuwa tunataka tujuwe, kwa sababu tunajua wanafanyakazi nzuri, wanatoa taarifa mbali mbali na wanatusadia pia.

Vile vile taarifa za mawio, huwa wanatoa taarifa za wananchi wetu wanaotukosoa mpaka na sisi. Kwa hivyo, wanafanyakazi nzuri, kwa sababu isiwe sisi tunasema tu na sisi tusisemwe, tunapokosea tusemwe, ndio kama hukusemwa huwezi kujirekebisha. Kwa hivyo, mimi naomba nijuwe kama waandishi hawa wana mikataba au vipi. Hivi sasa kuna waandishi pale redio wamefanyakazi wengine miaka mitano, wengine sita na wengine saba.

Sasa hivi tayari imekuja ajira tayari wakubwa wanaanza kutafuta watoto wao, wale waliokuwepo pale zaidi ya miaka mingapi wamewekwa. Leo mtu keshafanyakazi miaka saba pale, anataka kuajiriwa anaambiwa afanyiwe *interview*. Eeh! Kama huyu kafanyakazi miaka saba kama hamjaridhika naye hamjamuondoa tu. Kwa hivyo, mimi nadhani kama kuna suala la *interview*, sawa. Lakini hebu tuangalie mtu keshakuleteeni habari, keshawaandikieni habari, keshakwenda kuchukua habari zaidi ya miaka mitano. Maana yake ile kuleta habari peke yale na kuzipokea habari zake na mkazitoa ile tayari ni *interview*.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi nakujua, nimeshafanyakazi na wewe sana ni mtu mchapakazi mzuri, hupendi kulaumiwa kwa mambo madogo madogo. Kwa hivyo, na hili naomba ulichukulie hatua. Hivi sasa wameshafanyiwa *interview*, lakini wanaambiwa tunalisubiri Baraza ili tutowe matokeo. Baraza hili ndio linasema matokeo hayo ya *interview* hayatolewi, kwa sababu kuna ubaguzi mmeshaufanya. Leo Mhe. Waziri hapa mpaka kieleweke, tujuwe kwanza katika kipaumbele kwenye ajira waangaliwe wale waliokuwepo kwa muda wa miaka mingi. Mhe. Mwenyekiti, hili nilisema nitowe angalizo mapema, ili baadae tusije tukabuburishana huko mbele.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka niende katika vyombo vya habari binafsi. Mhe. Mwenyekiti, vyombo vya habari binafsi vinalalamika kuhusu mashirikiano na wizara yako yapo lakini hayajatosheleza. Vyombo vya habari Mhe. Mwenyekiti, ukishapewa kuwa wewe ndio waziri unayeshughulikia masuala ya habari, sio ya serikali tu, yote unatakiwa vile vile uvisimamie viende katika utaratibu mzuri, uhuru wao wanapodai ukae na uwasikilize ili vyombo hivi viweze kuridhika. Naomba katika hili wala sipigi buti lakini nasema uwe karibu na vyombo vya habari ili shughuli zao ziweze kwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, tunawashukuru sana vyombo vya habari binafsi, kwa sababu vinasaidia kutoa taaluma, vinasaidia vile vile kutoa ajira. Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa zamani Sauti ya Tanzania Zanzibar na TVZ basi, lakini hivi sasa vijana wetu tunashukuru kuna vyuo vingi, hata sisi CCM pale Mkoa tumeanzisha Chuo cha Uandishi wa Habari, tunashukuru vijana wetu wameajiriwa katika vyombo mbali mbali vya binafsi, tunawashukuru sana vyombo binafsi na waendelee na moyo wao kama kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile TVZ. Mhe. Mwenyekiti, katika matunda ambayo tunatakiwa tuyaenzi ni matunda yale ya waasisi. TVZ Mhe. Mwenyekiti, kwa pande wa Afrika kama sikosei, nadhani nchi ambayo ilikuwa mstari wa mbele katika uhuru wa habari, maana yake mpaka TV tena tulikuwanayo ya rangi. Lakini hivi sasa ukenda Karume House bado hali hairidhishi. Tunataka Karume House, kama jina la Karume tunavyomsifu siku zote kwamba kakomboa nchi na alisimamia utawala wake ndani ya miaka minane, nchi ilikwenda kama mshare kwa maendeleo. Tunataka Karume House, jina lake lilingane na Karume House. Leo tunasikitika kwamba waandishi wetu pale, pakiwa na sherehe mbili tu basi kamera hawana.

Mhe. Mwenyekiti, juzi pametokea matukio ya kuzama kwa meli, basi hawana kamera ile ya moja kwa moja ambayo inaweza kurusha vitu moja kwa moja, wanaazima azima kamera. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kwanza tunashukuru Serikali yetu ilifanya jitihada, tulikuwa hatuna kamera, wametafuta kamera za *digital*. Kwa hivyo, mimi naomba katika kila mwaka tuhakikishe tunaongeza kamera ili taarifa zetu ziweze kupatikana wakati wowote.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuanzisha ile masaa 24 ya televisheni ya Zanzibar. Tulikuwa tunaomba hata hivyo vipindi vya usiku visijekuwa tena ni vile vipindi vya vibindankowe vya usiku usiku. Tunataka vipindi vya usiku viwe vya taaluma zaidi, msije kutuwekea tena vipindi vile vya mstari mdogo ule, aaah! Ile kidogo tutakuja kuwa haturidhiki.

Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza sana Mhe. Waziri kwa jitihada zao hizi na nawaomba muendelee. Vile vile kuhusu gari la matangazo, ingawa siku hizi kuna TV katika kila maeneo,

lakini bado gari la matangazo ni muhimu, kwa sababu kuna *function* mbali mbali za kitaifa, wakati mwengine kuna shughuli zetu pale uwanja wa amani, wananchi wanakuwa wameshaingia wengi ndani ya viwanja. Ukiacha lile gari, tuwe na ile *screen* kubwa ambalo linaweza kuonesha hata wakati wa mchana wa jua, tulikuwa tunaomba sana Mhe. Waziri TVZ uweze kuwaboresha ili waweze kutoa habari na matangazo yao kwa muda wowote na pahala popote.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la ukarabati wa hiyo studio ambayo inataka kujengwa. Mhe. Waziri naomba kaa na Mama Maryam Hamdan. Kuna Muingereza mmoja alikuja kufanya utafiti na Muingereza huyo alikwenda katika nchi zote za Bara la Afrika, akagundua katika Afrika nzima ni nchi mbili tu, Zanzibar na Ghana ndio wenye jengo ambalo lina studio ambayo inaweza ikarikodiwa muziki pahala popote duniani, ukatoka kama umerikodiwa Ufaransa au Uingereza.

Mhe. Mwenyekiti, jengo hili tumepata wenzetu Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, wametujengea pale kwa msaada, lakini jengo lile haliridhishi sasa hivi. Lakini tunaomba ile studio waliotujengea wenzetu wa China, isifike pahala wakaja kutuona Wachina kwamba hawa kazi yao ni kuomba tu, lakini mbona kuendeleza hawaendelezi.

Kwa hivyo, naomba hiyo studio kama haijaanza kujengwa basi muiangalie studio ile na ripoti kaweka. Leo kwa bahati mbaya nimeitafuta, nina ma- *document* mengi sikuipata, lakini nitajaribu kuitafuta, lakini nadhani yule mama anayo akupe ile ripoti. Sasa kama leo ile studio ya Zanzibar, ndio unaambiwa katika Bara la Afrika ndio moja kati ya nchi mbili Ghana na Zanzibar peke yao. Sasa leo tunapokwenda kutengeneza studio nyengine, mimi nadhani ni kutumia fedha za umma vibaya.

Kwa hivyo, mimi nadhani mujaribu kuiangalia studio hiyo hiyo iliyojengwa na Wachina, kwa sababu tunaambiwa Zanzibar Leo wamehamishwa, wamepelekwa katika vijichumba sijui vinne tu, lakini kama tunalo jengo letu kwa nini tusilitumie hilo. Mhe. Mwenyekiti, nadhani suala hili naomba ulichukulie hatua za karibu ili tuweze kupata kitu ambacho kilicho bora.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa habari nimejitahidi na nafikri nimesema sana. Nakuja katika michezo. Kwanza nataka niwapongeze wanamichezo wote wa Zanzibar, kuanzia mpira wa miguu, riadhaa, *basketball*, *cricket* na kila michezo pamoja na *kick boxer*. Mhe. Mwenyekiti, naomba mchezo wa *kick boxer*. Mhe. Mwenyekiti, nataka niwaambieni kitu kimoja, hebu siku moja hapa, tena siku moja tulisema hapa, kuwa tuweke ukumbi hapa tukufundisheni. *Kick boxer* mtu akipigwa haumii bwana, kwa sababu ukishakuwa na mazoezi, wewe mtu akikupiga unaona raha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba, Mzee Karume kweli aliukataza mchezo wa ngumi, lakini ule mchezo wa *kick boxer* hakukataza. Mzee Karume alikataa yale magumi tu ambayo unavaa ma- *gloves* yale, lakini *kick boxer* hakukataza na hakuna sheria yoyote iliyokataza mchezo wa ngumi. Mimi nadhani Wazanzibari ni katika watu hodari kwa kupigana na kupambana na historia yetu tulipindua hapa kwa ngumi tu, ndio. Sasa leo vijana wetu wameshafika Japan, Korea na kila pahala wanachukuliwa. Pamoja na kwamba sifa inakuja Tanzania. Lakini bado mimi naomba mchezo huu tuutambuwe.

Mhe. Mwenyekiti, moja katika sekta ya utalii *kick boxer* inaleta utalii, mchezo huu unapendwa duniani. Leo yule kocha wangu Shumaika pale Kariakoo, yule alifanya jitihada ya kuanzisha ule mchezo wa Judo, katuletea vifaa chungu nzima kutoka Japan, aliwachukua vijana wengi wa Kizanzibari kawapeleka Japan. Vijana wa Kizanzibari ukiangalia katika michezo hii ya Afrika ya Mashariki na Kati, siku zote vijana wa Zanzibari ndio wanaokuwa na ushindi wa mwanzo, kwa nini michezo hii tunashindwa kuitambua.

Mhe. Mwenyekiti, nikiwa mimi mmoja kati ya wapiganaji wa *kick boxer,* leo hapa bajeti hii kama hujaniambia kwamba mchezo wa *kick boxer* utatambulika, katika kifungu cha michezo mimi sitoipitisha kabisa, haiwezekani. Leo tunazungumza ajira, *kick boxer* ni ajira. Mimi nataka niwaulizeni ni nani kazikwa hapa Zanzibar kwa kupigana *kick boxer*, hajazikwa mtu, kwa sababu mchezo ule kwanza unafundishwa kupiga na kukinga. Mhe. Mwenyekiti, kama ingekuwa mtu akipigwa *kick boxer* anakuwa hendi tena, basi mimi nadhani vijana wetu wote wangekuwa wameshakimbia. Watu wa zamani wanasema ‘meno ya mbwa hayaumani’, mbwa ukiwakuta wanatafunana ndio mchezo wao ule. Sasa hawa *kick boxer* ule ndio mchezo wao kupiga na kupigwa. Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la michezo. Hapa nilisema niseme sana kwa sababu nitakuja kuwa mgumu sana katika idara hii ya michezo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la uwanja wa amani. Tunaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetujengea uwanja mzuri wa amani, lakini *pitch* mbovu. Wale Simba na Azam juzi, msifikirie mchezo, wale wanawanunua wachezaji kwa gharama kubwa. Mimi siku ile niliyocheza pale uwanja wa amani Mhe. Mwenyekiti, nilipigwa *push* nikaanguka wiki nzima nilikuwa nauguza gwaru. Tunataka vijana wetu wakishafunga goli wanaogelea pale *fyaaaa* kwenye majani. Leo pale ukianguka tu basi moja kwa moja Hospitali ya Mnazi Mmoja mabendeji tele.

Kwa hivyo, mimi nadhani wale waliokimbia pale msifikirie masihara, uwacha wetu kwa kweli ni mzuri, lakini *pitch* mbovu na pale tatizo letu ni maji. Kuna kipindi tuliwahi kusema kwamba pale kiwanjani pachimbwe kisima, tukaambiwa kisima kipo. Leo kama kisima kipo, uwanja ungekuwa mkavu kiasi kama kile. Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri, mimi namjua ni mfuatiliaji sana, nafikiri atajaribu kufuatilia. Kama hatuwezi uwanja ule kuutia maji ukaweza kuwa katika hali nzuri, basi pamoja na kwamba sio wanachama wa FIFA Zanzibar, basi tuwaombe hao wenzetu shirikisho la soka TFF katika hiyo misaada wanayoletewa, wakiletewa lile jora la majani bandia na sisi watuletee, tukaweke pale ili uwanja wetu uendelee kuwa wa kimataifa ujulikane kabisa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Zingatia muda Mhe. Mjumbe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya. Mhe. Mwenyekiti, namalizia malizia. Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima la upande wa mahoteli. Tunawashukuru sana wenzetu wawekezaji na hasa wazalendo waliowekeza katika sekta ya utalii. Jana Maalim Haroun alitoa takwimu na takwimu hizo za hoteli nyingi zilikuwa zinaonesha kwamba wenyewe ni wazalendo. Kwa hivyo, tunashukuru kwa ajira zinazotolewa katika mahoteli.

Lakini bado Mhe. Mwenyekiti, nitajaribu kumpa *copy* hapa ya barua kutokana na muda, kuna Kampuni hii inaitwa *Oraly Resort and my Blue Nungwi*. Hawa Mhe. Mwenyekiti, wanadaiwa na ma-*supplier* wetu. Ma-*supplier* wengi vijana wetu kama unavyojua ajira hawana, wamepeleka mizigo katika mahoteli mbali mbali. Kwa hivyo, hii ni kampuni ambayo ndio ina-*organize* katika kupeleka bidhaa zao kule kwenye mahoteli. Kwa hivyo, bado kuna fedha nyingi ambazo bado hazijalipwa, nitaomba *copy* hii ili baadae uweze kuifuatilia pamoja na Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, vyombo sekta ya habari bado ni changa kwa upande wa Zanzibar, hasa hizi binafsi. Tulikuwa tunaomba tu lile Baraza la Habari au ile taasisi inayosajili vyombo hivi wajaribu kuangalia tena zile kodi zao, kwa sababu kama tunavyoambiwa hapa wanatoza kodi kwa dola. Sasa leo Zanzibar tunatoza kodi kwa dola. Mimi nadhani tujaribu kuangalia. Kwa sababu mtu unatakiwa shilingi yako uipe thamani zaidi, ukianza kuruhusu watu kulipa kwa dola, labda katika zile sekta maalum, lakini mimi sijaona hii sekta ya habari ikawa katika suala zima la kutoza kodi kwa dola.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, ni ujenzi wa nyumba za ghorofa ambazo zinajengwa, halafu baadae zinageuzwa kama hoteli. Zimewekwa katika mitaa yetu ya ng'ambo. Mhe. Mwenyekiti, hizi kidogo zinaweza kuleta matatizo. Unajua nyumba zetu za ng'ambo ni tofauti na za siku hizi, kuna nyumba ya mbele, kuna uwa na uko kwenye uwa kuna choo, hivyo mambo yote yanafanyika uko. Leo mtu ananunua nyumba anajenga ghorofa halafu baadae mambo mengine yote anakuwa anayaona. Mtu anatoka usiku anajidai anachungulia, kumbe vile anaangalia nyumba za chini.

Vile vile hawa wanaonunua hizi nyumba. Kwa mfano kuna baa moja inaitwa Kwa Mzushi. Mhe. Mwenyekiti, ile ilikuwa ni baa, lakini baadae baada ya wananchi kupiga kelele baa ile ilifugwa, lakini sasa hivi imegeuzwa *guest house*. Lakini *guest house* yenyewe kuna malalamiko kwamba kunafanywa part time. Sasa hii nilikuwa naomba Mhe. Waziri ujaribu kuifuatilia, kama inafanywa *part time,* sio *short time* ni *part time,* basi mimi nadhani uifunge na akae yeye kama mwenye nyumba yake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache, mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura tunaikubali hotuba hii pale ambapo maslahi ya hasa wale vijana wetu wa Idara ya Habari pale watakapopata haki zao, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe, kwa mashirikiano ambayo mmenipatia kwa siku ya leo. Lakini kwa mara nyengine tena niendelee kuwaomba tena radhi wale wote ambao walikosa nafasi ya kusimama na kuchangia, lakini hii ilitokana na matatizo ya muda ambayo yalitukabili.

Vile vile naomba kuwatangazia na kuwakumbusha wajumbe wote kwamba leo ndio ile siku ambayo Mhe. Maalim Haroun Ali Suleiman, ametualika futari katika Ofisi yake na kila mjumbe nina imani kwamba amekwisha kukabidhiwa kadi yake. Ahsanteni sana, na *Inshaallah* nachukua fursa hii kuakhirisha Baraza hili mpaka kesho siku ya Ijumaa tarehe 27/07/2012 saa 3:00 za asubuhi. Ahsanteni sana

(Saa 8:30 Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 27/07/2012 saa 3:00 za asubuhi)